ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
41.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
42.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
43.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
46.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
50.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
52.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
54.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
57. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
61.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 8 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha kwenye meza yako hati ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: *Bismillahi Rahmani Rahym.* Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Mkaazi, Maji na Nishati ya Serikali ya Mapinduzi ya Mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 195

Uzalishaji wa Mafuta

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Kwa kipindi sasa dunia kwa ujumla imekumbwa na tatizo la upungufu wa chakula hasa bidhaa muhimu za nafaka zikiwemo mchele, maharage, mahindi, mtama na kadhalika. Upungufu huu wa chakula duniani unatokana na sababu nyingi zikiwemo zile za kiuchumi na za kimazingira, ikiwemo matumizi ya teknolojia ya kisasa kutengeneza mafuta ya kuendesha mitambo kwa kutumia nafaka.

(a) Kwa kuwa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (*FAO*) linaendeshwa kwa malengo na taratibu za kimataifa. Je, maamuzi yatokanayo na nafaka yanatokana na malengo na maelekezo ya *FAO*.

(b) Nchi kama Marekani imeanzisha kiwanda cha kuzalisha gesi ya *Ethanol (Ethanol plant)* kutokana na mahindi na mtama. Je, gesi hiyo ya *Ethanol* hutumiwa kwa matumizi gani.

(c) Zipo taarifa kuwa nchi ya China kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watu, imechangia sana upungufu wa chakula duniani kutokana na nchi hiyo kubadilisha mfumo wa chakula. Je, kama hilo ni kweli, Zanzibar kama sehemu ya dunia tunakabiliana vipi na changamoto hiyo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 195 lenye vipengele (a, b na c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) lilianzishwa mwaka wa 1945 kwa lengo la kuinua viwango vya lishe bora na maisha, kuongeza uzalishaji wa kilimo na kuimarisha hali ya maisha ya wakazi wa mashambani. Maamuzi yanayotokana na matumizi ya nafaka katika kuzalisha nishati za kibaolojia hayatokani na malengo na muelekeo wa *FAO*. *FAO* inalenga katika kupunguza umasikini na njaa kwa kuendeleza maendeleo ya kilimo, lishe bora na kutafuta kuwepo chakula cha kutosha. Mwelekeo wa *FAO* ni kufanya mageuzi ya kilimo kutoka kilimo cha asili cha kutumia zana duni na kufikia kilimo cha kisasa, kinacho tumia pembejeo na zana za kisasa, kinacholinda mazingira na *bioanuwai* na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mhe. Naibu Spika, Gesi ya *Ethanol* ni moja kati ya nishati za kibaolojia zinazozalishwa kutokana na mazao ya kilimo na kasi ya uzalishaji wake umekuwa ukiongezeka hivi karibuni. Gesi hii inatumika kama nishati mbadala ya mafuta kwa matumizi ya magari, mashine na vyombo vyegine vya moto. Miongoni mwa mazao yanayotumika kuzalisha nishati hii ni pamoja na mahindi, mpunga, miwa, mtama na ngano. Matumizi ya nishati hii mbadala yana nafasi kubwa siku za usoni kutokana na matokeo mazuri ya tafiti zinazoendelea kufanyika duniani. Tafiti hizi zimepelekea kuongezeka kwa ufanisi katika uzalishaji wa nishati. Kwa mfano, hapo kabla nafaka ndizo zilizokuwa zinatumika katika kuzalisha gesi hizi lakini hivi sasa mti mzima (majani, kigogo na nafaka) pia hutumika. Maendeleo hayo yanaonesha dhahiri mwelekeo wa kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi za kibaolojia duniani sambamba na kuongezeka kwa soko na bei za bidhaa hizi katika soko la dunia.

Ni dhahiri kwamba maendeleo ya kiuchumi katika Bara la Asia na Marekani ya Kusini ni miongoni mwa changamoto zinazopelekea kuongezeka kwa mahitaji ya chakula na upandaji mkubwa wa bei za vyakula duniani. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia nayo pia inakabiliwa na changamoto hizo kutokana na hali ya sasa ya kuwa na utegemezi mkubwa wa chakula kutoka nje ya nchi hasa mchele ambao ni chakula kikuu hapa nchini. Kwa wastani, Zanzibar inaagiza

tani 80,000 za mchele kwa mwaka huu ni sawa na asilimia 84 ya mahitaji yetu kwa mwaka huu.

Zanzibar inaelewa bayana athari za kuwa na utegemezi mkubwa wa chakula kutoka nje ya nchi na katika kukabiliana na hali hii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili ina mikakati ifuatayo ambayo tayari imeanza kufanyiwa kazi:

- Kuanzisha Hifadhi ya Akiba ya Chakula. Hifadhi hii itakuwa inaweka chakula cha akiba cha kutosheleza mahitaji ya miezi mitatu kwa kuanzia. Chakula hichi kitakuwa kinatumika pale kutakapokuwa na dharura au upungufu wa chakula katika soko la ndani;

- Kutekeleza Mkakati wa Kukuza Kilimo cha Mpunga ambao umepitishwa hivi karibuni na Baraza la Mapinduzi. Lengo la mkakati huu ni kupunguza utegemezi wa chakula kutoka nje, kutoka asilimia 85 mwaka 2010 mpaka asilimia 40 hadi 50 mwaka 2015/16. Maeneo ambayo mkakati huu umeyapa kipaumbele ni pamoja na:

i. Kuongeza eneo la miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo uvunaji wa maji ya mvua;

ii. Kuongeza uzalishaji kwa hekta kutoka kiwango cha sasa cha tani moja hadi tani tatu kwa hekta ya mpunga wa juu, na kutoka tani 3.5 hadi tani 7 kwa hekta kwa mpunga wa umwagiliaji maji;

iii. Kuongeza matumizi ya zana za kisasa;

iv. Kuongeza huduma za utafiti, mafunzo na elimu kwa wakulima katika zao la mpunga na mazao mengine;

v. Kuongeza matumizi ya pembejeo za kisasa.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba wizara yangu imeanza kuuwasilisha mkakati huu kwa washiriki wa maendeleo na hivi sasa ipo dalili kwamba serikali itapata mchango wa washirika wa maendeleo katika kutekeleza mkakati huu. Miongoni mwa washirika ambao wameonesha nia ya kushirikiana na serikali ni Serikali ya Korea na *USAID* kupitia *program* yao ya *Feed* the *Future*, na mazungumzo yanaendelea na washiriki wengine wa maendeleo (*DPS*). Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amekiri

kwamba suala hili la nafaka limekuwa ni changamoto duniani na hatuna uwezo wa kulizuia, kwa sababu nchi wazalishaji wa nafaka hizi wameamua sasa kuzigeuza kwenye nishati mbadala. Na kwa kuwa serikali imedhamiria kuimarisha Mapinduzi ya Kilimo kwa kuleta mbegu mpya ya mpunga ya Nerika, mbegu ambayo bila shaka itaondosha tatizo la chakula hapa Zanzibar.

Je, haoni haja sasa serikali kubadilisha maamuzi ya Kiwanda cha Sukari, Mahonda pamoja na bonde lake hivi sasa likatangazwa bonde lile kuwa ni la kilimo cha mpunga wa Nerika badala ya kilimo cha miwa ambayo huzalisha spiriti ambayo Zanzibar haihitajiki.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, ni sahihi kabisa kwamba kila dunia yetu inapoelekea katika maandalizi ya nishati mbadala kutokana na sasa kuanza kutoweka au kupotea na ughali wa nishati tulizozizowea za mafuta kwa maana ya *diezel* na *petrol,* kuongezeka kwa watu na pia kuna baadhi ya nchi uchumi wao kuimarika. Matumizi ya nafaka umeongezeka na kufanya hali kuwa tete katika soko la dunia. Kama nilivyojibu kwenye jibu mama kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona hiyo hali na ina mikakati endelevu ya kukabiliana na hali hiyo.

Kuhusu suala lake la Kiwanda cha Sukari Mahonda niseme tu Mhe. Naibu Spika kwamba, serikali imeagiza kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi kufanya mapitio juu ya hali halisi ilivyo, na hatimaye kutoa ushauri kwa Baraza la Mapinduzi ili maamuzi thabiti yafanyike juu ya matumizi ya maeneo ya kiwanda hicho na kiwanda chenyewe.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Kwa kuwa alikiri kwamba kuna mkakati wa kuweka ghala ya akiba, lakini tutaweka itakuwa hatufiki. Na kwa kuwa kama hakukuwa na muda maalum uliyowekwa, wakulima wengi watakula mbegu zao kwa kuwa serikali haina akiba ya chakula. Je, ni lini serikali imepanga hasa kuanzisha hii ghala ya akiba ili wananchi wapate uhakika na wanakoelekea.

(b) Katika maelezo yake Mhe. Waziri katika kupambana na hali hii ya chakula, jambo moja sikulisikia. Je, halimo katika *list* yao au wameghafilika? Kupambana na wadudu waharibifu wa mazao yakiwemo ya mpunga na matunda. Je, suala hili limepewa uzito gani katika wizara kutokana na hali ilivyo hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, kwanza nilipongeze sana Baraza hili tukufu la Wananchi wa Zanzibar, kwanza kwa kupitisha Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe na hatimaye kupitisha sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe miezi michache iliyopita. Sheria ile imetuwekea msingi mzuri na imara wa kuelekea katika programu zetu nyingi za uhakika wa chakula na lishe na nitazizungumza nitapowasilisha hotuba ya bajeti yangu.

Lakini swali la kwamba lini maghala ya akiba yataanza kufanya kazi. Mhe. Naibu Spika, niseme tu kazi hiyo imeshaanza, tulipopitisha ile sheria ya uhakika wa chakula na lishe, wizara yangu hatua ya mwanzo imefanya mapitio ya maghala yote yaliyokuweko ndani ya nchi yetu kuyatambua, kutambua milki yake, hali halisi yalivyo ili tupate msingi kwanza wa kuanzia. Tunategemea kuanzia mwaka ujao wa fedha tutafanya matengezo ya maghala manne, lakini hapo hapo tayari tumeandaa utaratibu wa kushirikiana na *FAO* kufanya tathmini na maandalizi juu ya muundo na matumizi ya maghala ya akiba. Kanuni zake, utaratibu wa kuhifadhi, utaratibu wa manunuzi, utaratibu wa utoaji, utaratibu wa msimu wa manunuzi na kadhalika.

Stadi hiyo hivi sasa inafanyika na hiyo pia itatupa msingi sasa ya kuweza kushirikiana na serikali na washiriki wa maendeleo kwanza katika ujenzi wa maghala ya kisasa ya akiba na hatimaye kuwa na utaratibu mzuri wa usimamizi wa utaratibu wetu wa ghala za akiba. Kwa hivyo, kazi hizo nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kwamba tayari zimeshaanza, hatusubiri mpaka litufike. Kazi hiyo imeanza itaendelea kuwa endelevu mpaka tufikie malengo ya nchi yetu ya kuwa na maghala ya kisasa kwa ajili ya kuhifaedhia chakula.

La pili Mhe. Naibu Spika, amezungumzia wadudu waharibifu. Swali lililoulizwa Mhe. Naibu Spika, halikuhusiana na wadudu na ndio maana sikuzungumzia wadudu. Lakini katika utaratibu wetu wa mageuzi makubwa ya kilimo huwezi kuendeleza Mapinduzi ya Kilimo bila ya kuwa kwanza kuwa na kitengo cha utafiti wa wadudu waharibifu ambacho tunacho, chuo cha utafiti ambacho tunacho na kimeongezwa hadhi na serikali ya Dkt. Ali Mohammed Shein. Pili tutayazungumza kwa undani wakati tutapokuja kuwaarifu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili katika bajeti yetu. Lakini kupambana na wadudu ni sehemu ya kuendeleza kilimo kila siku, huwezi kuendeleza kilimo bila ya kuwa na utaratibu mzuri wa kupambana na wadudu waharibifu. Nashukuru Mhe. Naibu Spika.

Nam. 78

Tatizo la Umeme Matemwe

Mhe. Kazija Khamis Kona – Aliuliza:-

Kwa kuwa sera na dira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa ni kuleta maendeleo bora na ya haraka kwa wananchi wake. Moja kati ya maendeleo yanayokusudiwa ni kuwapatia ufumbuzi wa kudumu wananchi kuhusu tatizo kubwa la umeme.

Na kwa kuwa jimbo la Matemwe ni moja kati ya sehemu iliyoathirika zaidi na tatizo hilo, mbaya zaidi ni kwamba ndani ya jimbo hilo kuna sehemu kama vile Pwani Mchangani nishati hiyo inapatikana na sehemu nyengine kama vile Kandwi, Kijini, Mbuyutende na Mikuuni nishati hiyo haipatikani kabisa.

(a) Ni nini hasa kinachozuia kufikishwa huduma ya umeme katika maeneo hayo wakati wananchi wenyewe wamejidhatiti kusaidia upatikanaji wa nishati hiyo.

(b) Mhe. Waziri, kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu unaahidi kitu gani mbele ya Baraza hili tukufu katika kutatua tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji, na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yangu ni kuhakikisha kuwa vijiji ambavyo havijabahatika kupata huduma ya umeme vinapatiwa huduma hiyo. Wizara yangu inathamini sana michango ya wananchi kwani inarahisisha upatikanaji wa huduma hiyo. Mhe. Naibu Spika, kilichokwamisha kwa sasa ni mawasiliano baina ya wanavijiji husika na shirika, hivyo kwa kuwa wanavijiji tayari wameshajidhatiti basi wafike shirika ili kupimiwa na kubainisha michango yao na shirika lijipange kwa kile kilichobakia ili kukamilisha zoezi hilo.

(c) Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa wizara yangu kupitia Shirika la Umeme itawasiliana na Mhe. Mwakilishi ili kuhakikisha kuwa vijiji hivyo navyo vinafaidika na huduma hiyo.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa vijiji hivyo ni muda mrefu sasa havijapata nishati hiyo ya umeme na umeahidi kuwa utafanya utaratibu ili vipate huduma hiyo. Je, Mhe. Waziri haraka zako hizo utazozifanya ni lini hasa utahakikisha kuwa huduma hiyo inapatikana au ni muda gani itapatikana huduma hiyo.

Pili Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Jimbo la Matemwe kuna baadhi ya shehia tayari zimeshapata huduma hiyo, lakini pamoja na kuwa wamepata huduma hiyo bado wana matatizo ya kuanguka kwa nguzo za umeme katika maeneo hayo. Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini hasa utakwenda kuwafanyia marekebisho nguzo hizo zilizoanguka chini ili isijetokea athari kwa wananchi wa vijiji hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, vijiji hivyo vilivyobakia kama nilivyoeleza katika jibu mama kwamba, tutavipatia umeme lakini siwezi nikasema ni muda gani, lakini ninachoomba ni kwamba baada ya kupitisha bajeti yetu vizuri tutajiandaa kwa ajili ya kuvishughulikia vijiji hivyo.

Swali la pili, ni kweli nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kuna nguzo nyingi nyingi kwa kipindi hiki na sio Matemwe tu, ni katika maeneo mengi ya Zanzibar. Lakini shirika tayari limeagiza nguzo zipatazo 2,700 ambazo zimeshawasili na tayari tumeshaanza kuyashughulikia masuala ya kuzibadilisha nguzo mmbovu. Lakini kwa sasa tunabadilisha laini za *HT* na baada ya kumalizika kwa nguzo hizo basi tutaingia katika laini za *LB* na *Inshaallah* tatizo hili litamaliza Zanzibar. Kwa sababu lengo la shirika langu ni kuwatumikia wananchi na kuwang'arisha zaidi ili waonane katika huduma hii ya umeme.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri anasema lengo la wizara yake ni kuhakikisha wananchi kupata huduma ya umeme kwa haraka. Atakubaliana nami kwamba wizara yake hivi sasa haiko tayari kwa suala hilo. Kwa sababu kuna vitu vidogo vidogo tu vya kuunga kwenye vituo vya maji inachukua siku kadhaa. Je, wananchi wetu unawaeleza nini kuhusu suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, sitokubaliana na yeye kwa hili. Kwa sababu shirika langu linajitahidi sana kufuatilia matatizo haya. Aidha, tunapopata taarifa tu ya kwamba sehemu fulani ina matatizo basi wafanyakazi wa shirika wanajitahidi kufuatilia. Kwa hivyo, kwa suala hili sitokubaliana naye.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, moja katika jimbo ambalo vijiji vyake vina ukosefu mkubwa sana wa umeme ni Jimbo la Mtambwe. Hivi sasa ninavyojua Pemba kuna nguzo nyingi sana za wizara zimeletwa inafika mwezi wa pili huu, lakini unapoomba huduma ya umeme unapewa makisio na kutakiwa uhudumie mwenyewe, zile nguzo zimekaa kwa madhumuni gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, naomba arejee swali lake sijalifahamu vizuri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nasema kuwa, moja katika ya jimbo ambalo lina upungufu wa umeme ni Jimbo la Mtambwe, ni vijiji vingi tu. Hivi sasa kule Pemba kuna nguzo nyingi sana za umeme na tunapokwenda kuomba huduma ya kupelekewa umeme katika vile vijiji ambavyo havina umeme nashukuru shirika linajitahidi kutoa makisio, lakini mwisho wake hutakiwa wananchi tuchangie ndio umeme huo uweze kufika. Swali ni kwamba, zile nguzo nyingi zilizoko zimewekwa kwa ajili gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiria Mhe. Mwakilishi ana haraka sana, lakini lenog la kutafuta nguzo hizo ni kwa ajili ya kusambaza umeme na kutumiwa na wananchi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi avute subira kama nilivyoeleza kuwa nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yangu ni kuwasambazia wananchi wote umeme katika vijiji vyote vilivyobakia. Kwa hivyo, avute subira na sisi tuko pamoja naye na Inshaallah hivyo vijiji vilivyobakia huko katika jimbo lake basi vitapatiwa huduma hiyo.

Nam. 70

Walimu Kuchangishwa Fedha Maskulini

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa wizara yako imekuwa na utaratibu wa kuwachangisha fedha walimu kutoka katika mishahara yao. Na kwa kuwa michango hii ni kwa ajili ya sherehe mbali mbali za kiserikali kama vile, Elimu bila ya Malipo, Siku ya Walimu Duniani na kadhalika. Na kwa kuwa mishahara ya walimu ni midogo mno haitoshi kukidhi hali ngumu ya maisha.

(a) Je, Mhe. Waziri, huoni kwamba kuendelea kuwachangisha walimu fedha kwa ajili hiyo kunawazidishia walimu hao ugumu wa maisha.

(b) Ni vipi wizara yako inafaidika na michango inayotokana na Mwenge wa Uhuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 70 lenye sehemu (a) na (b), lakini kwanza ningependa kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba walimu na wafanyakazi wengine wa wizara wanachangia fedha katika kufanikisha baadhi ya sherehe za kitaifa kama vile sherehe za Elimu bila ya Malipo, Siku ya Walimu Duniani na Juma la Elimu ya Watu Wazima. Walimu wanachangia shilingi 1,000/= kwa kila sherehe kwa kila mwaka. Mbali ya sherehe hizo, walimu wanachangia kiasi ya shilingi 1000/= kwa kila mwalimu kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa Vituo vya Walimu. Kiwango hicho cha fedha kinakusanywa na walimu, hakitoshi mahitaji yote ya sherehe, bali husaidia sana katika kutimiza baadhi ya mahitaji na serikali hutowa fedha nyingi zaidi katika kufanikisha sherehe hizo adhimu.

Mojawapo ya sababu za walimu kuchangia sherehe hizo ni kutokana na kufahamu kuwa sherehe hizo zina umuhimu mkubwa katika taaaluma ya ualimu, kwani zinawaelimisha umuhimu wa elimu na walimu katika jamii.

Pili, ni kweli kuwa mishahara ya walimu kama ilivyo mishahara ya watumishi wa kada nyengine haikidhi gharama za maisha. Hata hivyo, bado walimi wana moyo wa kuchangia sherehe hizo na mambo mengine muhimu ya maendeleo ya nchi yao pamoja na kukabiliana na ugumu wa maisha. Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Walimu kuchangia fedha katika kufanikisha sherehe hizo hakuwazidishii ugumu wa maisha, kwani kiwango cha fedha wanachochangia kwa mwaka ni kidogo sana. Kwa niaba ya wizara napenda kuwapongeza walimu na wafanyakazi wengine wa wizara kwa moyo wao wa kuchangia sherehe hizo mbali mbali za kitaifa na shughuli nyengine za maendeleo na ninaomba waendelee na moyo huo.

b) Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ndizo zenye kutoa maamuzi juu ya matumizi ya fedha zinazokusanywa katika mbio za mwenge. Napenda kuthibitisha kuwa wizara yangu imefaidika na michango ya fedha zinachangwa na wananchi katika mbio za mwenge wa uhuru. Baadhi ya fedha hizo zimetumika katika mwenye wa uhuru zinatumika na kuunga mkono nguvu za

wananchi katika ujenzi wa madarasa mapya. Kwa mwaka 2010, baadhi ya skuli zilizopatiwa fedha kama hivi ifuatavyo:-

i) Skuli ya Fuoni Msingi ilipata shilingi 150,000/=
ii) Skuli ya Fuoni Kibondeni ilipata shilingi 200,000/=
iii) Skuli ya Mwanakwerekwe 'G' na 'H' zilipata shilingi 200,000/=
iv) Skuli ya Mwanakwerekwe 'F' ilipata shilingi 150,000/=
v) Skuli ya Regeza Mwendo ilipata shilingi 200,000/=
vi) Skuli ya Bwefum ilipata shilingi 200,000/=
vii) Skuli Mtambile ilipata shilingi 100,000/=
viii) Skuli ya Ngwachani ilipata shilingi 300,000/=
ix) Skuli Skuli ya Kilima Juu ilipata shilingi 200,000/=
x) Skuli ya Gamba ilipata shilingi 200,000/=. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ya kuwapongeza walimu juu ya michango yao. Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba, mbali ya pongezi hizo lakini walimu wengi wana masononeko juu ya michango hii.

(b) Kwa kuwa wizara yake imekuwa ikisherehekea sherehe za Elimu bila ya Malipo katika kila ifikapo tarehe 23 Septemba, na kwa kuwa maandalizi ya sherehe hizi huwa yanaanza mapema miezi sita kabla ya kilele cha sherehe hizo. Na kwa kuwa wanafunzi wengi huwa unawafanya wakose nafasi ya kushughulikia masomo yao.

Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba wakati sasa umefika wa sherehe hizi kufanywa kila baada ya miaka 5 na sio kama ilivyo sasa kufanya sherehe hizi kila mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nilivyozungumza mwanzo nimesema kuwa michango hii ni michango ya hiari sio michango ya lazima. Mhe. Naibu Spika, sisi tuna walimu karibu 11,000, lakini ukitizama wanaotoa michango hii ni nusu yao tu na wale ambao waliokuwa hawatoi hakuna aliyefukuzwa skuli wala aliyepewa barua ya onyo. Kwa hivyo, hii ni michango ya hiari na Mhe. Naibu Spika, kutoa ni moyo si utajiri kwani huwa wanachangia suala ambalo ni lao wenyewe. Hivyo sio vizuri kuwavunja moyo sisi kama Waheshimiwa Wawakilishi ni vizuri kuwapa

moya kwa sababu fedha hizi ambazo zinachangiwa kwa sherehe za elimu zinazowahusu wao wenyewe walimu na wafanyakazi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala Nam. 2 ambalo anasema imefika wakati wa kuzitizama hizi sherehe zetu kama zifanyike baada ya miaka 5.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa serikali ina utaratibu wa kupitia sherehe zote, hivyo mimi siwezi kulitolea maamuzi hapa tusubiri uamuzi wa serikali ambapo utapitisha sherehe gani tuifanye kwa muda gani, na sherehe gani tuifanye kwa muda gani. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwanza napenda kumwambia Mhe. Naibu Waziri kuwa atakubaliana na mimi kama hii michango si ya hiari ni ya lazima kwa sababu wanakwata katika mishahara yao.

b) Kwa sababu sherehe zote zinazofanywa katika nchi yetu tuna mazoea kuwa serikali inahudumia sherehe na tunasikia kila siku kama sherehe hii imegharimu shilingi milioni kadhaa. Je, atakubaliana na mimi kama hakuna haja ya kuwatonza walimu kwa sababu mshahara wao ni mdogo na serikali ikasimamia hizi sherehe ikiwa wanataka ziendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, sikubaliani na Mhe. Mwakilishi kama michango hii inakatwa kwenye mishahara yao, sio kweli. Mhe. Naibu Spika, michango hii ni ya hiari na haikatwi kwenye mishahara yao.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyozungumza katika jibu mama kuwa serikali inagharamia sherehe hizo na hutoa pesa nyingi kwa ajili ya sherehe hizo, lakini bado huwa hazitoshelezi kutokana na mahitaji ya sherehe hizo, na sio walimu tu na wafanyakazi wetu ambao wanachangia. Mhe. Naibu Spika, hata wafanyabiashara hutusaidia sana kwa mfano watu wenye meli huwa wanatusaidia japo nusu tiketi kwenda na kurudi. Kwa hivyo, hili jamani ni jambo la Wizara ya Elimu ni kwa nini tuwazuie walimu wetu ambao wana moyo wa kuchangia kwenye sherehe hizi.

Nam. 35

Kitengo cha Afya Akili Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwanza naipongeza Wizara ya Afya kwa azma yake nzuri ya kuanzisha kwa mara ya kwanza kitengo cha huduma za afya ya akili huko kwenye Hospitali ya Wete Kisiwani Pemba.

(a) Ni hatua gani ambayo imefikiwa katika utekelezaji wa azma hiyo.

(b) Je, Serikali haioni kuwa nafasi finyu iliyopo kwenye Hospitali ya Wete inaweza iwe ni tatizo kwa Kitengo cha Afya ya Akili kuwekwa ndani ya hospitali hiyo.

(c) Kwa nini Serikali haitafuti sehemu nyengine popote pale mbali ya hospitali ya kawaida kwa ajili ya kitengo hicho ili kuepusha kusababishwa na wagonjwa wa akili kwa wagonjwa wengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kuipongeza wizara yangu kwa juhudi tunazozifanya hususan katika kuanzisha Mrengo wa Afya ya Akili Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyojibu katika suala Nam. 31 kwa hivi sasa hatua zote za maandalizi ya ujenzi wa Mrengo wa Afya ya Akili Pemba tayari zimekamilika. Mkandarasi ameshachaguliwa na kazi za ujenzi zimeshaanza kwa mujibu wa mkataba.

Mhe. Naibub Spika, maamuzi ya kujenga katika eneo hilo yamefikiwa baada ya kukaa pamoja na wataalam wa magonjwa ya akili na wahandisi wetu. Tumekubaliana kwamba nafasi iliopo inatosha na haitakua kero au kuleta usumbufu kwa wagonjwa wengine. Vile vile kuwepo mrengo huo karibu na hospitali kumezingatiwa kamba wagonjwa hao kikawaida huhitaji huduma nyengine na sio za akili pekee. Aidha, kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu wagonjwa hawa hawapaswi kutengwa kwani kufanya hivyo ni kuwanyanyapaa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (a) Mhe. Naibu Spika, ninavyofahamu mimi Mhe. Naibu Waziri kunyanyapaa ni mtu kumdharau au kumdhalilisha, lakini kumtenga mwandaazimu si kumyanyapaa. Kwa hilo anaweza kufanya jambo bila ya kukusudia lolote lile hivyo naomba Mhe. Naibu Waziri unifahamishe kunyanyapaa hapo pako wapi.

b) Pia Mhe. Naibu Waziri kuna mtu yeyote aliyelalamika kwa kuwataja wagonjwa wa akili wa Kidongochekundu ni kinyume na haki za binadamu au kuwanyanyapaa.

c) Kuna huduma gani za matibabu walizokosa wagonjwa wa akili wa Kidongochekundu kutokana na kutengwa kwao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza unyanyapaa ni tendo lolote lile ambalo litakalomfanya mtu ajihisi kwamba yeye hana thamani kwa watu wengine. Kwa hivyo, njia za kunyanyapaa zipo nyingi kutokutaka kukaa nae hiyo ni moja ya kwamba unamnyanyapaa na hasa kama mtu yule ni mgonjwa na anahitaji huduma.

Mhe. Naibu Spika, tangu juzi hapa tunazungumza watu watataka wakae karibu na watu, wanataka kubembelezwa kwa kuwa kakosa akili ndio asikae karibu na watu. Pia anahitaji matibabu Pemba kama tunavyojua ukosefu wa wafanyakazi walivyo tukatafute pahala mbali tuwatenge likitokea la kutokea hivyo kweli itakuwa ni vizuri.

Mhe. Naibu Spika, sisi kama wataalamu tumeona kwamba kuwaweka karibu na hospitali ni sehemu ya kuwaenzi watu wale na tusiwanyanyapae. Kwa hivyo, hiyo ni dhana ya kitaalamu, nafikiri kama ni dhana ya kitaalamu hatukukosea.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Kidongochekundu ilipojengwa ilijengwa maisha ya nyuma, kule iliko na hospitali nyengine zilijengwa. Hospitali ile ilijengwa baada ya kuwa watu wale zamani walikuwa wakipelekwa jela, na ndio maana hata hiyo Kidongochekundu wenyewe ilikuwa inaitwa jela la wendawazimu na sasa hivi tunaiita Hospitali ya Wagonjwa wa Akili.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa katika Kisiwa cha Pemba kunaongezeko kubwa la ugonjwa wa akili katika kipindi hiki, na kwa kuwa maradhi hayaleti barua wala salamu yanapokuja, na kwa kuwa ni juzi tu katika kijiji changu cha Vitongoji mgonjwa wa akili amemuuwa bibi yake mzaa mama kwa mapanga.

a) Je, ni hatua gani za dharura katika hali hii ambapo kabla ya huyo mkandarasi hajamaliza hospitali yake tufanye nini ili kuepuka hayo maafa ya kuuliwa na wendawazimu pale Pemba.

b) Je, isingekuwa vyema katika hiki kipindi cha mpito ukatuletea madaktari wa akili pale Pemba angalau kuweza kutunusuru na mapanga ya wendawazimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, napenda nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kuwaita wendawazimu ndio katika hiyo sehemu ya kuwanyanyapaa, wale ni wagonjwa wa akili naomba tubadilike jamani.

Mhe. Naibu Spika, hayo anayoyasema Mhe. Mwakilishi kama yametokea huko nakubaliana na wewe, lakini pale hospitali ya Chake Chake tunasehemu ambapo wagonjwa wa akili wanapelekwa na wanakaa pale halafu wanapata huduma. Katika hao madaktari wengi niliokupelekeeni Pemba kuna madaktari ambao wamesomea maradhi ya akili na hapo katika hiyo wodi ya Chake Chake ndio waliopo. Kwa hivyo, kama kumetokea tatizo kama hilo sehemu yako fanyeni utaratibu mumpeleke hospitali akapate matibabu.

Nam. 184

Mikopo ya AK/ JK

Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali hili ameliondosha.

Nam. 79

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi

Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali hili ameliondosha.

Nam. 72

Matengenezo ya Maboya na Minara

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya njia kuu za usafiri inayotumiwa na wengi kwa usafiri wa Z'BAR – DAR, Z'BAR–PEMBA ni usafiri wa baharini, na kwa kuwa maboya na minara ambayo ndiyo inayoongoza safari haifanyi kazi ipasavyo.

Je, Serikali imeandaa mpango gani wa kurekebisha hali hiyo.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano) - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa usafiri wa baharini ni muhimu kwa Zanzibar na usalama wake hutegemea minara na maboya. Aidha, ni kweli baadhi ya wakati hutokezea minara na maboya hayo kuwa hayafanyikazi ipasavyo.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na tatizo hilo wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imeandaa mpango wa muda mfupi wa kuzibadilisha taa zote za minara mikubwa na midogo ili kuondokana na matumizi ya mvuke (*acetylene gas*) na kufunga taa mpya za kisasa zinazotumia teknolojia ya nguvu za jua (*solar*). Mpango huo umebuniwa baada ya mafanikio yaliyopatikana kwa mnara wa Pungume ambao hivi sasa unawaka kwa taa ya *solar* bila ya matatizo makubwa. Hivyo, tuna lengo la kuzibadilisha taa za Kigomasha na Matumbini Pemba pamoja na minara iliyobakia yote.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Shirika la Bandari inatarajia kutumia zaidi ya Tsh. 182,824,000.00 katika mradi huo wa ubadilishaji wa taa za minara kumi na saba (17) kutoka matumizi ya gesi na kutumia nguvu za jua (solar).

Aidha, kwa upande wa maboya yenye taa tayari yote yanatumia *solar* na yanafanyakazi kama inavyotakiwa isipokuwa pale inapotokea ajali ya boya hilo kugongwa na meli na kubiruka. Kwa mfano, hivi sasa maboya matatu (3) ya Unguja ambayo ni kisiki, chapwani na mtwana yanafanya kazi kama inavyotakiwa. Kwa upande wa Pemba boya Nam.1 haliwaki na hii imetokana na boya hilo kugongwa na kubiruka na kuzama baharini na maboya yaliyobaki ambayo ni boya Nam. 2 na boya Nam. 3 yanawaka katika Bandari ya Mkoani.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata jibu la kutia tamaa sana na Mwenyezi Mungu amejaalia kuwa limekuja wakati marekebisho yameshafanywa. Lakini katika bandari ya Wete hapo zamani kulikuwa na maboya yanawaka na vyombo vikawa vinaweza kuingia na kuondoka mpaka usiku, lakini siku hizi kwa sababu baadhi ya maboya hayawaki hasa huku mwanzo kwa kutokea unapoingia bandarini ni vigumu kwa chombo chochote kuweza kusafiri kwa wakati wa usiku. Mhe. Naibu Spika, kwa vile safari zinaongezeka kila siku na mahitaji yanakuwa ni lini Mhe. Waziri ataona kuwa iko haja ya kurekebishwa katika safari ya kuelekea kwenye

bandari ya Wete kuona kuwa meli nazo zinaweza kuingia na kutoka wakati wa usiku.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba kwa wakati tuna maboya ya aina tatu, tuna maboya ya kijani, mekundu na njano. Mhe. Naibu Spika, maboya haya yanaongoza kuingiza meli katika bandari zetu na sasa hivi tatizo letu kubwa ilikuwa katika bandari ya Mkoani na Malindi na zote zinafanya kazi, kama kuna tatizo katika bandari ya Wete basi mamlaka husika itashughulikia.

Nam. 212

Hoteli Kuunganisha Kuta

Mhe. Ussi Jecha Simai (Kny: Mhe. Suleiman Hemed Khamis) - Aliuliza:-

Kumekuwa na tabia iliyojengeka kwa Wawekezaji wanaomiliki hoteli za kitalii kuunganisha kuta (*fence*) baina ya hoteli na hoteli kwa kufunga njia ya asili ambayo wananchi huitumia kwenye shughuli zao za uvuvi au shughuli nyenginezo. Suala hili limebainika pia katika Kijiji cha Kijijini Makangale.

Kwa kuwa ujenzi wa ukuta huo haujafanyika. Je, Mhe. Waziri utawasaidia vipi wananchi wa Kijijini – Makangale kuhusiana na kadhia hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 212 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, suala la wawekezaji kuziba njia za asili bila ya ridhaa za wananchi halikubaliki. Aidha, kumekuwa na baadhi ya vijiji ambavyo vinakubaliana na Wawekezaji kuziba njia za asili kwa kutoa njia mbadala. Mhe. Naibu Spika, kwa wananchi wa Kijiji cha Makangale, kwa kuwa ukuta huo bado haujajengwa naziomba taasisi zinazotoa vibali vya ujenzi kutoruhusu ujenzi wa kuunganisha kuta (*fence*) baina ya mradi na mradi kwa kufunga njia za asili kama ilivyoainishwa katika *Tourism Zoning Plan* na Sheria ya Usimamizi na Matumizi ya Ardhi ya mwaka 1992 inayowataka wawekezaji kuacha njia biana ya mradi na mradi (*buffer zone*).

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri huoni iko

haja wizara yako ikatunga sheria yakuwadhibiti hao wanaofanya hivyo kwa kuwadhalilisha wavuvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali mama kuwa wananchi wenyewe ndio wanaoshirikiana pamoja na wawekezaji, lakini wizara yangu italisimamia na italifuatilia pamoja na serikali kuweka sheria ambayo inaweza kushughulikia suala hilo.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Afya

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba nitake radhi kidogo kwa sababu wizara hii ilikuwa tuimalize tangu juzi, lakini kwa kuwa Waheshimiwa wengi walijitokeza kuchangia tumetoa nafasi yakutosha sasa nimebakia na Waheshimiwa sita naomba radhi kwamba sasa hivi tumpe nafasi Mhe. Naibu Waziri halafu tumpe nafasi Mhe. Waziri ili aweze kufanya majumuisho na saa moja iliyobakia tuweze kumpa Mhe. Waziri kupitisha vifungu. Kwa hivyo, Waheshimiwa ninaowataja naomba radhi sana wajitayarishe kwa wizara inayokuja nao ni:-

1. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
2. Mhe. Omar Ali Shehe
3. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
4. Mhe. Salim Mohammed Ali
5. Mhe. Ashura Shariff Ali
6. Mhe. Mussa Hassan Omar na
7. Mgeni Hassan Juma.

Waheshimiwa Wajumbe tunaomba radhi kwa hilo ili tuweze kuimaliza wizara hii ili jioni iingie wizara nyengine. Kwa hivyo, hivi sasa tunamwita Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu napenda nianze kutoa shukurani kwako kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe kutoa ufafanuzi kwa yale ambayo yaliyoulizwa. Pia nitamuachia Mhe. Waziri wangu yale ambayo anahisi kwamba yeye yako kwa upande wake na ayajibu. Mimi nitazungumzia zaidi linalohusu utaalamu na yeye atazungumza yaliyobaki.

Mhe. Naibu Spika, napenda nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein pamoja na Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini mimi kwa kunichagua kumsaidia Mhe. Waziri wa Afya ili kutekeleza ahadi na ilani za Chama cha Mapinduzi kuhusu afya.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wangu wa Afya kwa mashirikiano yetu mazuri lakini sote tuna dhamira moja yakutekeleza yale ambayo wananchi wanayataka nayo ni kuleta afya bora kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote waliochangia na waliokuwa hawakupata fursa ya kuchangia kwa namna moja au nyengine. Mhe. Naibu Spika, waliochangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 kuchangia kwenu kumetupa faraja. Mimi hasa kama mtaalamu wa afya najua sasa wagonjwa wa *pressure* humu tena katika Baraza watapungua moja ya sababu kubwa ya *pressure* ni mtu kutokupata nafasi ya kusema. Mhe. Naibu Spika, itakuwa kitu kinamuudhi mpaka *pressure* inapanda, lakini akishazungumza basi *pressure* itashuka.

Kwa hivyo, kila mmoja kwa namna mbali mbali ametoa mawazo, ametoa maoni, ametoa ushauri, ametoa joto na mmeniuliza masuala kwa nia moja tu yakutaka kuimarisha huduma za afya na wananchi wetu wapate huduma bora zinazostahiki na wasihangaike kuzifuata nje ya nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana kwa kutuombea bajeti izidishwe na msisite kufanya hivyo kila mnapopata fursa kwa sababu afya ni ya wote. Mhe. Naibu Spika, mengine yote yanawezekana kwa vyenginevyo, elimu ukisoma utaishi ukisoma utaishi, kilimo ukilima utakula usipokula utakula, lakini afya utaugua itabiti uende hospitali. Kwa hivyo, hakuna anayeweza kuepuka afya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nisichukue muda wako mkubwa nataka nitoe ufafanuzi kwa baadhi ya masuala ya yaliyoulizwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa kipande kimoja tu cha maswali aliyouliza kuhusu daktri wa macho wa Kichina tuliyenaye Mnazi Mmoja Hospitali. Naomba nimfahamishe Mhe. Mshimba na Waheshimiwa wengine wote na wananchi wote kwa daktari tuliyenaye Mnazi Mmoja Hospitali ni daktari bora kuliko madaktari wote wa Afrika Mashariki. Hilo ni kwa uhakika na linajulikana kwa sababu sasa watu wanatoka nje ya nchi yetu kuja kutoa huduma. Kiingereza anachokisoma daktari yule ni miezi mitatu na ndio maana kunakuwa na mtaalam wa kuweza kumsaidia. Kwa hiyo,

wananchi tusiwe na mashaka daktari wetu ni mzuri nathubutu kusema hivyo ukilinganisha na wengine wengi tulionao.

Mhe. Naibu Spika, pia ningependa kumjibu Mhe. Assaa Othman Hamad baadhi ya masuala aliyouliza. Alisema kuna madaktari 216 wako nje ya Zanzibar. Kwanza naomba tuelewe kwamba hospitali kuna kada za afya, si kila aliyeko hospitali ni daktari, kuna daktari, kuna wasaidizi wa daktari na kada nyengine maabara na *pharmacy*. Sasa kwa taarifa tulizonazo sisi kwamba kuna manesi 72 wameondoka nchini na madaktari 27 na sio 216.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala jengine linalohusiana na uajiri wa watu wasio Wazanzibari. Napenda kumhakikishia Mhe. Assaa Othman Hamad kwamba kwa muda wa miaka 6 sasa Pemba hatujaajiri ma-*orderly*, mara ya mwisho tuliajiri *orderly* mwaka 2005 mwisho wa Julai. Tunakiri kuwa tuna upungufu wa *orderly* lakini tuhuma za kuwa tunaajiri wasio Wazanzibari sio za kweli.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la wafanyakazi nyumba mbovu, Wizara ya Afya hili imeliona nyumba ziko nyingi. Lakini hata sisi juhudi tumechukua mwaka huo uliopita tumeshuhudia nyumba 40 zimejengwa Unguja na nyumba 40 zimejengwa Pemba. Nafikiri ni hatua moja kubwa kuifanya kwa mwaka mmoja.

Mhe. Naibu Spika, lakini hata hivyo hatujafika mbali vituo tuna vingi Unguja tuna 72, Pemba tuna 59, nyumba 40 Pemba, nyumba 40 Unguja hazijatosha. Sasa mimi nilikuwa na ushauri kwa Waheshimiwa Wawakilishi kama hilo tunaliona tungewaomba tusaidieni, isiwe badala ya kujenga tena vituo vingi basi natuache kujenga hizi nyumba angalau wale madaktari wetu tunapowaomba wapate pakukaa. Tukiendelea tu kujenga vituo halafu wafike nusu na sisi kushindwa kuvimalizia kikimalizika hakuna daktari wa kumuweka, kikimalizika hakuna dawa kwa kweli nafikiri tutakuwa hatwendi mbele tunarudi nyuma.

Kwa hiyo, nawaomba tusaidiane na ikiwezekana hata kuvifanyia matengenezo hakuna ubaya. Tusaidiane tuweze kuzikarabati hizi nyumba ili wataalam wetu waende wakakae. Maana tukiangalia hata hizo mbovu hazitoshi.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kumjibu Mhe. Salmin Awadh Salmin kuhusu suala la mkahawa uliopo katika maeneo ya hospitali kuu. Tumefahamishwa kwamba kuna mikahawa ya aina mbili, kuna chai maharage na ile mikubwa. Wizara ya Afya kitengo cha afya kinahusika na mikahawa mikubwa na ile midogo midogo inahusika na Manispaa na Halmashauri kwa sababu wao ndio wanaotupa leseni na ndio wanaopita kuzikagua. Kwa hiyo, hili lielekezwe huko

kwenye halmashauri na manispaa lakini ushauri tumeupokea, tukiwa tunapita katika shughuli zetu tutapita tuchungulie huko tuone kinachoendelea na tujaribu kusaidiana nao.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu utanuzi wa hospitali ya Kivunge kuwa ina hali mbaya ya majengo na kila kitu kimechoka. Hilo tunalikubali kwa sababu hospitali hii imejengwa kitambo. Lakini kwa vile hospitali hii ni moja katika hospitali zilizomo katika mpango wa kuipandisha hadhi na daraja kwa sasa tunajiandaa tunafanya tathmini ili kujua nini kinahitajika katika hospitali zetu zile. Wakati huo huo tunafanya majaribio katika hospitali ya Makunduchi, Fuoni na baadae tutahakikisha kwamba hospitali zetu zote zimefanyiwa marekebisho kufikia hadhi hiyo iliyotakiwa kufika kwa wakati uliopangwa.

Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwa na malalamiko ya hospitali ya Muembeladu kwamba hakuna vyandarua wala ma-*heater* kwa ajili ya maji ya moto. Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba vyandarua tayari vimeshapelekwa na suala la *heater* linafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwa na suala lile linalozungumza kujali nguvu za wananchi kwa kujenga vituo. Kwa kweli tunathamini nguvu za wananchi hususan linapokuja suala la ujenzi wa vituo. Lakini tatizo linalojitokeza kwamba pale viongozi wetu na wananchi wanaposhawishika kujenga vituo tunatakiwa tufuate ushauri. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya inatoa wito kwa sasa kwamba tunachokihitaji nyumba za wafanyakazi, vifaa katika kuimarisha vituo vya afya. Mhe. Naibu Spika, pia kuna sera maalum inayohusiana na ujenzi wa vituo.

Kwa hiyo, pale tutakapohisi kwamba hii huduma ni lazima ifanyike tuiteni Wizara ya Afya twende tukapaangalie pahala tuangalie kweli kama pana mahitaji tukupeni ramani ambazo zinazohusika tujenge tuko pamoja na nyinyi hakuna tatizo.

Mhe. Naibu Spika, pia ningependa kujibu baadhi ya masuala ya Mhe. Abdi Mosi Kombo kuhusu utaratibu wa kupima afya kwa wananchi wa vjijijini. Hili tumelisikia, tumelipokea na limo katika mipango ambayo inafanyiwa kazi na tunategemea karibuni tutaanza rasmi baada ya kupitishwa sheria inayohusika na hilo. Kwa hiyo, tunajipanga na inshaallah litafika.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Abdi Mosi Kombo alisema ma-*orderly* waangaliwe. Mhe. Naibu Spika, hili suala limeshatolewa jibu na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwamba kila mmoja atapewa haki kwa mujibu wa nafasi yake.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Abdi Mosi Kombo amezungumzia kuhusu kichocho kuenea kaskazini. Hiyo ni kweli kwa upande wetu wa Zanzibar kaskazini ni sehemu ambayo ina kichocho kingi lakini Mradi wa Kichocho wizara imeelekeza juhudi zake zote kaskazini katika mambo ya kupima, kutoa madawa maskulini na kulifanyia elimu ya afya katika maskuli na katika jamii. Hiyo kazi inaendelea na pia tuna program imeanza sasa hivi inafanya utafiti wa kina kuhakikisha kwamba hilo tatizo linaondoka kabisa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia ningependa kutoa ufafanuzi kwa suala la Mhe. Asha Abdu Haji kuhusu hospitali ya Mnazi Mmoja kuna matatizo na kwamba wajawazito wanapewa lugha mbaya. Mhe. Naibu Spika, ningeomba nianze na kitu kimoja, kwenye ulimwengu huu wote tulionao panapoishi watu basi watu wa aina mbili wapo wazuri na wabaya, pana dhambi pana thawabu. Ina maana kila kitu kipo katika pande hizo mbili. Mimi sifikiri kwamba labda mtu akitoka akenda pengine hapati lugha mbaya, tunakwenda sote tunatembea kila pahala tunapata lugha mbaya na nzuri. Lakini la kwetu limekuwa gumu zaidi kwa sababu pale pana uhusiano na afya na ndio maana limekuwa na mambo ambayo tunaambiwa kwamba lugha ni mbaya.

Lakini wafanyakazi wa afya tuko 3,000 kweli hawa wote wanatoa lugha mbaya, kama ingekuwa kweli ni hivyo sidhani kama watu wangekuwa wanafika mahospitalini. Kwa hiyo, nafikiri wale ambao wanafanya vizuri tungewapongeza na ndio wengi na huyu mmoja mmoja anayejitokeza tutahakikisha kwamba hatua zinazohitajika zitachukuliwa kwa sababu sisi wafanyakazi wataalam wa afya tuna maadili na kwa wao kufanya hivyo ni kukiuka maadili ya kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, pia ningependa kujibu suala la Mhe. Farida Amour Mohammed kuhusu hospitali ya Wete kwamba haina daktari wa upasuaji na hajui atapatikana lini. Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kutambua mchango wa *Zanzibar Outreach Programme* kama Jumuiya isiyokuwa ya Kiserikali lakini mchango wake ni mkubwa kwa kufikisha huduma za afya vijijini na katika hospitali mbali mbali. *Zanzibar Outreach Programme* ina utaratibu wa kupita kila mwezi na kutoa huduma hizo. Lakini hata hivyo, tunafahamu wataalam wapo kidogo na sisi tutajitahidi wizara kutatua tatizo lile kama ilivyofanya kwa daktari wa magonjwa ya kike.

Mhe. Naibu Spika, napenda niendelee kujibu suala la Mhe. Raya Suleiman Hamad, suala nitakalolijibu katika mengi aliyoyasema kuhusu semina zitolewe kwa wote. Hasa alikuwa anakusudia wale wanaohusika na walemavu na akawataja watu wawili wanaofanya kazi pale. Mhe. Naibu Spika, napenda nimtoe wasi wasi pale pana watu wawili tu na pana mafunzo mengi, wale wanakwenda mafunzo kuliko madaktari wote walioko Pemba kwa sababu

chochote kinachotokea wanakwenda wao. Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, ninavyokwambia mmoja wao hayupo yuko Tanzania Bara kwa mafunzo mafupi.

Mhe. Naibu Spika, pia ningependa kujibu suala la kusafirisha wagonjwa wa akili litamalizika lini. Kama nilivyokwisha kusema tatizo hili litamalizika tu wakati jengo letu la Hospitali ya Wagonjwa wa Akili litakapomalizika na ujenzi umeshaanza.

Mhe. Naibu Spika, pia ningependa kumjibu Mhe. Suleiman Hemed Khamis kuhusu dawa za malaria kupulizwa zinawasha tutafute mbadala. Mhe. Naibu Spika, nataka kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba tatizo linajitokeza kwa wale wanaoshindwa kufuata ushauri wanaopewa. Tunatakiwa dawa inapopigwa kwenye majumba watu wakae nje ya nyumba ile kwa masaa mawili, kabla ya kupulizwa inatakiwa nguo zote, mashuka, mapazia, nguo za kuvaa ziondoshwe ziwekwe pahala ambapo dawa haitofika.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya yakiwa hayo hayakufanyika, ikiwa mtu atavaa nguo, atazigusa au atagusa pazia lililotiwa dawa kwa siku ile na sio wote ni baadhi tu ya watu nao ni kidogo watapata hilo tatizo watawashwa. Lakini si kitu cha kutisha ikitokea hiyo wakimbilie kwenye hospitali watapata dawa. Mhe. Naibu Spika, shahidi wangu Mhe. Viwe Abdalla Khamis hapa juzi kulitiwa dawa nyumbani kwake akaja hapa asubuhi akanihadithia nikamuandikia dawa na mchana akarudi salama usalimini.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Mwakilishi kashauri kwa nini dawa zinapulizwa ndani tu nje hazipulizwi na mbu nje wako. Dawa zinazopulizwa ziko aina mbili tofauti, kuna dawa za ndani na dawa za nje. Kwa sasa hivi tunapuliza dawa za ndani ambazo ni *indo-residence spray* na hizo za kupuliza kwenye madimbwi zitaanza karibuni. Kwa hiyo, asiwe na wasi wasi Mhe. Mwakilishi yote mawili yatafanyika kuhakikisha kwamba malaria hayarudi tena.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Mwakilishi alitoa ushauri kwamba labda tufanye utafiti tuwaulize wananchi. Tumeyafahamu na ndio hayo tuliyokwisha kuyatolea ufafanuzi kwa hiyo hakuna haja tena ya kufanya hivyo.

Lakini Mhe. Mwakilishi alikuwa na wasi wasi mkubwa na *qualification* za madaktari wetu pamoja na mimi kwamba je, *qualification* zetu ni zipi, zinafaa. Mimi napenda nimhakikishie Mhe. Suleiman Hemed Khamis kwamba madaktari wote waliopo Unguja na Pemba na hao waliohama nchi hii wakenda nje wana *qualification* zinazostahiki ambazo kigezo chake kmepitishwa na *WHO* ambaye ndio kiongozi mkuu wa mambo ya afya. Tumepata vyeti vya kuambiwa kwamba sisi tunaweza tukatoa huduma na tunatambuliwa na Baraza

la Madaktari. Kwa hiyo, asiwe na wasi wasi na sisi tunaweza kutoa huduma zinazotakiwa.

Lakini pia Mhe. Suleiman Hemed Khamis alizungumzia habari ya kituo chake cha Konde akasema kwamba wafanyakazi hawatoshi ni wawili tu kwa maabara, hakuna mfamasia. Mhe. Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba Kituo cha Konde katika wafanyakazi waliopelekwa wao ndio katika waliopata wafanyakazi wengi na kidogo kidogo tutajaribu kujaza nafasi zilizobakia.

Mhe., Naibu Spika, pia ningependa kutoa shukurani zangu kwa Mhe. Fatma Mbarouk Said sio kama wengine hawajawahi kwenda hospitali lakini ndio mtu pekee namshukuru sana tena sana kuona kwamba kuna wema wauguzi wetu huduma wanazozitoa. Huu ni ushahidi kwamba si wafanyakazi wote wa afya wana lugha mbovu. Mfano alioutolea ni huko huko *maternity* mimba nane si kidogo na zote hizo kapita salama. Kwa hiyo, wenye lugha mbovu wako lakini ni kidogo, tusiwachanganye wote wengine mpaka tukawafanya mtu sasa akitaka kuja afya akaanza kujiuliza maswali. Tupeni sifa pale tunapofanya mazuri kama alivyofanya Mhe. Mwakilishi, Mhe. Fatma nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kujibu baadhi ya masuala ya Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa kuhusu mrundikano wa wagonjwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kama tunavyofahamu ile ndio hospitali kubwa tuliyonayo. Kuna baadhi ya walioko hapo walisema kwamba pana watu ukiwafahamisha vipi watatoka wanakotoka kwenda Mnazi Mmoja Hospitali. Mara nyingi ndio hospitali ambayo inafanya kazi kwa masaa 24 kuliko nyenginezo. Kwa vile tunatoa huduma nzuri ndio maana watu wakawa wanakusanyika hapo, pangekuwa na huduma mbaya watu wasingekuja. Kwa hiyo, tunazidiwa sisi na watu pale lakini kwa kuwa ndio pao inabidi wote tuwahudumie. Ni kweli lakini hilo karibu litamalizika na mheshimiwa atakuja kulitolea ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa alizungumza kuhusu watoto wa kike kusomeshwa hata kama hawana fedha za kulipia na ikiwezekana waje walipe watakapomaliza. Mhe. Mwanaidi na mimi mwanamke mwenzio nakubaliana na wewe tuwape nafasi wanawake wasome. Lakini uzuri wa kwetu Wizara ya Afya hata kama ukitazama kitakwimu wanawake ndio tunaoongoza pale. Tunapokea ushauri na kwa sasa nataka nikuhakikishie kwamba kuna wanafunzi wengi wa kike katika kada zote na sasa kumejengwa hata majengo mapya ya hosteli ili kuwawezesha kusoma.

Sasa hivi tuna hosteli mbili moja wanaume moja wanawake, zinajengwa nyengine mbili watakaa wanawake watupu kwa hiyo watakuwa na hosteli tatu kuthamini tiba. Kumefanyika majaribio mbali mbali ili kuweza kuwaombea

wanafunzi wapate mikopo lakini jitihada hizo zimegonga mwamba. Lakini hata hivyo, suala hili tutalifanyia kazi na utaratibu wa kuangalia njia za kuwasaidia wale watakaoshindwa na malipo na hasa wale wanaotoka vijijini na kuthibitisha kuwa hawana uwezo wa kulipia.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa alizungumzia kuhusu *Mental Hospital* kuwa na wanawake wengi. Juzi nilipokuwa najibu swali hapa nilisema kwamba kuna sababu nyingi tu zinazofanya watu wapate maradhi ya akili. Lakini kama kuna kitu kimoja ambacho kinafanya wanawake waweze kupata maradhi mengi ni *tension*, uzito wa maisha, udhalilishaji na hilo lote limeelekezwa kwetu. Kwa hiyo, kwa hakika wanawake tutakuwa wengi *mental* mpaka hapo yatakapopunguka hayo.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa kumjibu Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak kuhusu wafanyakazi wanaouza dawa ambao hawana ujuzi. Tumelisikia hilo lakini kuna Bodi ya Madawa ambayo inaangalia maduka ya binafsi na hilo halijaripotiwa. Lakini kama hilo linatendeka tutashirikiana na Bodi ya Madawa tuone kwamba hayo hayatendeki kwa sababu mtu asiyekuwa na utaalam hapaswi kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumalizia kwa watu watatu waliobakia suala lao moja moja, kwanza ni la Mhe. Panya Ali Abdalla ambapo anataka wakunga wa jadi wathaminiwe. Mhe. Naibu Spika, ni kweli ushauri tumeupokea na unafanyiwa kazi nao karibu sio tu watapewa vitambulisho lakini hata na vitendea kazi kuweza kuboresha maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Rufai Said Rufai alizungumzia elimu ya afya kwamba iendelezwe kutolewa hasa kuhusu maradhi ya kichocho na matatizo ya dawa mgao wake hautoshi. Suala la kichocho linafanyiwa kazi kwa nguvu zote na mgao wa dawa sasa hivi kuna utaratibu uliobadilika kutoka ule wa kupelekewa dawa na kuomba dawa zile wanazozitaka wao. Kwa hiyo, wataomba kwa dawa wanazozitaka na kwa idadi wanayoitaka kulingana na wagonjwa wao, tutegemee kwamba mpango huu utasaidia kubadilisha tatizo hilo au kuliondoa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nimalizie kwa Mhe. Saleh Nassor Juma. Mhe. Naibu Spika, napenda nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa kuniona kati ya wengi mlioko hapa kwamba najibu vizuri, nafanya vizuri na shahidi walioko nje wanaonisikiliza, sijisifu lakini sifa nimepata. Halafu akaniomba kwamba kuna baadhi ya watu wanaokwenda dago wakirudi tuwapime ili tunusuru wanawake kwa sababu wanawake ndio wengi wanaougua ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nilikuwa najiuliza hawa watu dago wanakwenda wanaume watupu kule tena huo ukimwi unapatikana wapi. Nikaambiwa sio hivyo karibu na vijiji kuna wanawake kule, nikasema sawa sawa nimeshafahamu. Sasa kupima ukimwi ni jambo la hiari tutawashajihisha wakitoka huko wapimwe, kuwalazimisha itashindikana lakini tutajitahidi.

Halafu Mhe. Saleh Nassor Juma akazungumzia masuala ya chumba cha *ultra sound* Makunduchi, kweli na tunakifanyia matengenezo kwa hayo aliyoyashauri. Pia mengine yote ya vyumba vya maabara na wodi katika mpango huu wa kuhakikisha kwamba Hospitali ya Makunduchi inafikia katika kiwango cha Hospitali ya Wilaya yale yote yatarekebishwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba niwashukuru watendaji wote tulioshirikiana kufanya shughuli hii. Ahsanteni.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru tena kunipa ruhusa kusaidia kufanya ufafanuzi wa baadhi ya mambo ili Wajumbe wa Baraza lako tukufu waelewe tunachokifanya na tunachotegemea kukifanya na wakisha waturuhusu kutumia fedha tulizoomba.

Mhe. Naibu Spika, ningeanza kwa kutoa shukurani kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na mwenzangu amenipa sifa mimi nafikiri kwamba wanatupenda na kuwa wawazi kwa kutwambia yale ambayo wanayaona aidha ni mapungufu au ni mazuri yaliyomo kwenye Wizara ya Afya. Mheshimiwa pengine akisema kwa hamasa na uchungu kwa sababu sote tuliopo hapa hakuna kitu muhimu kuliko uhai, kama huna uhai maana yake hupo duniani na ukishakuwa unahitaji uhai ukiugua kimbilio lako hospitali.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambaye naona leo hayupo pamoja na wajumbe wake kwa ushirikiano aliotupa kufanya uchambuzi wa kumbukumbu na data zetu zinazohusu Wizara ya Afya na bajeti yetu na mara nyengine kutoa ushauri kufanyike mabadiliko machache.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia nikushukuru wewe kwa kutueleweshe na kuwapa nafasi wajumbe wengi tu mpaka wengine wakabaki. Kwa jumla waliochangia hawapungui wajumbe 37, kuna baadhi ya wajumbe wameleta michango yao kwa maandishi, ambao nao nimewaorodhesha. Nitawataja kwa majina na yule mjumbe ambaye sikumtaja sikusudii kumtenga. Nao ni:

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Assa Othma Hamad
3. Mhe. Salum Amour Mtondoo

4. Mhe. Abdi Mosi Kombo
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Asha Abdu Haji
7. Mhe. Rashid Seif Suleiman
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
9. Mhe. Subeit Khamis Faki
10. Mhe. Farida Amour Mohammed
11. Mhe. Hija Hassan Hija
12. Mhe. Hamza Hassan Juma
13. Mhe. Raya Suleiman Hamad
14. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
15. Mhe. Mohammed Haji Khalid
16. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando
17. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
18. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
19. Mhe. Mohammed Said Mohammed
20. Mhe. Rufai Said Rufai
21. Mhe. Panya Ali Abdalla
22. Mhe. Fatma Mabrouk Said
23. Mhe. Salum Nassor Juma
24. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
25. Mhe. Mwanaid Kassim Mussa
26 Mhe. Salim Abdalla Hamad
27. Mhe. Mohammed Said Mohammed

Mhe. Naibu Spika, kuna Waheshimiwa Wajumbe ambao walichangia kwa maandishi.

28. Mhe. Salma Mussa Bilal
29. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
30. Mhe. Nassor Salim Ali
31. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma
32. Mhe. Mgeni Hassan Juma
33. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
34. Mhe. Omar Ali Shehe na
35. Mhe. Salma Mohammed Ali

Mhe. Naibu Spika, inawezekana kabisa mjumbe mmoja au wawili nimewasahau, naomba waniwie radhi sikukusudia kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kumetolewa hoja nyingi baadhi nimesaidiwa na Mhe. Naibu Waziri wangu Dk. Sira. Kwa hivyo, sitozirudia, nitakaposahau nikazirudia ni kwa sababu nimeshindwa kutia alama.

Mhe. Naibu Spika, nianze na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Waheshimiwa wengi katika mjadala huu walizungumza sana pamoja na mambo mengine lakini kuhusu hospitali ya Mnazi Mmoja. Ni wachache mno ambao hawakuzungumza hoja ya Hospitali Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, mara nyengine pale nitakaposema hili limeshajibiwa ni kwamba nimejibu kwa pamoja kwa yale yanayostahiki.

Vile vile alisema kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja haifai kuitwa ya rufaa. Neno rufaa kwa kitaalamu ya afya ni mgonjwa anapotibiwa daraja moja kama vile kituo, akienda *Cottage hospital* maana yake anakwenda kupata rufaa, yaani anakwenda *stage* ya pili ya kutafuta matibabu bora baada ya lile daraja la kwanza.

Kwa hivyo, unaweza ukatoka kwenye kituo ukenda katika hospitali ya kijiji, ukenda hospitali ya wilaya, ukenda hospitali ya mkoa na mwisho ukafika hospitali kuu kama ile pale Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, daraja zote hizo ni rufaa. Kwa mfano ukitoka hospitali ya Makunduchi ukija hospitali ya Mnazi Mmoja ni rufaa. Ukitoka Kitogani kwenye kituo ukenda hospitali ya Makunduchi vile vile ni rufaa. Kwa hivyo, bado hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali ya rufaa kwa maana ndio hospitali yetu kuu na ndio yenye madaktari maalum kwa yale maradhi ya daraja za juu ambayo yanashindwa kupatikana matibabu yake huko vituoni.

Mhe. Naibu Spika, lengo la kwenda huko na kufikia rufaa kamili pale mambo tunapotegemea kuyafanya katika miaka miwili au mitatu ijayo kama nitakavyoeleza baada yatakapokua yametekelezwa. Hospitali ya Mnazo Mmoja itabakia kuwa ya rufaa, tunataka ifikie kiwango cha juu na tutafanya hivyo kwa kuendelea kuimarisha huduma zake na kiwango bora cha kuwapa huduma wagonjwa.

Vile vile alisema kwamba nguo zile za *theater* ni mbovu. Waheshimiwa Wajumbe tatizo la nguo za *theater* ni nguo ambazo ukishafanywa upasuaji mmoja, huwezi tena kuendelea nayo katika upasuaji mwengine mpaka ifuliwe, ihakikishwe kwamba haichukuwi matatizo ya mgonjwa huyu kwenda kwa huyo mwengine atakayefanyiwa upasuaji. Kwa hivyo, kuchakaa kwake ni mara moja.

Hata sisi kule kwetu Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na ngoma tunaita kauka nikuvae, kwamba hata ukitaka kwenda mazikoni kwanza ufuwe nguo ikauke uivae tena, ukitaka kwenda harusini kesho uifuwe uivae tena. Sasa nguo za *theater* ni za aina hiyo, zinahitaji kufuliwa mara kwa mara na hivyo kuchakaa kwake ni upesi. Nguo hizo zipo tunazo na zile zilizochakaa tutachukua juhudi kama tulivyoambiwa tununuwe nyengine. Wajumbe wanasema hapa kwamba

wakienda na wagonjwa wanatoleshwa pesa. Upasuaji unaendelea maisha yote haya na bila shaka madaktari wanavaa nguo na siamini kwamba wanavaa nguo hizo hizo. Hata hivyo tumelipokea hilo na tutanunua nyengine ili Mhe. Mshimba atakapokwenda azikute mpya badala ya zile kongwe.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mshimba alizungumza mchango wa baskeli na makusanyo mengine ya pesa ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwamba kwa nini hazipelekwi serikalini au hawapewi hospitali ya Mnazi Mmoja. Suala hili tumeshakubaliana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tangu mwezi wa Mei kwamba tukamilishe utaratibu fedha zote zinazokusanywa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja zifuate utaratibu wa kiserikali. Moja katika utaratibu wa kiserikali ni kwamba unapolipa upewe risiti ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, yaani vile vitabu vinavyostahiki ili vitowe nafasi kuhakiki na kufanya ukaguzi. Hilo tulikubaliana.

Jambo jengine ambalo tulikubaliana ni kwamba watatuletea watu wenye taaluma ya uhasibu wanane, ili wakae katika maeneo yote yanayokusanywa fedha za kuchangia kwa muda wa saa 24 ili tuepuke daktari, muuguzi, muhudumu au karani kukusanya fedha hizi. Yote hii ni kwa dhamira ya kudhibiti.

Vile vile tumekubaliana kwamba fedha zote hizo zitakazokusanywa hata kama zitakwenda hazina, kwa sababu walitushauri tufunguwe *account* inayoitwa *suspension account* ziingizwe huko na kisha waturuhusu zirudi tena Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, badala ya ile kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja inazikusanya na kuzitumia yenyewe, sasa itakuwa zinakusanywa kwa utaratibu wa kiserikali halafu zote zitarejeshwa hospitali ya Mnazi Mmoja kusaidia huduma za hospitali.

Mhe. Makame Mshimba pia alizungumzia habari ya mabusha. Tumejifunza kwamba kumbe yeye ni mshabiki sana katika kampeni hizi za mabusha. Tunapenda kumpongeza kwamba yeye ni mwanaharakati hodari na amejitahidi sana kushiriki katika kampeni yeye mwenyewe binafsi. Tunaomba kueleza kwamba kampengi ya matibabu ya mabusha inaendelea, wale wagonjwa wanaendelea kufanyiwa matibabu katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja na hospitali za binafsi, hata ile ya Al Rahma ina kumbukumbu zisizopungua watu elfu moja. Kwa hivyo, mkipeleleza siku hizi mjini hata vijijini kina baba wenye mabusha wamepungua sana. Hata yule mbu ambaye anaeneza maradhi hayo nao pia wamepungua. Tunategemea baada ya muda maradhi haya yatatoweka.

Vile vile Mhe. Makame Mshimba alizungumzia habari ya *lift*. Yeye alisema ameshaiona *lift* moja mpya ipo na ile nyengine inatengenezwa. Lakini akasema hapana, tusitengeneze kongwe mpya ikivunjika na kongwe ikivunjika ni vizuri

tukapata mpya. Tunakubali ushauri wake na tutajitahidi katika hiyo hiyo hali ngumu tuone vipi tunaweza kununua nyengine.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Makame Mshimba alizungumzia juu ya maposho, ambapo wajumbe wengi walilizungumza suala hili, kuhusu maposho ya madaktari na maslahi. Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na Mhe. Haji Omar Kheir Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wamelieleza hili kwa urefu na kwamba tutaongezwe asilimia 25 na kwamba zile *areas* zinaanza katika mwaka mmoja au miwili nyuma. Isipokuwa tunachopenda kueleza hapa ni kwamba suala hili linaangaliwa kitaifa na kuonekana kwamba wataalamu wetu tunawaenzi wa aina zote, sio madaktari tu. Kuna wataalamu tunawaita *backup support staff* wote pamoja na *orderly* mishahara itapanda na tunategemea kupanda kwa mishahara ya madaktari, ma-*nurse*, ma-*orderly* na wengine.

Kwanza ni kuondoa manung'uniko ya muda mrefu ya watu wetu wanaofanya kazi mahospitali. Pili ni kuwapa moyo kuonesha kwamba serikali inajali na kwamba maslahi hayo, naendelea kusema mimi sijaiona *scheme of service* ya serikali, lakini wataalamu wangu wananiambia kwamba tutakuwa hatuna tofauti kubwa sana, ingawa Mhe. Salmin Awadh Salimin alisema wakati nyinyi mnasogea pale walipo Bara na Bara wameshasogea zaidi. Sisi tutafanya hivyo kila uwezo wa serikali utakaporuhusu. Dhamiri ni kuhakikisha wale wachache waliokubali kupata tabu, maisha yote haya wengine wanakimbia na wao wanasema hapana, sisi hapa hapa ndio kwetu, dhamiri ni kuwapa moya, kuwapa haki zao na kulinda maslahi yao. Wale ambao wametoka nje kwa ajili ya kutafuta *green pasture* tunaita, washawishike warudi kuja kushirikiana na wenzao walioko hapa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kliniki ya macho na masuala mengine naona Mhe. Naibu Waziri alisaidia kueleza, kwa hivyo nanusuru wakati.

Mhe. Assa Othman Hamad alizungumza suala la matatizo ya sigara. Ni ushauri mzuri na kwa kweli moja katika sababu ya maradhi ya TB na mengine, inatokana na uvutaji wa sigara. Hivi sasa sisi tuna sheria yetu iko juu ya meza, sheria ya public health. Hili limeingizwa katika kudhibiti uvutaji wa sigara ovyo kama ni moja katika sababu ya kuchafua mazingira.

Mhe. Naibu Spika, sitaki kuwasema wavutaji sigara, lakini mara nyingi huwa hata hawajali kwamba anaweza kuwa kwenye daladala akavuta sigara bila kujua kwamba wengine anawaudhi. Tunawanasihi kama umekaa na mtu asiyevuta sigara, hebu jifiche kipembeni uvute kwa starehe zako peke yako. Lakini ikija sheria, haa! sheria itakukamata kwa sababu unatuongezea wagonjwa na hivyo kutuongezea matatizo ya matibabu.

Mhe. Assa Othman Hamad, alizungumza habari ya maradhi ya saratani kwamba yameongezeka. Ni kweli yameongezeka, lakini sababu mbali ya kwamba maradhi haya zamani yalikuwa sio mengi, lakini ni kwamba wengi wetu zamani tulikuwa hatuko na hadhari ya kujua hivyo. Sasa watu wanakwenda mahospitali kuna mabadiliko ya maisha, vyombo vya kufanyia uchunguzi sasa hapa kwetu vimeongezeka, zamani ni lazima uende Dar es Salaam au nje. Mara nyengine unaumwa na saratani unafikiri umerogwa, mambo hayo sasa yanapungua. Hali ya maisha yetu yamebadilika, tunakaa kitako sana, japo masafa madogo ni lazima kwenda kwa gari, zamani hata daladala mjini ilikuwa hakuna, unatoka Jang'ombe kwa miguu mpaka sokoni.

Kwa hivyo, mambo ya aina hii ni hayo mabadiliko ya mfumo wa maisha yamesaidia kuleta matatizo hayo. Lakini hata hivyo, tumesema hapa katika kujibu baadhi ya maswali kwamba tunafanya uchunguzi kujua sababu zikoje na kwa nini na halafu tutaeleza serikali na Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Mhe. Mjumbe alizungumza habari ya kwamba bajeti imepungua na kwamba miradi ya maendeleo kwa upande wa Pemba hakuna, kuna Unguja tu. Katika hotuba yangu ile nilisema kwamba miradi ya maendeleo tunayofanya ni miradi ya kitaifa. Ukishakuwa mradi wa maendeleo ni wa Unguja na Pemba, sasa inakuwa inategemea shughuli yenyewe.

Mfano mzuri Mhe. Naibu Spika, mradi wa *African Development Bank* ulitusaidia katika kuimarisha huduma za kinamama kutujengea nyumba 40 na baadhi ya vituo, vyengine kuvibomoa na kuvijenga upya na baadhi kuvitengeneza. Mradi ule nyumba 20 zimejengwa Unguja na nyumba 20 zimejengwa Pemba, lakini ni mradi tu sio kuwa ni mradi wa Pemba au mradi wa Unguja. Mara zote miradi ya maendeleo inakuwa ni kwa pamoja. Naomba kumueleza hilo kama ni mfano.

Mhe. Naibu Spika, katika fedha za kawaida idara yetu ya Pemba ina mafungu yake, kufanya makisio yake. Tukishapewa ile *ceiling* yetu na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tunakaa, tunakubaliana. Baada ya hapo fedha za Pemba zinakwenda moja kwa moja hazipitii afisi yetu kuu. Wakati wa *as basement* huwa zinakwenda kwa mafungu moja kwa moja. Masuala mengine alinisaidia Mhe. Naibu Waziri Dk. Sira. Kwa hivyo, sina sababu ya kupoteza muda.

Mhe. Abdi Mosi Kombo alijibiwa na Mhe. Naibu Waziri, kuhusu suala la kujenga chuo cha afya, alitaka kijengwe na Kaskazini. Masharti ya kujenga hivi vyuo kuna mambo ya kitaalamu, kuna suala la *catchments area, population* yenye uwezo wa kusoma, kuweza kukihudumia, walimu wataalamu. Sasa chuo chetu tulichonacho hivi sasa Mbweni mpaka sasa kinatosheleza na ameeleza

Mhe. Naibu Waziri kinapanuliwa kwa ma-*hall* na ma-*lecture hall*, ili kiweze ku-*cater* kwa Unguja na Pemba. Kulikuwa na mawazo ya kuwa tujenge Pemba. Tukasema kwanza tukiimarishe hiki cha Unguja, kiweze kusaidia Unguja na Pemba. Tusitizame suala hili kwamba ukishajenga chuo mwaka huu na mwakani, ujuwe kwamba kila mwaka itakuwa watu wanatoka.

Kwa mfano, Chuo chetu hivi sasa cha Mbweni kwa wastani kinatoa si chini ya wanafunzi 300 kwa mwaka, hivi sasa walioko wanaosoma ni kati ya 500. Kwa hivyo, ina maana mwaka huu 300, mwakani 3000, mwakani 3000 kwa miaka 10 maana yake ni 300. unaweza kujikuta umejenga vyuo halafu una *redundancy* au kwa maana hiyo labda usafirishe wengine. Japokuwa wengine watakuwa wanakufa na wengine watakuwa wanastaafu. Lakini hadi sasa chuo chetu tulichonacho kitatosha kuhudumia kisiwa chetu na tunategemea kukiimarisha kifikie hadi kiwe kinatoa digrii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu amezungumzia masuala mengi na kwanza alisema kuhusu hotuba ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilitoa kipaumbele kuhusu afya, lakini hali halisi alipochukua *data* na kulinganisha na akaona kwamba Wizara ya Afya iko nambari 4 au 5. Nadhani suala hili hakunielekeza mimi, alilielekeza kwa Waziri wa Fedha, kwa bahati mbaya hayuko nadhani angeweza kulitolea ufafanuzi.

Vile vile alieleza na kutupa sifa kidogo kuhusu utaratibu mzuri wa kupata huduma kwamba imeanza kuongezaka. Tunamshukuru kwa hilo na kwamba anataka tuweke mpango maalum utakaoonesha utaratibu. Alisema mara unaambiwa chumba cha upasuaji kiko juu, ukipanda unaambiwa kiko chini, ukishuka unaambiwa nenda kule. Kwa kweli taratibu za hospitali ya Mnazi Mmoja zinaendelea kubadilika na sikuja nacho kipande, lakini hivi karibuni mtaanza kuona kwamba kila mfanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja amevaa beji tena beji hiyo itakuwa na picha na jina.

Kwa hivyo, tunawaomba wale watakaokwenda kupata huduma badala ya kulalamika kila mara basi hata kama humwambii yule wewe piga jicho tu kwenye kifua chake, ukishaona jina pale basi tuambie kuwa huyu kanijeuri au huyu kanikashifu au huyu kanitolea maneno mabovu. Sisi tutakuwa tunajua tumfanye nini. Tunategemea pia kuna ofisi pale inaitwa *public relation office* inawezekana haijaimarika sana, lakini sasa tutaiimarisha na tutaitangaza iwe ni ofisi ambayo unapokuwa na tatizo lolote la kulalamika basi unakwenda kwenye ofisi ile unaripoti na yule bibi au bwana uliyemuona na picha yake unamwambia nimemuona Maryam Jecha kanifanyia hivi. Pale pale hatua itachukuliwa, kwa sababu ile ofisi itakuwa inafanya kazi masaa 24, ili kujenga heshima ya wananchi wetu na vile vile kulinda heshima ya kazi za afya.

Pia alizungumza habari ya kuwa na watu wengi wanaokaa kuhudumia wagonjwa. Suala hili hata sisi hatulipendi, lakini katika hali ya upungufu wa ma-*nurse* wa kutosha, wagonjwa wengine wanahitaji msaada wa huduma zaidi ya yule *nurse* mmoja. Lakini nayo tunaifanyia utaratibu, tutakuwa tunawaruhusu kama mtu mmoja au wawili ili waweze kukaa na ule wakati unaostahiki watakuwa hawaruhusiwi kukaa kwenye wodi huyo tu ndiye atakayeruhusiwa. Hivi sasa kumekuwa na tabia kwamba *Lailahaillah Wallah*, mkiwa kumi nyote mnakwenda kukizunguka kitanda cha mgonjwa, mwengine utamkuta kakaa kama vile anastarehe kwenye hoteli, sio vizuri.

Mhe. Naibu Spika, tunahitaji na wananchi wajirekebishe. Vijana wetu wale wauguzi wengine ni wadogo sana, mfano akimwambia mama huruhusiwi kukaa hapo kitandani. We mtoto wee, sasa na yeye ananywea. Mheshimiwa si hurusa kukaa kitandani. Wengine bwana. Kweli wafanyakazi wa afya ni wajeuri, lakini na sisi wengine ni jeuri bwana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando hayupo hapa, lakini mimi nimeshapewa ripoti pale kwetu Kivunge, mlinzi anawaambia jamani ngojeni watoke pale. Alipigwa utafikiri kule ndani kuna karamu ya biriani. Ziko hizo tabia za baadhi ya watu wanaokuja kutazama wagonjwa, pengine kwa sababu ya madhila ya mwanawe anaumwa au mama yake kumzuwia anaona kama vile unamnyima ile nafasi. Lakini jamani hospitali ina utaratibu wake. Ukenda polisi kuna utaratibu wake, ukenda shule kuna utaratibu wake. Sasa kama hatutaki kuufuata huo basi tutakuwa hatuna utaratibu wa kutawala. Kwa hivyo, tunawaomba wananchi na hilo walitambue.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na yeye alisema vile vile kwamba kuna tatizo la uaminifu, hiyo dawa ya kuweka vitambulisho tutaiondoa kwa sababu atakayemuomba pesa atamjua ni nani. Kasema pia kuna ongezeko la maradhi ya LCD hivi sasa. Jana tumemuita daktari wetu dhamana, sio vibaya kumtaja Dk. Faidha hivi sasa wanaendelea kufanya uchunguzi huo wa kwa nini mambo haya yanaendelea kuongezeka.

Vile vile alisema kwamba *maternity ward* wazazi wanahitaji kupewa staha, kwamba kuna kinababa wanaingia kule kwenye chumba chao. Tumelifuatilia suala hili na tumegundua kwamba kuna muhudumu mmoja ambaye ni mwanamme ambaye shughuli za kule *maternity ward*, mnajua jamani mara nyengine kutoa mifano sio vizuri, lakini hakuna kiwanda muhimu duniani kama kiwanda cha kuzalisha watu. Sasa zile harakati za pale mwanamke mmoja haziwezi ni nyingi za kwenda na kurudi kuchukua yale matatizo ya kina mama. Watu wa *maternity* wenyewe wamesema jamani kazi hizi mwanamke haziwezi anahitaji msaada. Lakini tumekubaliana kwamba yule bwana aishie pale mlangoni tu, kule ndani awaachie mama na stara zao. Tumesema hebu

tumwite isiwe na yeye anapenda kwenda kule kwa mapenzi yake badala ya kuambiwa aende. Tunasikitika kwa hilo kama lilitokea na tunawaomba radhi wale kina mama waliopata kufanyiwa yaliyokuwa sio mazuri au kuonekana wakiwa kwenye wodi.

Mhe. Naibu Spika, pia alizungumzia kwamba bajeti ya dawa ingeongezwa badala ya kutegemea DANIDA. Sio vibaya kuongezwa lakini tusisahau kwamba mwaka jana tulikuwa tumepewa na serikali milioni 300. Mara hii Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imejitahidi imetupa milioni 700. Wakati tunafanya hivyo, tuna maombi kutoka kwa wafadhili wengine mbali ya hawa waliotajwa na tunategemea nayo yatazaa matunda.

Mhe. Naibu Spika, suala nililotaka kusema na nitaendelea kulisema kurudia hapa ni kwamba jamani Serikali ya Umoja wa Kitaifa ina umri wa miezi saba. Mhe. Naibu Spika, juzi nilipokuwa nikitaniana na Mhe. Othman Masoud, nikamwambia Mhe. Othman. Maana mimi kila mtu namwita babu, nikamwambia babu wananihukumu kwa mimba ya miezi saba, akasema wanakuonea pengine itaharibika. Kwa hivyo, ni muda mdogo mno kutegemea kwamba matatizo yote tutaweza kuyatatua kwa miezi saba hii. Mnajua kwamba moja katika tatizo lililokuwa ni hadithi na kila mara, Mnazi Mmoja hakuna maji, watu wanachukua vidumu.

Mhe. Naibu Spika, nikasema hili bila ya maji hakuna uhai, basi baada ya miezi miwili tukalitatua. Lakini haya mengine yanayotaka fedha si masuala ya shikamoo, marahaba. *(Makofi)*

Kwa kweli haya na masuala ya utaratibu wa kupanga na kusema hiki tukose tufanye hiki. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe si vibaya kutoka milioni 3 mpaka milioni 7. Mhe. Naibu Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu mwakani tukija hapa itawezekana pengine nusu mahitaji ya dawa za serikali zikawa zinatolewa na serikali yenyewe. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu alieleza kwamba Hospitali za *Private* ni nyingi, yaani zinachipuka kama uyoga. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwa kiasi fulani zinapunguza matatizo ya hospitali zetu. Lakini napenda kukuhakikishia Mhe. Naibu Spika pamoja na Baraza lako tukufu kwamba haifunguliwi hospitali yoyote kama haijakaguliwa mazingira yake, mazingira yasipokuwa mazuri basi inafungiwa. Kwa mfano, tunamuuliza nani daktari wako, tukiwakuta madaktari ovyo nayo pia inafungiwa.
Kwa hivyo, usimamizi wa kuyafuatilia haya unafanyika na tunayo Kamati Maalum na hivi karibuni nilikuwa nimepata *document* kutoka kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kurekebisha ile sheria, ili kuifanya iwe kakamavu zaidi na kushirikisha hata Jeshi la Polisi kuona kwamba zile

Dispensaries ambazo hazifuati masharti basi tuzifunge na tuzipeleke Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Saratani ya Matiti. Kwa kweli ilifanyika research na nilieleza kwenye hotuba yangu pale na tuliwakuta baadhi ya akinamama watatu wanne tayari wameshapata na mimi mwenyewe nimeshapoteza shemegi yangu mmoja naye hivyo alijiona anakichungu kwenye nyonyo kumbe amekwisha.

Sasa hii inahitaji kampeni kubwa na Mhe. Naibu Spika, si vizuri kusema, lakini siku hizi Wizara ya Afya inapata kila ya watu. Kwa mfano, anakuja mtu anasema Mheshimiwa naomba msaada wako ninayo matatizo kwenye nyonyo na mambo mengine, basi moyo hupiga mtume amekwisha huyo, sasa kumwambia anayo kensa siwezi, basi utamwambia mama chukua hizi nende hospitali upesi.

Kwa kweli kuna haja kwa akinamama kufanya vipimo vya aina hii, kwa sababu dalili za Saratani ya Matiti huumwi, yaani unajiona tu umetunga kipele kwenye nyonyo na hata ukija ukifahamu basi umekwisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Sheria ya Afya ya Jamii, tunairekebisha na Mwenyezi Mungu akitujaalia Kikao cha Baraza kijacho basi tutaifikisha hapa ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka nayo izingatiwe. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman naye pia alizungumzia suala la kupewa kipaumbele Wizara ya Afya. Kwa kweli tunamshukuru kwa kuliona hilo na ni kweli kuna Kauli ya Abuja inayosema kwamba Nchi za Kiafrika mpaka itakapofika mwaka 2015 *fifteen percent* ya Bajeti za Serikali zipewe Wizara za Afya. Mhe. Naibu Spika, umuhimu huo umetolewa na viongozi na unastahiki kutekelezwa kila uwezo unaporuhusu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nirudie tena kwamba sisi tumeanza *Government of National Unity* mwaka huu, nategemea *percent* hii Mhe. Seif itaongezeka kila tunavyokwenda miaka ijayo na mpaka tutakapofika mwaka 2015 nategemea hatutopungua asilimia 10 mpaka 12 ya Bajeti ya Serikali. Kwa mfano, wenzetu Bara wamejisukuma kidogo na hivi sasa wako *twelve* na sisi tunahitaji kujisumuka na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo analijua hilo, lakini kupanga ni kuchagua lazima shughuli nyengine ziende.

Vile vile Mhe. Mjumbe alisema kuhusu suala la Elimu ya Afya ipewe kipaumbele. Kwa kweli tunashukuru kwa ushirikiano pamoja na maoni hayo. Kwa hivyo, tunacho Kitengo cha Afya ya Jamii ambacho kinajitahidi sana. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, alisema mbali ya upungufu wa bajeti bado wizara kuna mambo yanayohitajika, yaani katika hospitali yoyote iwe ya kijiji, kituo, basi kuna mambo ya msingi. Kwa mfano, usafi, godoro, kulala kitandani, Mhe. Naibu Spika alisema kumekuwa na tabia wakisikia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anakuja siku hiyo hospitali ndio inafyagiwa.

Kwa hivyo, alisema kuna haja ya kubadilika na kuna matatizo kwenye hospitali basi tuyaache yaonekane na wakubwa, ili tupate msaada. Mhe. Naibu Spika, tunashukuru kwa ushauri huo na tutajitahidi na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo. *(Makofi)*

Kwa mfano, juzi alikwenda Hospitali ya Mnazimmoja kwa ghafla na aliyakuta mambo aliyoyakuta, basi nilikwenda ofisini kwake kwa ajili ya kumpongeza kwa kunisaidia kazi. Kwa maana hiyo, tutajitahidi kusimamia hayo na pia kuyaeleza matatizo yake na badala ya pale alinipa ushauri kwamba nimeliona hili na lile na tunaomba hili ufanye hivi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia alisema kuhusu wafanyakazi wa zamu ya usiku wengine wanakuwepo ambao wameekewa zamu, lakini hawaonekani. Kwa kweli hili ni suala la usimamizi na tutaliimarisha na kama nilivyosema kwamba hivi sasa sote tumekubaliana na Wakurugenzi pamoja na watendaji wa Hospitali ya Mnazimmoja, kuwa si vibaya kufanya *duty roster*, yaani leo atapita nani hospitali na kesho, ili wale wafanyakazi wetu waone kumbe *the boss is looking at me*, kwamba kuna mtu ananiona. Kwa hiyo, tunashukuru kwa hilo.

Sasa aliuliza kuna mabadiliko gani yaliyojitokeza kwa upande wa maabara hususan katika Uchunguzi wa Saratani. Mhe. Naibu Spika, mambo haya kitaalamu nilielezwa, isipokuwa vipimo vimeongezeka kutoka 32 hadi 64 na kati ya hivyo ni vile vinavyohusiana na Saratani. Kwa kweli ushahidi wa hivyo ni kwamba tunao Mabingwa kutoka Spain pamoja na Turkey, ambao wanakuja kufanya *operation* za kichwa na nilisema juzi na leo nalirudia, yaani kichwa wanakipasua pamoja na mgongo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hivi sasa tayari wameshapasua kiasi *case* 105, yaani huwezi kufanya *case* hizo kama huna vipimo vya kutosheleza kwenye maabara pamoja na *Radiology* na *X-Ray*. Kwa maana hiyo, ile *CT Scan*, *Pathological* sehemu ya Uchunguzi vile vipimo vimeongezeka kiasi kwamba hawa madaktari wa nje wanaweza kuamini na kuja na kumpasua mtu.

Kwa mfano, kuna kiongozi wetu mmoja si vizuri kumtaja, hivi karibuni amepasuliwa mgongo nimemkuta New York tulikuwa sote kwenye ziara, nilimuuliza babu vipi aliniambia hivi sasa *smart*, yaani wamempasua hapa hapa

mgongo. Hivyo, hiyo ni dalili kwamba hali inabadilika kila siku zinavyokwenda na dhamira yetu ni kwenda huko. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ufanisi wa *CT Scan*. Kwa kweli tunakwenda vizuri na tumelieleza kwenye bajeti yetu, yaani tume-*save* si chini ya shilingi milioni 350/= kwa ajili ya kupeleka wagonjwa nje. Kwa mfano, leo nimearifiwa na watu wangu kwamba pale kwenye *CT Scan* wamepita watu 1,112 kwa ajili ya kupigwa *CT Scan*, hawa wote walikuwa usiku ukicha wanajaa kwenye boti na safari Dar-es-Salaam na sasa yote yanamalizia hapa hapa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, umebaki na nusu saa uangalie muda.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, *Inshaallah*. Kwa kweli nilitaka kueleza mengi, lakini mengi yaliyoelezwa yalikuwa yanahusu hali ya utendaji wa Hospitali ya Mnazimmoja, Uimarishaji wa Huduma za Afya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazimmoja kama nilivyosema kuna mradi mkubwa wa *ORIO*, ambao utahamisha Wodi ya Wanawaka pale itakuwa *Maternity* itajengwa kwenye Kiwanda cha Madawa cha zamani, Wodi ya Watoto, Huduma za *Out Patients* zote zitakwenda kule. Kwa hivyo, nyumba vyote ambavyo hivi sasa vinatoa huduma ya Hospitali ya Mnazimmoja vitakuwa vitupu kwa ajili ya kutoa nafasi ya kuvitengeneza kwa hayo masuala ya Kensa, Mkojo pamoja na Moyo. *(Makofi)*

Vile vile kuna suala la *Maternity* ambalo amelizungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Mhe. Mjumbe lazima ajibiwe kwa sababu yeye ni mpenzi sana wa hali ya *Theater*. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, napenda kumueleza Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwamba suala la *ICU* limetejwa na yeye, Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine na nitalijibu mwisho kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, tayari nimeshaeleza habari ya hali ya Chumba cha Upasuaji na mashuka. Vile vile alitaka kuelezwa kuhusu waandishi wa habari tunawazuia na wala mimi sijawazuia na kama mnakumbuka ni mara tatu au nne wakati niko safarini nikitumiwa *Email* kwamba leo kuna makala kubwa kuhusu *ICU* kwenye gazeti la *Daily News* au Jambo Leo ama Magazeti ya Nishati, yote yamekuwa yakiandika. *(Makofi)*

Kwa kweli kumekuwa na mawasiliano ya moja kwa moja baadhi ya wafanyakazi wetu na Redio Zenji kuhusu matatizo ya Wizara ya Afya. Kwa maana hiyo, hatuwazui waandishi wa habari na waje milango yetu iko wazi na tutawajibu watakayotuuliza na kila watakapoelewa wananchi, basi watakuwa wanatusaidia. Mhe. Naibu Spika, tunachowaomba wanapoandika mabaya, basi

na mazuri waandike na wala wasibaki kutusimanga tu, wakiliona jema nalo waseme kwamba sasa kuna mabadiliko. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki amelizungumza suala la *X-Ray* Micheweni. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na tatizo la daktari wa Micheweni, lakini yule alikwenda likizo na sasa tunatafuta mwengine kwa ajili ya kushughulikia suala hilo.

Vile vile amesema *Theater* ndogo. Kwa kweli Hospitali zote za *Cottage* nyumba vyake ni vidogo, kwa sababu ilijengwa kama ni Hospitali za Vijijini. Sasa katika kuziimarisha hospitali hizi tumeshaambiwa na hata Mhe. Rais wakati alipokuwa Makunduchi alituambia ni vizuri tujenge angalau wodi moja kubwa.

Pamoja na hayo, Mhe. Mjumbe alisema tatizo la kupooza. Wataalamu wanasema moja miongoni mwa sababu za kupooza ni ukosefu wa *Vitamin B Complex*. Kwa hivyo, namshauri Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwa jumla wale samaki tusiwauze tuwale, kwa sababu tunakwenda baharini kuvua samaki na baadaye kuwauza, halafu sisi tunachukua chakula kama vile ugali mwingi na pale juu kidaga kimoja, aa! Samaki wawe wengi kuliko ugali, ikiwa ni muhogo basi vichwa vya samaki viwe vingi kuliko muhogo. Kwa hivyo, suala hili linafahamika na wataalamu wetu na kimoja walichokigundua ni ukosefu wa hivyo *Vitamin B Complex*.

Mhe. Farida Amour Mohammed amejibiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Nikiendelea na majumuisho yangu sasa nije kwa Mhe. Hija Hassan Hija, alisimama kidete labda serikali haiko *serious* kuhusu afya. Mhe. Naibu Spika, naomba nimueleze Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwamba serikali iko *serious* tena inayo nia hasa. *(Makofi)*

Lakini ni kweli kwamba kuna sehemu kubwa ya bajeti ni fedha za nje, hiyo ni hali halisi kwa nchi zote. Kwa mfano, kuna fedha za aina tatu kwenye bajeti, zile zinazokusanywa ndani, zile zinazopatikana kwa njia ya misaada pamoja na zile za mikopo, sasa hizi zote ni fedha za serikali.

Sasa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ataeleza zaidi, kwa sababu ile bajeti nzima hapa ambayo tayari tumeshaipitisha hapa, tukiangalia miradi ya maendeleo ni asilimia 61 ni mikopo na fedha kutoka nje. Kwa hivyo, Wizara ya Afya nayo kuwa sehemu kubwa inategemea fedha kutoka nje si kitu cha ajabu, kwani ndio hali halisi.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka mwaka jana au juzi wakati nilipokuwa nikifuatilia Bajeti ya Muungano, ilikuwa asilimia 40 ni fedha kutoka nje na siku hizi wanajitahidi kama wanavyoweza ipungue hii. Kwa maana hiyo, suala la kutegemea misaada na mikopo kutoka nje haliwezi kuepukika katika umasikini tulionao, lakini kila siku vinavyokwenda basi mabadiliko haya yatatokea kutegemea na uchumi wetu unavyokua.

Sasa uchumi kukua maana yake tuekeze katika sehemu zotakazoongeza mapato na hiyo mara nyengine ndio inakuwa katika kugawa keki, kwa sababu keki unaitaka uile ibakie aa! Huku kunazalisha fedha tupeleke zaidi na huku hakuzalishi tupeleke kidogo na huyu akose, lazima katika hali hiyo tunaweza kuona michango ya kutoka nje si ajabu. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mjumbe alionesha pale fedha tulizotakiwa kuchangia katika Hospitali ya Mnazimmoja ilikuwa ni shilingi milioni 52 miaka ya nyuma, halafu imekwenda mpaka shilingi milioni 500/=. Mhe. Naibu Spika, ni kweli mwanzo tulitakiwa tuchangie shilingi milioni 52/= katika ile hali ya kawaida ni Kamati yao Mhe. Hija Hassan Hija alilosema sasa lazima fedha zinazochangwa Hospitali ya Mnazimmoja ziingie katika Mfuko wa Serikali. *(Makofi)*

Katika hali hiyo, wakauliza kwani hivi sasa Hospitali ya Mnazimmoja mnazipata kiasi gani katika michango ya wananchi, fedha hizi zote zilikuwa zinapatikana Hospitali ya Mnazimmoja kwa kuchangishwa wananchi, basi zilikuwa hazipungui shilingi milioni 441/=. Kwa hivyo, kule kuonekana kwamba sasa zimewekwa nyingi kwenye ile *vote* ya kuchanga imetokana na kuwa hivi sasa lazima zioneshwe. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, kule nyuma nilieleza kwamba Wizara ya Fedha tumekubaliana kama hata zitaingia mkono wa kulia basi zitarejeshwa tena mkono wa kushoto tupewe sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nieleze kitu kimoja ambacho inaonekana watu wengi hawakifahamu naomba unistahamilie. Kwa kweli Bajeti ya kuendesha ile Hospitali ya Mnazimmoja ni taasisi kubwa mno na wala si suala la kuitizama *maternity*, kwa sababu kuna vitengo pale havipungui 20, yaani ni utawala mkubwa sana. Kwa hivyo, bajeti ya kuendesha Hospitali ile ya Mnazimmoja ni *about* 2.8 *billions*, yaani ukitaka hasa iende kama taasisi.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazimmoja anaomba fedha hizo na hali ilivyongumu kwenye Wizara ya Fedha tunapewa shilingi milioni 189/= au 200/=. Sasa kwenye fedha za madawa tunasaidia kidogo na *DANIDA* pamoja na hii michango ya wananchi hizi shilingi milioni 400/= ndizo zinazozunguka katika hospitali kusaidia kupata huduma.

Kwa mfano, umekuja unataka kupiga *X-Ray* huwezi kusema ile picha haipo, ni fedha hizo ambazo zinakusanywa zinarudi kwenye Kitengo cha *X-Ray* kwa ajili ya kununulia zile *films*, huko *maternity* zinakokusanywa vinatakiwa vitu vya dharura, sasa fedha zile zinazokusanywa *maternity* ndio zinasaidia kwenye huko. Kwa hivyo, tunakwenda hivyo wakati tunajenga mtandao mzima wa marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, hapa ninayo *document* kamili ni muda mdogo tu, lakini miezi 7 tumefika mbali. Kwa hivyo, ninayo hapa *Document* of Mnazimmoja *Hospital 10 Years Strategic Plan*, tayari tumeshaimaliza, tunayo ya miaka mitano, pamoja na kila mwaka na tunategemea hapa Waheshimiwa Wajumbe muje mutuhoji baada ya miaka mitano, yaani 2015 tumefika wapi. *(Makofi)*

Kwa kweli tunayo malengo 9 ambayo ni *specific* kuifanya Hospitali ya Mnazimmoja kuwa Rufaa ya kweli. Kwa maana hiyo, si suala la kwamba serikali haiku serious Mhe. Mjumbe, isipokuwa inategemea ni ndondondo au chururu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nichupe kwenye Mkemia Mkuu na Waheshimiwa Wajumbe wamesema kwamba fedha zilizotengwa kwa Mkemia Mkuu ni kidogo. Kwa kweli mara hii tumetoa umuhimu kujenga Maabara ya Mkemia Mkuu jengo la kilichokuwa Kiwanda cha Sigara tumepewa kama vile tulivyopewa la Bohari.

Kwa hivyo, mara hii mradi wa Mkemia Mkuu umepewa umbele, ili wawe na jengo kabla hatujatoa umbele wa mambo mengine, ndio maana tukaona mara nyengine mambo haya inabidi mpe kuhu, tengeneza hiki na kile kisubiri. Sasa yule Mhe. Mjumbe aliyesema haungi mkono, basi tunamomba atuunge mkono, ili tuendelee kutekeleza yale yanayotuwajibikia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuna masuala mengine tayari yameshajibika. Lakini kuna mambo mawili kwa kumalizia naomba sana niyataje kwa pamoja na wale Waheshimiwa Wajumbe wengine ambao sikupata kueleza au kutoa ufafanuzi wa hoja zao moja moja, basi wanaomba wanisamehe. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kuna suala la Mhe. Hamza Hassan Juma alisema kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atoe kauli, mimi najifunza lakini kuna Kanuni hapa ya Baraza la Wawakilishi kifungu cha 27, ambapo naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 28 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi kinasema hivi:-

“Utaratibu wa Shughuli za Baraza.

(1) Ufuatao ndio utakaokuwa utaratibu wa shughuli za kila Kikao cha Baraza zitakazowepo katika kikao…

(h) Kauli za Waziri."

Mhe. Spika, hivi sasa tunazotaja na tunazojadili ni kauli za Waziri wa Wizara ya Afya.

Kwa hivyo, kauli inayohusu *ICU* anayestahiki kuitoa ni Waziri wa Afya kwa sababu yeye ni Waziri wa Serikali. *(Makofi)*

Vile vile kifungu cha 37 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 38 (1) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi kinasema hivi:-

"Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu…"

Mhe. Naibu Spika, ninayestahiki kujibu ni mimi tena kwa ukamilifu kama Waziri wa Afya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa heshima Mhe. Naibu Spika, mimi ndiye ninayestahiki kutoa kauli kuhusu *ICU* kwa niaba ya serikali na ninachokisema hapa kinasemwa na serikali na wala hakisemwi Juma Duni Haji. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kuisoma. Katika michango iliyokuwa inatolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu katika kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya, Wajumbe wengi walizungumzia kwa uchungu sana na hisia kali kuhusu hali ya Wodi yetu ya *ICU* katika Hospitali ya Mnazimmoja na kupelekea kutakiwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atoe Tamko la Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni nilizozisoma, basi mimi natoa kauli hiyo kama Waziri wa Afya kwa niaba ya serikali na kwamba ni serikali ndiyo inayoji-*commit* kwa kauli hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni kweli hali ya *ICU* hairidhishi na imo katika hali mbaya, ndio maana yake. Kwa kweli Hospitali yetu ya Mnazimmoja ikiwa ni Hospitali ya Rufaa kama nilivyoeleza kutokuwa na huduma ya *ICU* ya uhakika ni

mapungufu makubwa. Hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha kuona *ICU* inatengenezwa haraka iwezekavyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Bajeti ya Serikali ina maeneo makubwa matatu. Eneo la kwanza ni fedha zetu za ndani ambazo ni chache, eneo la pili ni misaada na eneo la tatu ni mikopo. Kwa hivyo, fedha zote hizi ni za serikali, ikiwa zimetoka kushoto au kulia ni fedha za serikali.

Kutokana na hali ya fedha zetu za ndani kuwa chache, basi tumewaomba rafiki zetu Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China watusaidie kuitengeneza upya *ICU* yetu na wamekubali kutengeneza mnamo mwaka huu. Lakini kama watashindwa katika kipindi cha miezi sita ijayo, basi serikali inakubali kuhakikisha kwamba *ICU* hiyo inatengenezwa kabla ya mwaka wa bajeti huu kumalizika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kutokana na *commitement* hiyo ya China tunaomba suala hili lifahamike hivi. Hata hivyo, kama Serikali ya China haitoweza kutimiza ahadi yake hiyo, jambo ambalo hatutegemei kutokea, basi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakata pua na kujengwa wajihi. Mhe. Ismail Jussa Ladhu anaijua kauli hii, anasema mara nyengine ukikata pua hata sauti hubadilika, badala ya kusema hamjambo basi ile sauti hutokea puani, yaani ikawa na king'ong'o. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba *ICU* kabla ya bajeti ijayo itakuwa *ICU* ya kisasa. Hata hivyo, kuanzia pale iliposasa ambapo si pazuri mpaka kuwa ya kisasa si suala la shikamoo, marahaba. Kwa kweli kuna taratibu za serikali za kutumia fedha za serikali.

Kwa maana hiyo, itabidi iitwe *tender*, wajenzi, uchunguzi na tayari watu wangu wamenipa kila kitu, yaani kunatakiwa *system* ya *oxygen* izunguke pote pale na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk anafahamu kuna zile *monitor*, yaani kila mgonjwa mmoja anastahiki awe na *nurses* wawili na *nurses* hao tayari wameshaanza kufundishwa na wala sio kama tumekaa tu kusubiri.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulishukuru Baraza hili tukufu kwa kuona umuhimu wa suala hili na kutaka serikali iingilie kati. Kwa hivyo, nawapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote waliochangia katika mada hii na pia naomba washirikiane na sisi katika kupitisha bajeti yetu kama vile tulivyosatahiki.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala jengine ambapo Mhe. Hamza Hassan Juma alieleza hapa alikuwa na wasi wasi kwamba fedha za Mradi wa *MDRI* ile *date relief* kuwa zililetwa hapa na badala ya kuzitumia kwa kujengea *ICU* labda

zimenunuliwa magari. Kwa hivyo, taarifa kamili ya nini kilichofanywa kwa fedha hizo na wala sitaki kumlaumu, kwa sababu yalipofanyika hayo yeye alikuwa ni Waziri wa Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu vipi Wizara ya Afya imetumia fedha *MDRI*. Kwa kweli *MDRI* ya kwanza ilikuwa ni dola 792 elfu na 81 na fedha hizi tumezitumia kama hivi ifuatavyo. Tumenunua hilo *CT Scan* aina ya *Siemens*, tumenunua *Fuoroscopy X-Ray machine* ambayo unaweza kuona mpaka tumboni kwako vile vijidudu vinavyotikatika.

Naomba kusema kwamba kuletwa kwa *CT-Scan* kumewezesha kufanyiwa operesheni za ubongo na uti wa mgongo wagonjwa 104 ambapo tungewapeleka nje wagonjwa hawa tungetumia milioni 520/=. Kwa hivyo, zimekuwa *saved* kwa sababu hiyo bila ya *CT-Scan* operesheni hizi zisingeweza kufanyika.

Fluoroscopy hii iliyonunuliwa ni *machine* ya *X-Ray* ambayo inafanya *special investigation* kama vile *IVP Barium meal and Barium enema*, yaani unatizamwe kwenye tumbo kama umechubuka mshipa.

Vile vile tukapata tena dola laki 770 elfu na 100 nazo tumezitumia kwa ajili ya kununulia vifaa sehemu ya wazazi, kama vile *Caesarian Section Set*, *Amputation Set* ile ya kukatia miguu, mashine inayokaa na kuzuia damu hapo hapo, yaani *Diathermy machine*, viti vitano vya meno, vitatu Unguja na viwili Pemba. Vyengine ni *Utral Sound* tatu, *Autoclave*, *Image Intensifier*, kulikuwa wakati mwengine tukitafuta *X-Ray* tunaiweka kwenye taa na kuiangalia, sasa ile mashine inaifanya iwe kubwa na kuona mpaka kwenye mfupa kumetokea nini, yaani ndani. Sasa vyote hivi vipo sasa kutokana na matumizi ya fedha hizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tumenunua tena *X-Ray* machine tatu katika Hospitali ya Mkoani, Wete na Mnazimmoja. Kwa hivyo, tunaomba kutoa taarifa kwamba fedha hizi hazikunuliwa magari, isipokuwa vimenunuliwa vifaa vya hospitali ambavyo sasa vinatoa huduma vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la mwisho kwa ruhusa yako Mhe. Salmin Awadh Salmin swahibu yangu, alizungumza kuhusu hali ya wazazi wanaokwenda hospitali kwa ajili ya kujifungua ni masikini sana na kwamba kuna fedha pale ambazo wanazotakiwa kutoa shilingi 40,000/= hasa kwa upasuaji.

Kwa kweli hili ni suala la msingi sana tena ni muhimu. Kwa mfano, kuna wakati nilikuwa katika shughuli za kusema juu ya jukwaa nilikuwa nikiwaambia watu kwamba mimi umasikini ninaujua, maana siujui kwa

kumuona mtu, isipokuwa nimeuishi, yaani naujua hasa. Kwa hivyo, ni kweli kwamba mama zetu ni masikini sasa mama yule akishajifungua bado unamwambia atoe pesa ni kitendo cha kuzingatia sana. Isipokuwa ninachoomba jambo moja waheshimiwa mimi ni mtu wa mahesabu na namba kidogo naweza kuzisoma, sasa kwa miezi sita iliyopita nawashika watu wangu wanieleze haswa kwani hasa ili mama apasuliwe kinahitajika nini na kiasi gani kazi hiyo wamekwenda mpaka tunaingia kwenye bajeti hawajamaliza juzi wananiletea *document* nawambia sasa hivi siwahi itabidi nikaogolee hivyo hivyo.

Kitu nilichoelewa ni kwamba kinamama wanaojifungua pale ni wa aina nne, kuna mama anajifungua uzazi wa kawaida kuna gharama yake, kuna mama anajifungua lakini njia yake ya uzazi ni ndogo inabidi asaidiwe ina gharama yake, kuna mama anajifungua lakini anatoka damu nyingi ina gharama yake na mama wa nne ni yule ambae kwa vyovyote hivi vya njia tatu hawezi ndio aende, sasa hilo nimelijua gharama sijakubaliana nazo nilitaka nizijue gharama niweze kuishauri serikali ipasavyo. Nilitaka nijue gharama nijue na mapato yanayopatikana sehemu nyengine Ex-ray, mlangoni, lebo, wapi na wapi ili ninapokuja hapa ninaweza kusema sasa gharama hizi zijaze hapa mlangoni. Mhe. Salmin Awadh akija na gari yake badala ya kutoa elfu tano atoe elfu kumi atakuwa amemsaidia mama wa kwangu na wa kwako, lakini hilo linahitaji utafiti.

Sasa ninaloliomba baraza hili na kumuomba Mhe. Salmin Awadh anipe muda ninahakikisha Oktoba nitakuja na jibu sahihi na inawezekana kabisa na mini ningependa moja katika juhudi zangu za kuwa Waziri wa Afya ndugu yangu na bibi yangu azae bila ya malipo hilo nalitegemea tutaliweza lakini naomba muda nilikamilishe kitaalam, nitakapokuja na jibu niwe na jibu sahihi kwa sasa naomba unipe muda nilishughulikie.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya masuala mengine yamejibiwa na Naibu wangu kuna baadhi ya masuala mengine yalikuwa ya kujirudia nikimjibu itakuwa nimejibu wengine, naomba wanistahamilie wale niliokuwa sikuweza kuwataja na kueleza moja moja. Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe sasa niwahoji wale waliokubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2011/2012 wanyoonshe mikono, waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Katibu: Waheshimiwa wajumbe ni kwamba tunapitisha mapato sasa *original* ilikuwa imo katika ukurasa wa 36 lakini kuna haya marekebisho ambayo yamesemwa na Mhe. Waziri kwa hivyo tutatumia hii *loose papet* ambayo imekuwa imegawanywa kwa wajumbe wote.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti ni kweli nikiwa mjumbe wa kamati ya Ustawi wa Jamii tulikubaliana kwamba mapato ya Wizara hii ambayo ni zaidi ya shilingi 52 ambazo Wizara ya Fedha waliwapangia, na kwa dosari za Wizara hii tulikubaliana kwamba sasa mapato yatakuwa ni milioni 537 lakini hoja yao ni kwamba walishindwa kuyakusanya vizuri kwa sababu walikuwa hawana washika fedha ambao wameahidiwa kutoka Wizara ya fedha kwa mwaka huu, baada ya leo bajeti hii kupita tayari kazi ya kusaili itaendelea.

Naomba nijue je wataalam hao kutoka Wizara ya fedha wamefika au fedha imekusanywa vipi naomba kujua.

Mhe. Waziri wa Afya: Nashukuru hivi sasa wawili tayari wamekuwa wakifanyakazi miezi miwili iliyopita na sita tunategemea kuwapata mara tu baada ya kumaliza bajeti hii.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, tuwasubiri kuwapa watu sita wakati jukumu la kusambaza wahasibu na washika fedha ni jukumu la Mhasibu Mkuu wa Serikali, nina hakika wafanyakazi hawa Wizara ya fedha wanao nina hakika kwamba makusanyo haya yatashindwa kukusanywa kwa sababu ya uzembe wa mtu mmoja, mimi naomba nipate maelezo Wizara ya Fedha kwa nini hujawapeleka washika fedha hawa nane wakati mnao wa kutosha hii kazi ikasimamiwa, badala yake mnawaachia wenzetu kufanya ukusanyaji ambao hauridhishi.

Mhe. Waziri wa Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya waziri wa Afya naomba kutoa maelezo kidogo juu ya suala ambalo Mhe. Hija Hassan Hija anataka ufafanuzi. Mhe. Mwenyekiti kama Mhe. Muwakilishi anavyosema kweli tunao wahasibu wengi lakini nataka niseme sio kila muhasibu unaweza kumpa dhamana hii ambayo tunataka

kuifanya Wizara ya Afya, hivi sasa tumeamua kwamba kuna baadhi ya wahasibu tuko katika mchakato wa kuwachunguza ili tukiwapeleka pale Wizara ya Afya waweze kufanya kazi kwa ufanisi. Nina imani kwamba zoezi hili tutalimaliza baada ya kupitishwa kwa bajeti hii ili tuweze kuwapeleka pale wale ambao tutakaoona sisi wanaweza kutusaidia katika kukusanya mapato kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, naomba tuendelee baada ya majibu ya Mhe. Waziri wa fedha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hotuba hii ya Waziri wa Afya rafiki yangu jamaa yangu, ndugu yangu, kaka yangu nilizungumzia katika suala zima la mapato kwa sababu walitupa kiambatanisho kilikuwa na a, b na c kitu kama hicho. Lakini kiambatisho cha C kilikuwa kinaelezea mapato ya *Ex-ray* milioni 35 ya mwaka 2011/2012 matarajio na mapato mengineyo yalikuwa miliioni 35. Lakini katika mwaka 2009/2010 kulikuwa kuna desh desh, sasa nilijaribu kumuuliza Mhe. Waziri je haya makadirio ambayo tunayategemea milioni 35 kwa upande wa makusanyo mbali mbali na milioni 15 kwa huduma za *Ex-ray* tulichukua vigezo gani kama huku nyuma hatukuchukua kumbu kumbu.

Sasa najua Mhe. Waziri alikuwa na mambo mengi kidogo na mengine alipitikiwa, sasa nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Kwa sababu tu muda ulikuwa finyu lakini maelezo kwa Mhe. Hamza nilikuwa nayo, yeye alitaka kujua hiyo miaka ya nyuma ilikuwaje. Kwanza wakati huo pesa zilikuwa zikikusanywa zilikuwa zinaishia kwenye Idara kwa hivyo ilikuwa hakuna suala la kuweka hapa kwa sababu zilikuwa haziji kwenye serikali, hivi sasa zinakuja kwenye serikali ndio zimeonyeshwa. Na kule Pemba alikouliza kulikusanya milioni 36,734,500 zilizokusanywa, kuna milioni 11 zimekusanywa kwa *Ex-ray* na Milioni 24, 834,500 kwa mapato mengineyo. Kwa hivyo nako kulikuwa na hayo makusanyo lakini yalikuwa hayaonyeshwi kwa sababu yalikuwa hayaji serikalini yameishia kule kule Pemba na yametumiwa kule kule Pemba kama vile ilivyokuwa Mnazi Mmoja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo mazuri tuendelee.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nikichangia niligusia juu ya hospitali yengu ya Mpendae nataka Wizara ijieleze hapa ni lini hospitali ile itatolewa tamko la kujengwa.

Mhe. Naibu Spika: Hiyo ni kwenye matumizi subiri kidogo.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango sera na Utafiti	1,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Kinga Unguja	21,000,000
Kifungu 0701	Idara ya Tiba Unguja	15,000,000
Kifungu 0801	Idara ya Tiba Pemba	50,000,000
Kifungu 1501	Hospitali ya Mnazi Mmoja	450,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**537,000,000**

Kifungu 0301	Wizara ya Afya	46,000,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe, Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikichangia juu ya hotuba ya Wizara ya Afya niligusia juu ya hospitali ya jimbo la Mpendae ambayo Mhe. Rais aliahidi na kuipandisha daraja hivi karibuni, sasa naomba wizara itoe tamko ni lini hospitali hiyo itajengwa, sikusikia katika majumuisho ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Hili ni agizo la Rais na hatuwezi kuacha kulitekekeleza kwa hivyo tunamuhakikishia Mhe. Muwakilishi kwamba litatekelezwa. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti ningemuomba Mhe. Waziri pamoja na kuwa ni ahadi ya Mhe. Rais lakini anipe *specific* ni lini hospitali ile itaweza kujengwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Kidogo ngumu kusema *specific* tunachoweza kusema ni kwamba tutaijenga na kabla hujaijenga lazime twende tukafanye makisio kwamba inahitaji kiasi gani ili ikamilike ili tuweze kufanya makisio na *engineer* wajenge, sasa ikiwa *specific* kidogo ngumu, lakini tunaahidi kwamba tutaijenga katika bajeti ya mwaka huu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Menyekiti kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi inaonyesha Mhe. Waziri ni mchapa kazi mzuri, kwa sababu alijaribu kuangalia hoja zangu akaangalia mantiki ya hoja zangu akaenda kwenye kanuni yote nimeridhika nayo.

Mhe. Mqwenyekiti najaribu kusema kwamba niliposema nitataka kauli ya serikali, tunajua mawaziri wanapotoa kauli ni kauli za serikali na kimsingi Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza hili na hata akiangalia kwenye Hansard yangu

nilitoa maelezo ya kutosha, kwamba suala la I.C.U pamoja na maelezo yote aliyoyatoa ukiacha pale mwanzo lakini na majibu aliyoyatoa sasa hivi Mhe. Waziri mimi bado sijaridhika nayo kuhusu suala la I.C.U kwa sababu amezungumza kwamba wameshazungumza na wahisani kama baada ya miezi sita hawajapata jawabu lolote pale serikali ndio itachukua hatua.

Mheshimiwa pale nilipozungumza tunataka kauli ya serikali kwa sababu tunajua sisi tuna fedha za msamaha wa madeni ambazo yeye pia alizitaja, fedha hizi nilizungumza kwamba inaonyesha waziri hajajenga hoja serikalini kwa sababu kama amejenga hoja serikalini kwa suala la umuhimu wa I.C.U fedha hizi zingelipatikana na nilitoa mfano. Kwamba fedha hizi hata katika awamu ya sita ambayo walizungumza pale mimi nilipokuwepo Waziri ni kweli tunakubali zilitumika vizuri na hiyo *city scan* na mambo mengine, lakini inaonyesha wizara suala la I.C.U hawakulipa *priorityi* hiyo *city scan* mtu ukishampeleka amezidiwa utamfanya nini. Bado sijaridhika na kauli ya Mhe. Waziri kwa kusema kwamba tuwasubiri wahisani baada ya miezi sita kama hawajatupa pesa ndio serikali ifanye kazi ile, kwa sababu bado tunaamini tuna fedha nyingi tumezihifadhi katika mfuko wa serikali kutokana na umuhimu wa I.C.U.

Mhe. Mwenyekiti, leo mimi hapa nikipata presha nikianguka ghafla mtanipeleka wapi, siwezi kukubali kwamba tunapitisha kodi za wananchi ambao sisi wenyewe tunapopata matatizo tukashindwa kuhudumiwa, nataka serikali itoe pesa kwa ajili ya kujenga I.C.U.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Hamza kwamba kama kauli ya serikali inasema itafanya kitendo tutafanya, lakini vile vile mengi tuliyoahidiwa na wachina yamefanyika sote tunajua kwamba hospitali ya Mkoani imejengwa na wachina, nyumba za Mkoani zimejengwa na wachina, kituoa cha macho hivi sasa ambacho Mhe. Hamza huwa anakwenda kimejengwa na wachina na kinahudumiwa na madaktari wa kichina.

Kwa hivyo naomba tuamini kwamba na hilo litafanyika na kama halikufanyika mimi nitajiuzulu. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uchapa kazi wa Mhe. Juma Duni Haji sitaki ajiuzulu lakini bado narejea tena Mheshimiwa ICU ni uhai wetu, suala la I. C.U sio suala la mradi mwengine wowote, wakati fedha tunazo tunataka I.C.U ijengwe sasa Mheshimiwa ukisema tunakubali wachina ni rafiki zetu wazuri basi hata sisi wenyewe katika masuala yetu ya umuhimu wa afya zetu sisi wenyewe pia mpaka tusubiri wafadhili. Mimi kama ungelinambia hakuna fedha hapo ningelikubali, lakini kwa kuwa fedha zipo kwa nini tusubiri wafadhili hawa wachina tuwape mradi mwengine wakati

tunahakikisha fedha zipo mimi sikubali suala hili kwa kusubiri wachina miezi sita mingi, hatujui mtu ataumwa lini hapa. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti hata mimi sitaki Mhe. Waziri wa Afya ajiuzulu, nataka nimhakikishie Mhe. Muwakilishi tukimaliza bajeti hii mimi na Waziri wa Afya pamoja na watendaji wetu tutaiangalia I.C.U kwa pamoja na tutachukua hatua za haraka ili kurekebisha kasoro zilizoko ndani ya I.C.U. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi ndio ninavyoipenda serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wale wanaofikiria kwamba Hamza Mkorofi na mtundu mtundu, lakini Hamza anasimamia masuali ya wananchi nimeridhika zana na kwa kuwa kauli imezidi kutiwa uzito, na kama nilivyosema sipendi Mheshimiwa mchapa kazi hodari ajiuzulu na kwa kauli ya rafiki yangu Mhe. Waziri wa Fedha, uchumi, Mipango na Maendeleo nimeridhika sana tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	85,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Kinga Unguja	104,590,000
Kifungu 0701	Idara ya Tiba Unguja	122,035,000
Kifungu 0801	Idara ya Tiba Pemba	229,914,000
Kifungu 0901	Idara ya Kinga Pemba	108,000,000
Kifungu 1401	Mkemia Mkuu wa Serikali Unguja	47,700,000
Kifungu 1501	Hospitali ya Mnazi Mmoja	

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya kwa kujibu masuala mengi ambayo waheshimiwa wajumbe wameuliza, lakini kuna suala moja ambalo wakati nilipokuwa nikichangia nilionyesha masikitiko yangu na nitakataka Mhe. Waziri anipatie jibu. Sasa sijui hili amelisahau au mimi mwenyewe sikuwa dhahiri wakati alipokuwa anajibu. Kwa hivyo kama amejibu naomba aniengeze zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia juu ya mwenendo ambao haupendezi wa madaktari wetu na wauguzi wa kwenda kazini na kufanya kazi bila ya kuvaa sare jambo ambalo halionyeshi kwamba linakwenda katika hali ya nidhamu, sisi tunapofahamu kwamba madaktari wana sare zao, wauguzi wana sare zao, wakunga wana sare zao na vyeo vyao. Sasa siku hizi kumegeuka mitindo unapokwenda katika hospitali hasa ya Mnazi Mmoja huwezi kumjua daktari yupi anayetibiwa yupi na anayekwenda kuangalia wagonjwa ni yupi. Lakini pia nimeangalia katika kifungu hiki cha hospitali ya Mnazi Mmoja haionyeshi kwamba kuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya *uniform* za wafanyakazi wa pale. Sasa hebu Mhe. Waziri tueleze kwamba ni kawaida hii au hakuna tatizo kwamba daktari asivae *uniform* ili kubainisha huyu ni daktari au vipi, lakini

kwa nini hakukutengwa hata fungu la fedha katika hospitali hii ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kununua *uniform* za wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Afya: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi tena kumueleza Mhe. Salmini Awadh juu ya Mnazi Mmoja, nakubali kwamba kweli suala la *uniform* halikujitokeza wazi hapa lakini fedha zilizowekwa hapa ni za jumla, nilipokuwa natoa maelezo yangu nilisema tunakwenda hatua kwa hatua. Ni kweli sare ni muhimu sana kama ilivyo sare ya Polisi, lakini kwa sababu suala la sare lilikuwa kwa muda mrefu halipo hatuwezi kwa mara moja ikawa kila mfanyakazi tutampa sare, lakini nakumbuka kwenye hotuba yangu nilipokuwa nikisoma niliahidi kwamba suala hili tutalishughulikia hatua kwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, naomba anipe nafasi tena kwamba hili tutalishughulikia lakini hatuwezi kulimaliza kwa mara moja, ndio maana nikasema kwamba kwa kuanzia kila mfanyakazi wa hospitali awe daktari nasi au *odaly* kwa sasa tutamtambua kwa kuvaa kitambulisho ambacho kina jina na picha, hiyo ni hatua ya mwanzo kuendelea kutekeleza wajibu wetu. Nia yangu sio kutekeleza *uniform* tu lakini kuna mengine makubwa ambayo tutawatekelezea wafanyakazi wetu lakini tupeni nafasi kidogo hatuwezi kufanya yote kwa mara moja. Naomba anikubalie anipe nafasi hiyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa maelezo ya Mhe. Waziri yanaonyesha nia ya kuondosha tatizo hili na kwa kuwa lengo langu ni kumueleza Mhe. Waziri juu ya matatizo yaliyokuwepo na namna ya kuweza kuonyesha namna ya kulitatua tatizo hili. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri alipe uzito jambo hili ili tunapokwenda pale katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tuweze kumfahamu nani daktari, nani sio daktari ili kuweza kujua na hivyo vitambulisha ambavyo amesema atavitoa basi navyo vitasaidia katika kuwafahamu wauguzi wako. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wakati nikichangia kwenye hotuba ya Mhe. Waziri nilizungumzia *Out Partient Department* kwenya chumba cha *emergence room* hakuweza kuitaja ni kipi kitafanyiwa marekebisho na kuweza kufanya kazi na kile ni kitu muhimu sana. Naomba maelezo ya ziada

Mhe. Waziri wa Afya: Naomba kumjibu Mheshimiwa katika hatua za matengenezo ya hospitali ya Mnazi Mmoja *Out Partient* yote tunategemea itahama itakwenda katika jengo jipya la viwanda na pale baadaye patatumika kwa shughuli za hospitali ya Rufaa. Kwa sasa hatua ya kutengeneza tunafanya kidogo kidogo kila hali inavyoruhusu. Namuomba kumuhakikishia kwamba

chumba hicho tutakitengeneza na meneja mkuu ananisikia juu kule kwamba itakuwa ni moja katika vile vinavyotengenezwa kwa dharura.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo mazuri ya Mhe. Waziri basi tutampa muda angalau atufanyie hicho kitu.

Kifungu 1501	Hospitali ya Mnazi Mmoja	272,178,000
Kifungu 1601	Mkemia Mkuu Pemba	7,396,000
Kifungu 1801	Huduma za Afya Wilayani Unguja	45,100,000

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamo wa Pili ra Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliobakia hautoshi kuweza kukamilisha shughuli iliyo mbele yetu. Na kwa kuwa leo ni siku ya Ijumaa tunaomba Baraza lako liridhie kuongeza dakika 15 mpaka saa 6:15 ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMZI

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Wakati nachangia nilizungumzia sana kuhusu huduma ya Afya ya Mama na Mtoto na nikaelezea jinsi wa Kituo kinachotoa huduma hii kilichokuwa Wilaya ya Mkoani kwamba kipo katika hali mbaya na kwa kweli hakina mazingira mazuri ya kuwahudumia akina mama.

Nilikuwa nataka nipate maelezo kwa Mhe. Waziri ni lini kituo kile watawahamisha akina mama kuwapa huduma ile ya afya ya mama na mtoto na kuwatafutia sehemu nyengine ambayo itakuwa ni nzuri kwa kuwahudumia.

Vile vile nataka maelezo Mhe. Mwenyekiti, juu ya lile jengo la ghorofa lililokuwepo pale Mkoani lilikuwa likitumika katika kutoa huduma ya afya ya mama na mtoto ambalo ni bovu. Nilieleza katika mchango wangu kwamba kuliacha vile ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi. Nilikuwa nataka Waziri anieleze lile jengo la ghorofa ambalo lipo pale Mkoani halitoi huduma yoyote. Ni lini watalifanyia ukarabati au kulitoa kwa wafanyabiashara

wakalikarabati halafu wafanyabiashara wakapata sehemu ya chini na wao wakapata sehemu ya juu kuwahudumia wananchi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma. Kuna mambo mawili aliyoyataka. Kuwahamisha wale akina mama wa MCH. Hilo nakubaliana na yeye na tutawahamisha.

Suala la jengo hatuwezi kuwapa wafanyabiashara kwa sababu ni jengo la serikali. tumekubaliana na wenzangu kwamba twende tukakague na tuishauri serikali ipasavyo. Hata kama italazimu basi livunjwe ili kunusuru maisha ya wananchi.

Mhe. Saleh Nasoor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye.

Kifungu 1901	Huduma za Afya Wilayani Pemba	41,600,000
Kifungu 2001	Idara ya Uendeshaji na Utumishi Unguja	6,342,906,000
Kifungu 2002	Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba	29,000,000
Jumla ya Kifungu		**2,496,094,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 2003	Idara ya Bodi ya Madawa	29,000,000
Kifungu 2101	Mfamasia Mkuu wa serikali	749,487,000
Jumla ya Fungu		**0,727,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niungane na wenzangu kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake fasaha kwa hoja tulizozitoa na hasa zile nilizozitoa mimi nashukuru. Naomba niulize suala moja ili turuhusu tuendelee.

Katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia *concern* yangu kwamba katika bajeti ya madawa ambayo ilikuwa inahitajika kama shilingi bilioni moja na nusu. Waziri alitwambia kwamba serikali imepanga kutumia milioni mia saba. Tukasema kwa nini hatuwezi kuzipata zote zile ambazo zinahitajika ambazo ni ziada ya shilingi milioni mia nane. Kinachonipa wasiti wasi Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Waziri nimeridhika nayo.

Lakini sasa ataje milioni mia saba nimeshindwa kuziona ninazotaka kuziulizia hapa. Nimeshindwa kuziona katika sehemu ya natumizi ya kawaida.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu, hii ni miradi ya maendeleo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nilikuwa nategemea kwamba sikuiyona huku kwenye fungu la kawaida nilitegemea nitaiyona katika fungu la maendelea chini ya Idara ile Mipango Uhusiano na Utafiti, lakini huku kwenye Idara ya Mipango, Uhusiano na Utafiti kwenye kazi za kawaida sikuliona wala kwenye fungu la Maendeleo sikuliona.

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa naomba radhi sijafahamu anachokihitaji.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nasema katika bajeti ya Waziri alitwambia kwamba fungu linalohitajika kwa ununuzi wa madawa zote zinazohitajika ni kama bilioni moja na nusu. Serikali ilijikubalisha kutoa milioni mia saba. Mimi nilitoa hoja kwamba hata hizo milioni mia nane zilizobakia zinapaswa zitafutwe. Kanipa maelezo kwa jumla kuhusu hoja hiyo, lakini kinachonishangaza hata hizi milioni mia saba nimeshindwa kuziona. Sikuziona katika lile fungu la matumizi ya kawaida chini ya voti ya ununuzi wa madawa na matibabu. Nikategemea labda lipo katika fungu la maendeleo. Katika fungu la kawaida hazipo hizo milioni mia sababa wala katika fungu la maendeleo hazipo. Naomba tusaidiwe fungu hili tutalipata wapi.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mheshimiwa lipo fungu milioni mia saba na tatu za madawa kwenye Idara ya Mfamasia huku tumeshapita fungu hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa nikichangia nilitia wasi wasi kwamba ukurasa wa 97 wa hotuba ya Mhe. Waziri alituomba fedha bilioni kumi na tatu milioni mia mbili ishirini na saba kama sehemu ya matumizi ya kawaida na bilioni mbili na nusu mchango wa serikali kwenye maendeleo. Lakini alisahau kutuomba fedha za wahisani ambazo pia ni fedha ya serikali. Sasa naomba maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hili naomba radhi nimeghafilika lakini lilikuwepo kwenye maelezo yangu. Ni ukweli kwamba nilipokuwa naomba fedha niidhinishiwe niliziomba za matumizi ya kawaida. Kwa kuamini kwamba kwenye matumizi ya maendeleo zimo kwenye buku hili. Kumbe ni kawaida na kwamba na matumizi ya maendeleo nazo niziombe pamoja.

Kwa hivyo naomba ruhusu kwamba nitumie hizi pesa za matumizi ya maendeleo kama vile inavyostahiki.

Mhe. Hija Hassan Hija: Naruhusu tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	6,708,401,000
Kifungu 0601	Idara ya Kinga Unguja	6,972,966,000
Jumla ya Fungu		**13,681,367,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makisio hayo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunawashukuru kwa mashirikiano mazuri na kuweza kuipitisha Wizara yetu hii na tunategemea jioni kusema wizara nyengine. Naakhirisha kikao mpaka Saa 11:00 za jioni.

(Saa 6:15 Baraza liliakhirishwa hadi Saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

TAARIFA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita Mhe. Waziri pana taarifa hapa kwamba katika ukumbi leo tumepata wageni kama ambavyo taarifa hii inavyojieleza. Tunaomba tuwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba leo tuna wageni wema wanatoka ***Ras gas ya Rasil hema*** inayoshughulikia mafuta na gesi. Wageni hao ni:-

1. Bwana Rund Abbma na
2. Bwana Gorge Silvester Oging

Wapo hapa na wote wapo juu pale wanaangalia shughuli zetu zinavyokwenda. Lakini baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe leo tutajadili hotuba ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, hivyo naomba mashirikiano yetu ili tuhakikishe kwamba kazi yetu tunaifanya vizuri. Ahsanteni.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa liingie katika Kamati ya Matumizi ili niweze kutoa maelezo kuhusu malengo yaliyomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla ya hapo naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia afya njema na uzima na kwa kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu kuwasilisha hotuba ya wizara hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wote wa wizara ninayoiongoza, napenda kuchukua nafasi hii adhimu, kumpongeza kwa dhati kabisa Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kuchaguliwa na wananchi kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hii inaonesha dhahiri kuwa wananchi wameweza kupima kwa kina na kuridhika na uwezo wake wa kuiletea maendeleo ya kweli nchi yetu kwa kuongoza Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, aidha nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kwao kuwa Makamo wa Kwanza Rais na Makamo wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Uteuzi wao unaonesha wazi imani ya Mhe. Rais kwao na kuamini kuwa watampa msaada na ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa tofauti katika kuitumikia nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa mmoja wapo wa wateuliwa hao, naomba nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais kwa imani yake kwangu ya kuniteuwa kuiongoza wizara hii. Namuahidi yeye, wananchi na Baraza lako tukufu kwamba nitaienzi imani hiyo kwa kutekeleza majukumu yangu ya nchi kwa uzalendo, juhudi na maarifa kwa kadri ya uwezo wangu. Inshalla Mwenyezi Mungu anisaidie, pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ni moja kati ya wizara kumi na sita (16) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wizara hii imeundwa na idara nane (8), Mamlaka mbili (2), Shirika moja (1), Mahakama

(1), Afisi ya Mrajisi (1), Bodi za Wakkurugenzi nne (4) na Afisi Kuu Pemba. Asasi hizo ni kama zifuatazo:-

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
ii. Idara ya Utumishi na Uendeshaji,
iii. Idara ya Ardhi na Usajili,
iv. Idara ya Mipango Miji na Vijiji,
v. Idara ya Upimaji na Ramani,
vi. Idara ya ujenzi,
vii. Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi,
viii. Idara ya Nishati na Madini,
ix. Mamlaka ya Mji Mkongwe,
x. Mamlaka ya Maji,
xi. Shirika la Umeme,
xii. Mahakama ya Ardhi,
xiii. Afisi ya Mrajis wa Ardhi,
xiv. Bodi ya Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo,
xv. Bodi ya Wakandarasi,
xvi. Bodi ya Nyumba,
xvii. Bodi ya Uhaulishaji Ardhi na
xviii. Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2010/ 2011, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM – 2005, kutekeleza Mpango Mkuu wa Taifa (*Zanzibar Vision 2020*) pamoja na Mpango Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA) wizara yangu iliweka kipaumbele katika kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa jumla, kwa kuziangalia zaidi sekta za maji na umeme. Utafiti wa pato la familia (*Household Budget Survey 2010/2011*) uliofanywa umeonesha kuwa hivi sasa asilimia 79.6 ya wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama Mijini na Vijijini, ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.6 kutoka asilimia 65 ya mwaka 2009/2010. Aidha, asilimia 82 ya Shehia zote nchini zimefikiwa na huduma ya umeme, ambao ni ongezeko la asilimia 2 kutoka asilimia 80 ya mwaka 2009/2010.

Mapato na Matumizi:
Mhe. Mwenyekiti, suala la ukusanyaji wa mapato ni kigezo muhimu sana katika kupima mafanikio ya utekelezaji. Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2010/2011 ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 2,361,619,000 kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato ya Taasisi zake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2011 jumla ya Tsh.1, 531,863,339 tayari zilikwishakusanywa sawa na asilimia 65 ya makadirio. Matarajio ya wizara yangu kuwa ifikapo Juni, 2011 tutakuwa tumefikia malengo yaliowekwa.

Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho “A”

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, bajeti ya wizara yangu ilikuwa ni Tsh 8,701,000,000. Kazi za maendeleo zilipangiwa Tsh .3,880,000,000 na kazi za kawaida zilipangiwa Tsh 4,821,000,000. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2011 wizara yangu ilikwishapatiwa Tsh.2,462,000,440 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 63 na Tsh.3,632,759,269 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 75 ya makadirio, hivyo kufanya jumla ya fedha zote zilizoingizwa kuwa ni Tsh 6,094,759,709 sawa na asilimia 70 ya makisio yote.

Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho “B1 na B2”

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2010/2011 NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kukamilisha muhtasari huu wa Mapato na Matumizi ya wizara yangu, sasa naomba uniruhusu kuelezea kwa kina utekelezaji wa kazi za kawaida na za maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 na malengo ya mwaka wa fedha 2011/2012 kupitia kila taasisi iliyomo ndani ya wizara hii.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

UTEKELEZAJI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango na Sera inaunganisha shughuli za wizara na taasisi zake zote, sambamba na kiungo na taasisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jumuiya mbali mbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali pamoja na kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa. Idara hii inawajibu mkubwa wa kusimamia na kuratibu kazi zote za wizara zikiwemo za kawaida na za maendeleo. Aidha, idara inasimamia Uajiri, Mafunzo, Nidhamu na Maslahi ya wafanyakazi waliopo na wanaostaafu. Pia idara inasimamia makusanyo ya mapato na matumizi ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Idara hii ilisimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ifuatayo:

i. Usambazaji Maji Vijijini
ii. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
iii. Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji

iv. Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira. (*AfDB*)
v. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Michenzani na Mpapa
vi. Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini.
vii. Mradi wa Kuweka Line ya Pili ya Umeme Ubungo hadi Mtoni (*MCC*)
viii. Mradi wa Kufunga Mita 10,000 za TUKUZA Unguja na Pemba
ix. Mradi wa Kuimarisha Shirika la Umeme (*FTA*)
x. Mradi wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati.
xi. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*)
xii. Mradi wa Kuijengea Uwezo Idara ya Mipango na Sera
xiii. Mradi wa Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari.
xiv. Mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Kupitia Sekta ya Ardhi (MKUMBITA)

Mradi wa Kuijengea Uwezo Idara ya Mipango na Sera.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka wa fedha 2010/2011, wizara imefanikiwa kuandaa ramani ya jengo jipya la wizara ambalo linategemewa kukidhi haja kwa mujibu wa mahitaji yake na Idara zake. Mradi huu vile vile umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuwapatia wafanyakazi wake mafunzo ya muda mfupi na mrefu ambapo wafanyakazi 5 wamesomeshwa kwa kupitia mradi huu.

Uendeshaji wa Kazi za Utumishi

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 wizara yangu imeendelea na jitihada zake katika kuangalia zaidi suala la rasilimali watu kwa kuwapatia fursa mbali mbali ikiwemo maslahi, hali ambayo imetoa mwelekeo mzuri wa ufanisi hasa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo wizara yangu imeweza kuajiri wafanyakazi 30 kwa kujaza nafasi zilizokuwa wazi kutokana na aidha kustaafu, vifo au nafasi mpya. Jumla ya wafanyakazi 40 wamestaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima, mfanyakazi 1 amestaafu kwa hiari, wafanyakazi 2 kwa kumaliza muda wa mikataba, na wafanyakazi 6 wamefariki dunia (Mwenyezi Mungu awalaze roho zao mahala pema peponi AMIN).

Mafunzo kwa Wafanyakazi

Mhe. Mwenyeiti, wizara imeendeleza juhudi za kuwajengea uwezo wafanyakazi wake katika viwango tofauti kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Jumla ya wafanyakazi 55 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu katika vyuo

mbali mbali vya ndani na nje ya nchi kwa viwango tofauti vya elimu. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi wizara imefanikiwa kuwapatia wafanyakazi 35 mafunzo ya vipindi vifupi ili kuwaimarisha wafanyakazi wake kiuwezo na kiutendaji, kwa kiasi kikubwa mafunzo hayo yamedhaminiwa na miradi mbali mbali iliyomo katika taasisi zetu yenye malengo ya kusaidia utendaji wa wizara pamoja na wafanyakazi wake.
Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia kiambatanisho C1 na C2.

Masuala ya Jinsia na Ukimwi

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011 wizara yangu imeyapa kipaumbele Masuala ya Jinsia na Ukimwi kwa kufanya mambo yafuatayo:-

i. Kuendelea na kutoa elimu kwenye masuala ya ukimwi na jinsia kwa wafanyakazi wa wizara ikiwemo kushajihisha wafanyakazi kupima afya zao kwa hiari.

ii. Kwa kupitia Mfuko wa Afya ya Dharura wa Wizara, wizara imeweza kuwasaidia wafanyakazi wenye matatizo ya kiafya.

MALENGO

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekusudia kuleta mabadiliko ya kiutendaji kwa Idara ya Mipango na Sera jambo ambalo limepelekea idara hiyo kugawanywa na kuwa na idara mbili tofauti ambazo ni:-

i. Idara ya Mipango Sera na Utafiti
ii. Idara ya Utumishi na Uendeshaji.

Lengo la mabadiliko haya ni kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa wizara kwa kuzingatia mipango yenye kutekelezeka, usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo ya kisekta, sera za wizara, pamoja na kuweka msisitizo wa uandaaji na usimamizi wa tafiti mbali mbali zinazohusiana na sekta zetu, ili huduma zetu ziweze kukidhi haja kulingana na maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kiteknologia. Mabadiliko haya vilevile yanakusudia kuimarisha utendaji wa rasilimali watu kwa kuzingatia kwa kina masuala ya nidhamu na uwajibikaji kwa watendaji.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Mipango Sera na Utafiti inakusudia kusimamina utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ifuatayo:

i. Usambazaji Maji Vijijini
ii. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
iii. Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)
iv. Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira. (*AFDB*)
v. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (*ADF12*)
vi. Mradi wa Uimarishaji wa Mji wa Zanzibar (*ZUSP*)
vii. Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini.
viii. Mradi wa Kuweka Line ya Pili ya Umeme Ubungo hadi Mtoni (*MCC*)
ix. Mradi wa Kufunga Mita 10, 000 za TUKUZA Unguja na Pemba
x. Uhuishaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme kwa Unguja (*JICA*)
xi. Mradi wa Matengenezo ya Kituo cha Umeme Mpendae
xii. Mradi wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati.
xiii. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE II*)
xiv. Mradi wa Utafiti wa Maji na Nishati Mbadala
xv. Mradi wa Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari Mizingani.
xvi. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Mpapa
xvii. Mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Kupitia Sekta ya
xviii. Ardhi (MKUMBITA)

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 1,930,454,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tsh 4,612,902,000 kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Mwenyekiti, idara hii inajukumu la kusimamia rasilimali watu pamoja na uendeshaji wa kazi za kila siku za wizara, katika kutekeleza majukumu hayo idara imelenga kutoa kipaumbele katika masuala ya nidhamu, uwajibikaji, mafunzo, maslahi na kusimamia mafao ya wafanyakazi wanaostaafu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile idara inakusudia kuimarisha utendaji kwa kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kazi ili kuongeza ufanisi katika utendaji sambamba na kuhakikisha kuwa haki na wajibu vinapewa nafasi sawa na hatimae wizara iweze kufikia malengo yaliokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako tukufu

liidhinishe jumla ya Tsh. 495,296,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA ARDHI NA USAJILI

UTEKELEZAJI

Usimamizi wa Ukodishaji Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya mikataba 38 ya ukodishaji ardhi ilitiwa saini na kupewa wawekezaji mbali mbali, miongoni mwa mikataba hiyo, 24 ni kwa ajili ya mahoteli, 4 kwa ajili ya vituo vya mafuta, 3 ardhi kwa kilimo na **7** kwa ajili ya minara ya mawasiliano ya simu za mikononi.

Utayarishaji na Utoaji wa Hati.

Mhe. Mwenyekiti, uendelezaji, utayarishaji na utoaji wa hati pamoja na ubadilishaji wa hati za zamani na kupatiwa za kisasa unaendelea kwa mujibu wa sheria. Jumla ya hati za zamani 210 zimebadilishwa na waombaji kupatiwa hati mpya. Hati za muda *'Provisional Certificate of Right of Occupancy'* 828 zimetolewa kwa maeneo mbali mbali.

Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za ardhi:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza mfumo mpya wa uwekaji kumbukumbu za ardhi na kutumia njia za kisasa (*computerisation*) ili kurahisisha uwekaji na upatikanaji wa kumbukumbu hizo, Idara tayari imekusanya kumbukumbu katika maeneo ya Mazizini *Unit* 34 (*LD*), Chukwani *Unit* 39 (*HD*) na Mombasa *Unit* 33, 32, 32B, vile vile katika maeneo ya Mwanakwerekwe *Unit*, 22, 21 na Amani Magogoni *Unit* 20, Tunguu *Unit* (3,4,5,6,8,9 na 10) na Kijichi (*Block A,B,C.*)

TATHMINI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ardhi na Usajili katika mwaka wa fedha 2010/2011 iliendelea na kazi zake za tathmini kwa ufanisi mkubwa. Jumla ya kazi 244 zimekamilika na kukabidhiwa wenyewe, kazi hizo ni kutoka katika taasisi mbali mbali, kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho "D".

Kuimarisha Udhibiti wa Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha udhibiti wa matumizi ya ardhi, idara iliendelea kutekeleza kazi za ukaguzi wa maombi ya ujenzi kutoka Baraza la Manispaa na kuyafanyia kazi kisheria kama inavyoonekana katika jaduweli nambari 1.

Jaduweli nambari 1.

AINA YA MAOMBI	IDADI YA MAOMBI	MAOMBI YALIOKUBALIWA	MAOMBI YALIOKATALIWA
Ujenzi wa Nyumba Mpya	38	32	6
Matengenezo Madogo Madogo	18	14	4
Jumla	56	46	10

AFISI YA MSAJILI WA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Msajili wa Ardhi inaendelea na kutekeleza shughuli zake za Usajili wa Ardhi nchini. Zoezi la majaribio ya usajili wa ardhi limeanzishwa katika Kijiji cha Wara, Shehia ya Mkoroshoni, Wilaya ya Chake Chake Pemba. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Afisi ya Msajili wa Ardhi imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kuendeleza shughuli za majaribio ya Usajili wa ardhi katika Kijiji cha Wara Shehia ya Mkoroshoni Chake Chake Pemba. Shughuli hizo ambazo zinafadhiliwa na Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*).

ii. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Maofisa wa Kitengo cha Utambuzi wa Ardhi wanaendelea kuwapa maelekezo watendaji wa Afisi ya Usajili namna ya njia bora ya utekelezaji wa kazi hiyo.

iii. Kuendelea na ukusanyaji wa fomu zilizogawiwa kwa wananchi wa eneo la Shehia 13 za Ng'ambo zilizobaki na kuendelea kugawa nyengine kwa watu ambao hawajapewa. Vile vile Kitengo cha Utambuzi kitaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili

kuelewa suala hili la usajili kwani uzoefu imethibitika kuwa wananchi bado hawajapata muamko unaostahiki.

MAHAKAMA YA ARDHI:-

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi imeendelea kupokea na kuziamua kesi mbali mbali zinazohusiana na migogoro ya ardhi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya kesi 306 zilifunguliwa, kwa ufanunuzi zaidi naomba muangalie Kiambatanisho "E".

BODI YA UHAULISHAJI ARDHI:-

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Uhaulishaji Ardhi kazi yake kuu ni kupokea, kujadili na kupitisha maombi ya uhaulishaji ardhi Zanzibar. Katika kuhakikisha hayo taratibu za uhaulishaji zinaanzia ngazi ya Shehia na Wilaya. Vile vile inawahusisha Mhaulishaji na Mhaulishwaji kwa pamoja na inapobidi hata wahusika wenye manufaa ya karibu zaidi ya kinachohaulishwa kwa upande wa Mhaulishaji.

Kazi za Uhaulishaji

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza utekelezaji wa majukumu yake Bodi ya Uhaulishaji Ardhi imeweza kupokea maombi mbalimbali kwa upande wa Unguja na Pemba ambapo inaonekana wananchi wameanza kuhamasika na kuelewa umuhimu wa Bodi hii.

Hadi kufikia Machi, 2011, jumla ya fomu za maombi 251 ziliwasilishwa idarani ambapo maombi 205 yalikubaliwa, 15 yalikataliwa na hatimae hati 175 zilitolewa.

MALENGO

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Ardhi na Usajili imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na kubadilisha hati za zamani na kuwapatia wananchi hati mpya na kutoa hati mpya kwa watakaopewa viwanja.

ii. Kuendeleza uwekaji kumbukumbu za viwanja kwa njia za kisasa.

iii. Kuendelea na kuimarisha shughuli za Mahakama kwa lengo la kupunguza migogoro ya Ardhi nchini kwa haraka na kushirikiana na Idara ya Mahakama Zanzibar katika kuwapata mahakimu watano wa Mahakama hiyo ambao bado hawajapatikana.

iv. Kuendelea na utambuzi na uthibitishaji wa wenye haki ya matumizi ya ardhi ndani ya Shehia za Ng'ambo ya mji wa Zanzibar na huko Pemba na kuanza shughuli za Usajili wa ardhi kwa maeneo ambayo zoezi la Utambuzi zimekamilika.

v. Kuendelea kusimamia shughuli za Ukodishwaji wa Ardhi *(Land Leases)* nchini na kuondoa msongamano wa wasiohusika na kazi hizi.

vi. Kuimarisha Udhibiti wa Umilikaji wa matumizi endelevu ya ardhi na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaovamia ardhi.

vii. Kusimamia shughuli za Uendelezaji wa Bodi ya Uhaulishaji Ardhi.

viii. Kufanya uthamini, uhaulishaji na ugawaji wa ardhi kwa shughuli mbali mbali ikiwemo kilimo, makaazi na biashara ili kukuza kipato cha wananchi wa Zanzibar.

ix. Kufanya mapitio ya Sera ya Ardhi pamoja na kuboresha Sheria mbali mbali za ardhi kwa ajili ya matumizi na udhibiti bora.

x. Kutunza na kuimarisha maeneo ya ukodishaji wa ardhi kwa kuhakikisha kwamba wanaendesha shughuli zao kwa mujibu wa makubaliano yalioainishwa kwenye mikataba na miongozo ya matumizi ya ardhi.

35. Mhe. Spika, ili Idara ya Ardhi na Usajili iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 524,135,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA UPIMAJI NA MIPANGO YA MIJI

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Idara ya Upimaji na Mipango ya Miji iliweza kutekeleza majukumu yake iliyopangiwa kama ifuatayo:-

Kuzifanyia Mapitio *(revision)* Ramani mpya za Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kufanikisha zoezi hili kazi inayoendelea hivi sasa ni kuzifanyia mapitio na uhakiki ramani hizo ili kuingiza taarifa mpya ambazo tunazo hivi sasa pamoja na kurekebisha makosa madogo madogo yatakayogundulika.

Kazi hii ni endelevu na inaendelezwa kwa kuutumia kikamilifu msaada wa kiufundi na kitaalamu kutoka mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira *(SMOLE).*

Kupima Viwanja vya Makaazi, Huduma na Mashamba Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kazi za upimaji wa maeneo ya makaazi, huduma za kijamii, mashamba ya wananchi na maeneo ya vitega uchumi zinaendelea Unguja na Pemba. Katika kipindi hiki kiasi ya viwanja 520 vimeshapimwa katika maeneo mbali mbali nchini.

Kuendelea na kazi za Upimaji wa Mipaka ya Mikoa na Wilaya.

Mhe. Spika, kazi hii ilipangwa kutekelezwa kupitia mradi wa *MACEMP*. Matayarisho yote ya kazi hii ikiwemo utayarishaji wa ramani za mipaka ya Mikoa na Wilaya pamoja na gharama zake yamekamilika. Kinachosubiriwa kwa sasa ni upatikanaji wa fedha ili kazi iweze kuanza.

Kuendelea na Kazi za Udhibiti Ujenzi kwa Kushirikiana na Taasisi nyengine za Serikali.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara iliendelea na kazi za udhibiti wa ujenzi Mijini na Vijijini. Idara ilishirikiana na Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji ya Pemba na Halmashauri za Wilaya Unguja katika kuyapitia na kuyathibitisha maombi mbali mbali ya ujenzi.

Hata hivyo, bado juhudi zaidi zinahitajika katika suala zima la udhibiti ujenzi nchini hasa katika kuziimarisha kisheria, kiutendaji na kitaalamu Halmashauri za Wilaya pamoja na Mabaraza ya Miji na Manispaa. Vyombo hivyo ni wadau wakubwa katika suala zima la udhibiti ujenzi na inapaswa viimarishwe.

Kuendelea na Kutayarisha Ramani za Mapendekezo ya Matumizi ya Ardhi .
Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ilifanya kazi hiyo katika eneo la Tunguu pamoja na maeneo mengine yaliyotokana na maombi ya wananchi na taasisi mbalimbali. Ramani hizo ni muhimu sana kwani ndizo zinazotoa sura ya mji au kijiji husika na pia zinasaidia kuondosha migogoro inayoweza kujitokeza wakati wa upimaji au uendelezaji wa maeneo.

Kuendelea kutayarisha Ramani za kina *(details plans)* za Matumizi ya Ardhi katika Vijiji vya Ukanda wa Pwani kwa Kushirikiana na Mradi wa *MACEMP*.

Mhe. Spika, kazi hii ilitarajiwa kuanza rasmi mwezi wa Aprili 2011, chini ya mradi wa *MACEMP* baada ya kukamilika utayarishaji wa ramani za kina katika ngazi za Wilaya.

Utekelezaji wa Mradi Endelevu wa Usimamizi wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira *(SMOLE).*

43. Mhe. Spika, mradi wa *SMOLE* awamu ya pili umeanza kutekelezwa kuanzia Januari, 2010 na utakamilika 2013, chini ya msaada wa Serikali ya Finland na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
Kazi ambazo zimefanywa na mradi huu kuanzia Januari , 2010 hadi Machi 2011 ni kama zifuatazo:-

i. Mradi umeweza kusaidia baadhi ya gharama za utekelezaji wa kazi za Idara kama Upimaji wa viwanja katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba.

ii. Kuendeleza uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za ardhi *(Land Information)* na kumbukumbu za umiliki wa ardhi kwa madhumuni ya usajili wa ardhi *(Land Registration)* na uhifadhi wa kumbukumbu za Mazingira *(Environmental Information)* za Unguja na Pemba.

iii. Kusaidia katika ununuzi wa vifaa vya ofisi vya Idara hizi kama vile kompyuta, magari ya kufanyia kazi, vifaa vya upimaji ardhi na vifaa vya uchunguzi wa mambo ya mazingira

iv. Kutoa elimu kwa jamii katika matumizi bora ya ardhi na uhifadhi wa mazingira kwa kuandaa semina na kutumia vyombo vya habari –TV, Radio na Magazeti.

v. Kuendeleza tafiti mbali mbali za usimamizi wa ardhi na uhifadhi wa mazingira katika visiwa vya Unguja na Pemba, ambazo matokeo yake yatatumika katika kuandaa sera mpya ya ardhi nchini itakayosaidia usimamizi na matumizi bora ya ardhi.

vi. Wafanyakazi wa Idara hizi wanaendelea kupatiwa mafunzo ya ndani katika kazi za utayarishaji ramani, utumiaji wa vifaa mbali mbali vya kisasa vinavyotumika katika kazi za upimaji wa ardhi.

vii. Kusaidia uanzishwaji wa Afisi ya Mrajis wa Ardhi Pemba pamoja na kuanzishwa kwa uhakiki ardhi (*land adjudication*).

viii. Uhakiki wa eka tatu kwa Unguja unaendelea katika kuandaa *Data base*.

ix. Kusaidia kuandaa mpango na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu (nchini Tanzania) wafanyakazi wa Idara hizi.

Mhe. Spika, Idara pia imo katika hatua za mwisho za kuanza utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara-Tanzania (MKUMBITA) *(Business Environment Strengthening for Tanzania- BEST)* na Mradi wa Uimarishaji wa Mji wa Zanzibar *(Zanzibar Urban Service Project - ZUSP)*

MALENGO

Mhe. Spika, kabla ya kueleza malengo, naomba kuchukua fursa hii kulijuilisha Baraza lako Tukufu kwamba, katika muundo mpya wa Wizara ya Ardhi , Makaazi, Maji na Nishati, Serikali imeamua kuigawa Idara ya Upimaji na Mipango ya Miji katika Idara mbili tofauti ambazo ni :-

i. Idara ya Mipango Miji na Vijiji na,
ii. Idara ya Upimaji na Ramani

IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI

Kwa upande wa Idara ya Mipango Miji na Vijiji, kazi zifuatazo zimekusudiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012:-

i. Kuratibu na kusimamia kazi zote za Mipango ya matumizi bora ya ardhi nchini katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Miji na Vijiji.

ii. Kutayarisha mpango wa matumizi bora ya ardhi nchini *(National Land Use Plan).* Ili kufikia mpango huu, Idara hii itaangalia upya mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya mwambao *(Coastal Zone).*

iii. Kuangalia na kutayarisha upya mfumo mzima wa mipango ya uendelezaji wa maeneo mapya ya makaazi pamoja na huduma mbalimbali.

iv. Kutayarisha Mipango bora ya kuyarekebisha na kuyaendeleza *(Improvements Plans)* maeneo mbalimbali ambayo yalijengwa bila ya mpangilio unaokubalika.

v. Kuendeleza mashirikiano na Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji pamoja na Halmashauri za Wilaya katika kazi za Udhibiti ujenzi katika uendelezaji wa Miji na Vijiji. Taasisi hizi zitahitaji kuelimishwa vya kutosha, ili wasikiuke mipaka ya majukumu yao.

vi. Kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na maendeleo na ukuaji wa Miji na Vijiji nchini, kwa kushirikiana na taasisi nyengine za Serikali na Washirika wa Maendeleo ndani na nje ya nchi.

vii. Kuijengea uwezo Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi wake

Mradi wa Uimarishaji wa Mji wa Zanzibar *(Zanzibar Urban Service Project - ZUSP)*

Mhe. Spika, Mradi wa *ZUSP* unaratibiwa na Ofisi ya Rais-Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Idara ya Mipango ya Miji na Vijiji inahusika katika utekelezaji wa mradi huo katika masuala yote yanayohusu maendeleo ya Mji. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 kazi zifuatazo zinakusudiwa kutekelezwa chini ya mradi huu ni :-

a. Kuandaa Hududi Rejea *(Terms of Reference)* kwa Washauri Waelekezi

b. Kutoa matangazo ya kutafuta Washauri Waelekezi wa kutayarisha mpango wa kuweka mazingira bora ya Mji

c. Kuchagua Mshauri Mwelekezi kufuatana na taratibu za Benki Kuu ya Dunia.

d. Kuandaa mpango kazi wa kutekelezwa na Mshauri Mwelekezi wa kukamilisha kazi hiyo.

Aidha kazi hii itajumuisha taasisi mbali mbali za Serikali katika kuandaa mpango huu ulio bora zaidi wa mazingira ya Mji wa Zanzibar.

Mradi wa Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara Tanzania *(Bussiness Environment Strengthening in Tanzania- BEST)*

Mhe. Spika, Mradi wa *BEST* unaratibiwa na Ofisi ya Rais-Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na unafadhiliwa na Benki Kuu ya Dunia. Idara ya

Mipango Miji na Vijiji inahusika katika utekelezaji wa mradi huo katika masuala yote yanayohusu sekta ya ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kazi zifuatazo zinakusudiwa kuendelea kutekelezwa :-
Awamu ya mwanzo ya mradi huu inajumuisha utayarishaji wa taarifa *(studies)* na Washauri Waelekezi zitakazowezesha kuandaa mambo yafuatayo:

a. Kuandaa muundo wa Sera ya Ardhi *(National Land Policy Framework).*

b. Kutayarisha mpango kazi wa kusajili ardhi *(Design of Land Registration Activities).*

c. Sera na taratibu za usajili wa ardhi kimazingira na kijamii *(Policy framework for Land Registration).*

d. Kuandaa taarifa za awali za kijamii na kiuchumi zinazohusu maeneo ya ardhi *(Socio-economic Baseline Data).*

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango Miji na Vijiji iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 106,800,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 66,000,000 kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara hii mpya ya Upimaji na Ramani inakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kushirikiana na Idara ya Mipango Miji na Vijiji katika kutayarisha mpango mzuri utakaopelekea kupima viwanja vya makaazi, huduma, vitega uchumi nk.

ii. Kuendelea na kazi ya Upimaji wa mipaka ya Wilaya na Mikoa.

iii. Kuendelea kuzifanyia mapitio ramani *(maps)* mpya za Zanzibar

iv. Kuendelea na utayarishaji wa ramani za kawaida kwa ajili ya utoaji wa hati mbali mbali za ardhi pamoja na uwekaji kumbukumbu *(Cadastral maps, Site plans etc.)*

v. Kuendelea na utunzaji wa kumbukumbu za ramani na taarifa mbalimbali za ardhi kupitia kitengo cha *ZALIS*

vi. Kuendelea na ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za kupwa na kujaa kwa maji ya Bahari kupitia kituo chetu kilichopo katika bandari ya Malindi Zanzibar .

Mradi Endelevu wa Usimamizi wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira *(SMOLE).*

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mradi wa *SMOLE*, utatekelezwa na Idara tano; Idara ya Upimaji na Ramani, Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Mipango Miji na Vijiji. (Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati) Idara ya Mazingira (Wizara ya Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais) na Idara ya Misitu (Wizara ya Kilimo na Maliasili). Mradi wa *SMOLE* kwa sasa unaratibiwa na Idara ya Upimaji na Ramani badala ya ile iliyokuwa Idara ya Upimaji na Mipango Miji.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mradi huu unakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. Kuendeleza uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za ardhi *(Land Information)* na Kumbukumbu za milki za ardhi kwa madhumuni ya usajili wa ardhi *(Land Registration)* na uhifadhi wa kumbukumbu za Mazingira *(Enviromental Information)* za Unguja na Pemba.

b. Kusaidia katika ununuzi wa vifaa vya ofisi vya Idara hizi kama vile kompyuta, magari ya kufanyia kazi, vifaa vya upimaji ardhi na vifaa vya uchunguzi wa mambo ya mazingira.

c. Kutoa elimu kwa jamii katika matumizi ya ardhi na uhifadhi wa mazingira kwa kuandaa semina na kutumia vyombo vya habari – TV, Radio na Magazeti.

d. Kuendeleza tafiti mbali mbali za usimamizi wa ardhi na uhifadhi wa mazingira katika visiwa vya Unguja na Pemba ambazo matokeo yake yatatumika katika kuandaa Sera mpya ya ardhi nchini itakayosaidia usimamizi na matumizi bora ya ardhi.

e. Kuwapatia Wafanyakazi wa Idara mafunzo ya ndani katika kazi za utayarishaji ramani, utumiaji wa vifaa mbali mbali vya kisasa vinavyotumika katika kazi za upimaji wa ardhi.

f. Kuendeleza uanzishwaji wa Afisi ya Msajili wa Ardhi Pemba pamoja na kuendeleza zoezi la kumtambuwa mwenye haki ya matumizi ya ardhi Unguja na Pemba (*land adjudication*).

g. Kusaidia kuandaa mpango na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu (nchini Tanzania) wafanyakazi wa Idara hizi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Upimaji na Ramani iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 295,100,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 170,000,000 kwa kazi za maendeleo

IDARA YA UJENZI

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Idara hii imetekeleza mambo yafuatayo:-

Bodi ya kusajili Wasanifu,Wahandisi Na Wakadiriaji Majengo

Mhe. Spika, Bodi hii inaendelea na kazi zake za kusajili na kuratibu shughuli za wataalamu wa ujenzi yaani Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo. Aidha Bodi tayari imeshatengeneza kanuni za kuendesha kazi zake za kila siku.

Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Bodi tayari imefanya usajili wa Wataalamu kama ifuatavyo:-

i.	Wasanifu Majengo	-	12
ii.	Wahandisi	-	34
iii.	Wakadiriaji Majengo	-	6
iv.	*Civil Engeneering Technician (FTC/NTA 4)*	-	6

Mhe. Spika, Bodi ya Kusajili Wakandarasi baada ya kupata Kanuni za kuendesha kazi zake inatarajiwa kuanza kufanya usajili wa Wakandarasi hivi karibuni baada ya kufanya semina ya utambulisho kwa wadau husika.
Aidha, Bodi imeshafanya matayarisho yote muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Nyumba za Maendeleo

Mhe. Spika, azma ya Wizara ilikuwa kulikabidhi jengo la Mpapa katika mwaka wa fedha 2010/2011. Pamoja na kujenga maegesho *parking* katika nyumba za Maendeleo Michenzani, Bloki nam.1,5,6 na 9, kutokana na ufinyu wa bajeti ilishindikana kufikia lengo hilo, kutokana na hali hiyo Idara ilitekeleza yafuatayo katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011:-

i. Ilijenga *partition* za vyoo na majiko kwa nyumba zote (Fleti 24).

ii. Ilijenga *parapet wall.*
iii. Iliweka fremu zote za milango na madirisha.
iv. kujenga njia ya umeme.

Mhe. Spika, kwa sasa idara imo mbioni kuanza kuweka plasta kwa jengo lote sambamba na uwekaji wa *fitting* za maji safi na maji machafu pamoja na kuweka *Conduit pipe* kwa ajili ya umeme.

MALENGO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 idara inakusudia kutekeleza mambo yafuatayo;-

i. Kushirikiana na Bodi katika kuendelea kuwashajihisha Wataalamu pamoja na Makandarasi wa ujenzi wanaofanya kazi zao hapa nchini kujisajili katika Bodi zetu mbili.

ii. Kushirikiana na Bodi kuona zinaanzisha uhusiano na Bodi nyengine katika nchi za Afrika ya Mashariki.

iii. Kumaliza kazi zote za *finishing* huko Mpapa katika fleti 24.

iv. Kushiriki kikamilifu katika maandalizi na utekelezaji wa ujenzi wa miji mipya *(New satellite Cities).*

Mhe. Spika, ili Idara ya Ujenzi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 464,600,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 100,000,000 kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Idara hii ilisimamia na kutekeleza kazi zifuatazo:

Matengenezo Nyumba za Serikali

Mhe. Spika, Idara imeendelea kufanya matengenezo katika maeneo mbali mbali zilizomo Nyumba za Serikali. Maeneo hayo ni pamoja na Michenzani, Kilimani, Mombasa na Kikwajuni kwa Unguja na Chake Chake, Mkoani na Wete kwa Pemba.

Matengenezo kwa sehemu kubwa yali husisha usafishaji wa *Septic Tank*, ubadilishaji wa baadhi ya bomba zilizoharibika na utengenezaji wa chemba.

Uundaji wa Kanuni kwa ajili ya Sheria ya *Condominium*

Mhe. Spika, Idara inakamilisha uundaji wa Kanuni zitakazowezesha Sheria ya *Condominium* kufanya kazi. Sheria hii itakapoanza kutumika, itawezesha wakaazi wanaoishi katika jengo moja lenye fleti zaidi ya moja kujua haki za matumizi ya jengo na uwajibikaji katika kuchangia gharama za matengenezo kwa sehemu za jengo zinazotumiwa na wakaazi wote *(Common Area).*

Uuzaji wa Nyumba za Vijiji

Mhe. Spika, Idara iliendelea na uuzaji wa nyumba za Vijiji kwa Unguja na Pemba, katika uuzaji huo Idara inazingatia kumpa nafasi kubwa mpangaji halali kuuziwa nyumba hiyo. Kinachohitajika ni muombaji kufuata taratibu zilizowekwa katika kuwasilisha maombi yake.

Maombi huanzia katika Kamati ya Shehia nyumba ilipo, Serikali ya Wilaya na baadae Serikali ya Mkoa na mwisho maombi hurejeshwa Wizarani.
Kamati ya Kuwatambua wale wote waliopewa nyumba na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Mhe. Spika, Kamati inaendelea na shughuli zake za kupokea madai na kuwasikiliza wahusika wote wenye madai ya kupewa nyumba na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Kamati imetoa muda zaidi ili kuhakikisha kila mwenye madai yake anapata fursa ya kuyawasilisha. Kamati inatarajia kukamilisha na kukabidhi ripoti hiyo mwishoni mwa mwezi wa Julai 2011.

Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba

Mhe. Spika, Bodi imeendelea kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri mbali mbali yaliowasilishwa. Jumla ya mashauri 27 yamewasilishwa kuanzia mwezi wa Julai 2010 kati ya hayo mashauri 12 yametolewa uamuzi na mengine yanaendelea.

MALENGO

Idara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuzifanyia matengenezo Nyumba za Serikali Unguja na Pemba.

ii. Kuangalia uwezekano wa kuongeza kodi za Nyumba za Serikali ili iendane na wakati.

iii. Kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Kodi za Nyumba za Serikali.

iv. Kuendelea kushajihisha wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba mpya za Makaazi ya kisasa.

v. Kuwapatia nafasi za masomo wafanyakazi wa Idara.

vi. Kuifanyia marekebisho Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba na kuendelea kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yanayowasilishwa kwa uadilifdu na uwajibikaji.

vii. Kukamilisha uundaji wa Kanuni za Sheria ya *Condominium*.

viii. Kuendelea na uuzaji wa nyumba za vijiji Unguja na Pemba.

ix. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba kwa kuwashajihisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta hiyo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Unguja maeneo yaliopendekezwa kwa mradi huu ni Binguni, Kibuteni, Fumba (maeneo huru) na Chuini na kwa upande wa Pemba ni eneo la *EPZ* – Maziwa Ng'ombe.

Miongoni mwa wawekezaji ambao wapo tayari na mazungumzo yameanza ni *UN-HABITAT* na Kampuni ya Dubai ijulikanayo kwa jina la *TECHNO GROUP*.

Mhe. Spika, ili Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 180,663,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi, 2011 Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe imetekeleza kazi zifuatavyo:-

Ufumbuzi wa tatizo la Msongamano wa Magari "Traffic "

Mamlaka ya Mji Mkongwe ilishirikiana na Taasisi mbali mbali za serikali kujadili kwa kina juu ya athari kubwa zinazosababishwa na ongezeko la vyombo vya moto katika eneo la Mji Mkongwe. Mjadiliano hayo yalipelekea kufanywa kwa mpango mzima wa "*Trafic plan*" ndani ya Mji Mkongwe. Zaidi, Mamlaka tayari imeshachukua hatua ya mwanzo ya utekelezaji wa mpango huo kwa kuweka mabango mawili ya kuzuia magari yenye uzito unaozidi tani mbili kuingia ndani ya eneo la Mji Mkongwe.

Mradi wa Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Baharini

Mhe. Mwenyekiti, Maandalizi ya ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari eneo la Mizingani umo katika hatua za mwisho na unatarajiwa kuanza wakati wowote mwaka 2011. Mradi huu unakisiwa kugharimu jumla ya Dola za Kimarekani Milioni Nane na Laki Tano (8.5 M USD) na unafadhiliwa na Benki ya Dunia.

Utayarishaji wa Vitabu vya Sheria na Mapitio ya Kanuni za Uhifadhi

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe imeifanyia marekebisho Sheria Nambari 3 ya mwaka 1994 ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi mwezi Juni 2010, na kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na hivi sasa Sheria hiyo inasubiri tamko la Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kutangaza siku ya kuanza kutumika kwa mujibu wa sheria hiyo na shughuli hizo zinakaribia kumalizika na punde si punde itatangazwa.

Uhifadhi wa Takwimu na Taarifa Muhimu

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mashirikiano na Chuo Kikuu cha Minesota Marekani, Mji Mkongwe imefanikiwa kupima maeneo ya wazi na kuweka katika kumbukumbu '*Data base'* maeneo mawili kati ya hayo yameshafayiwa makisio kwa madhumuni ya kuimarishwa ambapo Mamlaka imo mbioni kupeleka makisio hayo katika afisi za ubalozi wa Marekani ili kupata ufadhili.

Ukaguzi kwa Miji ya Urithi

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia kikao cha kamati ya urithi wa Dunia kilichofanyika Mwezi wa juni 2010 nchini Brazil, iliamuliwa kufanywa kwa ukaguzi yakinifu (*reactive monitoring*) kuangalia hali ya uhifadhi inavyoendelea. Mnamo mwishoni mwa mwezi wa Januari 2011 "*UNESCO World Heritage Center*" ilileta mtaalamu kuja kufanya kazi hiyo ambapo ripoti ya ukaguzi wake

itajadiliwa mwezi wa Juni huko Paris Ufaransa katika kikao cha UNESCO cha 35, taarifa imeshakaguliwa na imeshajadiliwa.

Kutoa Ushauri Wa Kitaalamu

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka inaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia miradi ya uhifadhi wa majengo, kwa vile Mamlaka imejijengea sifa katika kutengeneza majengo ya kale, kupitia UNESCO tumepata fursa ya kupeleka wataalamu Comoro kwa ajili ya kukagua jengo maarufu lililokuwa Kasri la Kifalme "*Ujumbe Palace*" na kufanya makisio ambayo yatapelekwa UNESCO kwa hatua za kuufadhili mradi huo ambao unategemewa kuwa chini ya usimamizizi wa Mamlaka.

Mkutano wa Mwaka na Mashirikiano kwa Miji ya Urithi kwa Kanda ya Afrika Mashariki

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ilitayarisha mkutano wa wadau mbali mbali wa Mji Mkongwe kujadili jinsi gani tunaweza kuimarisha mashirikiano ya miji ya kihistoria, ambapo wadau walishauri tutengeneze Tovuti au TV au mtambo wa TV ili kurahisisha mawasiliano baina ya wanachama wa kamati ya Sekreteriet ya Miji ya Urithi katika kanda ya Afrika Mashariki.

Kudhibiti Ujenzi Katika Eneo la Mji Mkongwe

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka katika kuulinda na kuuhifadhi Mji Mkongwe ili ubaki katika hadhi yake ya urithi imekua ikitoa vibali kwa kufanya matengenezo makubwa na madogo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaoenda kinyume na taratibu zilizoekwa. Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia kiambatanisho "F".

Maadhimisho ya Siku za Urithi wa Kimataifa

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka inaendelea kuadhimisha siku hizi za urithi wa kimataifa na kwa mwaka huu Mamalaka kwa kushirikiana na Jumuiya ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe, ilifanikiwa kuadhimisha siku ya mshikamano wa miji ya urithi wa Dunia, kwa kusafisha ufukwe wa bahari kuanzia hoteli ya *Mercury* hadi hoteli ya Tembo na kufanya kongamano kwa maafisa wa polisi, juu ya mpango wa matumizi ya Barabara za Mji Mkongwe "*Traffic Planning*".

Utoaji wa Elimu kwa Jamii

Mhe. Mwenyekiti, katika utoaji wa elimu kwa jamii Mamlaka ilifanikiwa kuwaalika wanafunzi wa skuli sita na kuwapatia mafunzo yanayohusu historia

ya Mji mkongwe na thamani yake katika urithi wa dunia na baadae kuwashirikisha katika mashindano ya kutoa maelezo kwa picha kuelezea umuhimu na changamoto zinazoukabili Mji Mkongwe wa Zanzibar ikiwa ni mji wa urithi.

Uendelezaji wa Eneo la Mambo Msiige

Mhe. Mwenyekiti, uendelezaji wa eneo la Mambo Msiige unaojumuisha Jengo na eneo la wazi, uko katika hatua za ramani. Tayari Wizara imesha wasiliana na *UNESCO* na kukubaliana juu ya umuhimu wa mradi huo. Hatua inayoendelea ni kwa pande mbili hizi kupitia na kukubaliana na ramani hizo ili zikidhi haja ya uendelezaji huo na matakwa ya urithi wa kimataifa.

MALENGO

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuandaa mpango wa kuitangaza Sheria ya Mamlaka kwa wadau na wananchi kwa ujumla.

ii. Kuendeleza kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia miradi ya uhifadhi wa majengo.

iii. Kuandaa maadhimisho ya siku mashuhuri za kimataifa kama vile siku ya urithi Duniani na siku ya mshikamano kwa miji ya urithi wa kimataifa.

iv. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo na kutoa elimu ya umma kuhusu uhifadhi wa Mji Mkongwe kwa kushirikiana na wadau mbali mbali

v. Kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa ukuta wa Ukingo wa bahari ya Forodhani.

vi. Kuusimamia utaratibu wa kupunguza msongamano wa vyombo mbali mbali ndani ya Mji Mkongwe (*Traffic Plan*).

vii. Kusimamia na kutunza mandhari ya Mji Mkongwe ikiwa ni pamoja na uondoshaji wa biashara holela katika maeneo yasiyostahiki.

viii. Kuwa na mpango maalum wa kuzielimisha Taasisisi za serikali, za watu binafsi na wadau mbali mbali kupitia matamasha makubwa yanayofanyika hapa kwa uwekaji wa "Government sign board, Private sign board and Posters".

ix. Kusimamia uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya wazi kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya jamii ndani ya Mji Mkongwe, hii itasaidia uimarishaji wa kumbukumbu "Data base" za Mamlaka.

x. Kuendeleza mashirikiano na vyuo pamoja na taasisi za nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 208,801,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

MAMLAKA YA MAJI

Ukusanyaji wa mapato

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2011, Mamlaka imekusanya jumla ya Shs 655 milioni kati ya bilioni 2,151 ambazo ni sawa na asilimia 30.45 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya kuwapa Wananchi taaluma ya kutosha kuhusu kuchangia gharama za huduma ya maji, bado muamko ni mdogo. Baadhi ya Washirika wa Maendeleo wamesitisha azma yao ya kuendelea kutusaidia kutatua matatizo ya maji, hasa ya Mjini na Magharibi hadi hapo Wananchi watakapo changia angalau kwa kiwango cha asilimia 60 kilchowahi kufikiwa hapo awali. Tuanomba msaada wenu Waheshimiwa wa kurudisha ari ya Wananchi ya kuchangia huduma hii ya maji pale maji yatakapopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara yangu ilijipangia kutekeleza miradi ifuatayo:-

i. Usambazaji wa Maji Vijijini;
ii. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini;
iii. Kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji;
iv. Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira.

Usambazaji wa Maji Vijijini

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unalenga zaidi katika vijiji ambavyo huduma ya maji bado haipatikani vizuri. Aidha mradi hugawiwa katika miradi midogo midogo kwa mujibu wa maeneo yaliyokaribiana.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imetekeleza miradi mbali mbali kama inavyoonekana katika Kiambatanisho "G".

Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara yangu kupitia mradi huu ilitekeleza miradi kama vile mradi wa maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi, uliogharimu Tsh Bilioni 32 ambao umekamilisha ujenzi wa awamu ya pili kwa ufadhili wa serikali ya Japani kwa thamani ya Tsh Bilioni 20. Mradi huo umejenga matangi makubwa mawili (yenye ujazo wa lita 1, 200,000 na 2, 700,000), wamejenga visima vitano (5) na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 21 kwa sasa umekamilika. Kazi inayoendelea sasa ni majaribio ya mradi kwa kuyapeleka maji kwa wananchi, katika maeneo mbalimbali ya mji.

Mhe. Mwenyekiti, Hata hivyo, kutokana na uchakavu wa mabomba, mafanikio ya mradi huo hayajaonekana sana kwa baadhi ya maeneo, kwa sababu maji mengi yanapotea ardhini kabla ya kuwafikia watumiaji. Pamoja na kuendelea na majaribio, hivi sasa Mamlaka inaendelea na kazi za kubadilisha mabomba yaliyochakaa na kuweka mapya, kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa mradi huo.

Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu ulitekeleza majukumu yake kwa kuwapatia wafanyakazi mafunzo mbali mbali ya ndani na nje ya nchi, kutoa misaada ya vitendea kazi kama vile gari, pikipiki na ufungaji wa mita za maji, ujenzi wa vioski vya majaribio Shehia ya Makadara, pamoja na Kusajili kwenye "*computer*" mita za wateja zilizofungwa.

Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira

Mhe. Mwenyekiti, katika jitahada za kuwapatia wananchi maji safi na salama, tumeanzisha mradi wa usambazaji maji na Usafi wa Mazingira unaotekelezwa kwa pamoja baina ya *AfDB, UN HABITAT* na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika miji mitatu ya Pemba ambayo ni Chake Chake, Wete na Mkoani. Aidha, mradi huu unahusisha pia Vijiji 9 ambavyo ni Nungwi,

Matemwe, Machui na Dunga Tunguu, kwa Unguja na Ndagoni, Wambaa, Mizingani, Vitongoji na Kambini kwa Pemba.

Kazi zilizofanyika ni za usanifu wa Mradi na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza mwaka 2012 ambazo zitahusisha pia usambazaji wa maji na ujenzi wa vyoo maskulini na kukuza maendeleo ya Rasilimali Maji.

KAZI ZA KAWAIDA

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/ 2011 Wizara yangu kupitia Mamlaka ilitekeleza kazi za kawaida kama inavyoonekana katika kiambatanisho "H".

MALENGO

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kupitia Mamlaka ya Maji imepanga kutekeleza kazi zifuatayo:-

i. Usambazaji wa Maji Vijijini
ii. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
iii. Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (*phase* II)
iv. Usambazaji wa maji na Usafi wa Mazingira
v. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (*ADF12*)
vi. Kuvilinda na kuviwekea uzio vianzio vya maji.

Usambazaji wa Maji Vijijini

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa China imekubali kuchangia jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 1.5 kwa kazi za uchimbaji wa visima zaidi ya 30 pamoja na ujenzi wa matangi, utiaji pampu, na ulazaji wa mabomba ya inchi 6 na 4 katika maeneo 24 ya Unguja na Pemba. Kwa maelezo zaidi angalia kiambatanisho "I".

Mradi wa Maji Safi na Mazingira

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mradi huu unatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. Usambazaji wa maji katika vijiji 4 vya Unguja ambavyo ni Nungwi, Matemwe, Dunga/Tungu na Machui na Pemba vijiji 5 vya Vitongoji, Kambini-Mchangamdogo, Ndagoni, Wambaa na Mizingani.

b. Usambazaji wa maji na ujenzi wa vyoo maskulini Unguja na Pemba

c. Kukuza maendeleo ya Rasilimali Maji Zanzibar

d. Kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji

Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2011/2012 inatarajia kuendeleza kutanua huduma ya maji kwa kuchimba visima 9 Mkoa wa Mjini Magharibi, ununuzi wa pampu na ulazaji wa mabomba katika maeneo mapya na kuimarisha mitandao katika maeneo ambayo huduma ya maji hazifiki vizuri.

Mradi wa Kuijengea uwezo mamlaka ya maji (Awamu ya Pili)

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji itatekeleza mradi huu kwa kufunga mita za maji kwa watumiaji ili waweze kulipa kutokana na kiwango halisi cha matumizi ya maji kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato pamoja na kupunguza kiwango cha upotevu wa maji na hatimae kuwa na huduma bora na endelevu za maji safi na salama.

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (ADF12)

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu uko katika hatua za awali za kutengewa fedha zinazofikia dola za Kimarekani Milioni 21, kwa ajili ya kubadilisha mabomba makongwe na kuweka mapya katika Mkoa wa Mjini Magharibi, aidha timu ya wataalamu kutoka *ADB* itakuja kuainisha maeneo yaliyopangwa kutekelezwa mradi huo **(***Project Identification* Mission)**,** kufanya tathmini ya mradi na hatimae kukubaliwa rasmi na kusaini mkataba wa utekelezaji **(***Project apprisal and signing of the loan agreement***).**

SHIRIKA LA UMEME

UTEKELEZAJI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TShs. 47,898,381,000.00. Kati ya fedha hizo, Shirika limekusanya T.Shs. 24,149,483,454.00 sawa na asilimia 51.06 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, katika makadirio ya mwaka wa fedha 2010/2011, Shirika la Umeme lilikadiria kutumia TSh. 41,684,015,241.00 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

Hadi kufikia Machi 2011 matumizi halisi ya Shirika yalikuwa TSh. 24,688,305,373.98. Kati ya fedha hizo. TSh. 13,712,747,912.00 zilitumika kwa ununuzi wa Umeme Tanesco. TSh.971, 720,927 zilitumika kwa ununuzi wa mafuta ya kuzalisha Umeme katika kisiwa cha Unguja na TSh. 10,003,836,534.98 kwa uendeshaji wa kazi za kawaida na za maendeleo.

Mradi wa ujenzi wa njia ya Pili ya Umeme Unguja

Mhe. Mwenyekiti, kazi za utengenezaji wa waya mpya wa baharini (*submarine cable*) imeshaanza kiwandani Japan na inategemewa kumalizika mwezi Julai, 2012 na ulazaji wa waya huo baharini inatarajiwa kukamilika Oktoba 2012.

Aidha, Kazi ya ujenzi wa vituo vya kupokelea umeme inategemewa kuanza rasmi mnamo mwezi wa Julai, 2011na inatarajiwa kumalizika mwezi Mei 2012.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya Tsh 5,301,000,000 zimetumika kuwalipa fidia wananchi 843 walioatihirika kwa namna mmoja au nyingene kutokana na mradi huu. Kati ya fedha hizo Tsh 3,201,000,000 zimelipwa na Serikali ya Marekani na Tsh 2,100,000,000 zimelipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mradi wa Ufungaji wa Mita 10,000 za Tukuza

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa kazi hii unaendelea vizuri, kwa sababu Shirika limeweza kuvuka lengo kwa kuzifunga mita 12,000, sawa na ongezeko la asilimia 20. Aidha, Shirika limefunguwa kituo kipya cha kuuzia umeme wa Tukuza pamoja na mita za kawaida huko Mkokotoni kwa ajili ya kuwahudumia Wanachi wa Tumbatu ambao wamefungiwa mita za TUKUZA.

Uimarishaji wa Miundombinu ya Kusambaza Umeme

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Japan zilitiana saini mkataba wa msaada wa fedha wenye jumla ya Yen za Japani Bilioni 3 sawa na Tsh Bilioni 55. Msaada huwo ni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vipya vya umeme pamoja na njia kuu za kusambazia umeme katika kisiwa cha Unguja.

Vile vile Shirika kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji tumekubaliana kuimarisha kituo kikuu cha umeme (*Substation*) kiliopo Mpendae kwa Mchina kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme katika maeneo ya Mpendae, Mombasa, Migombani, Kiembe samaki, Mazizini, Mbweni na Chukwani.

Kuendeleza mpango wa upatikanaji wa Nishati Mbadala

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme limeweza kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo ya kufanya mazungumzo na Taasisi tofauti, ambazo zimeonesha nia ya kutaka kuwekeza katika uzalishaji umeme kwa kutumia njia zifuatazo:-

i. Nishati ya upepo
ii. Nishati ya jua na
iii. Nishati ya gesi asilia

Aidha, Wizara pamoja na Shirika tunaendelea na jitihada ya kuifuatilia Kampuni ya *SDE* ya Israel ambayo imeonesha nia ya kutaka kuwekeza katika uzalishaji wa umeme kwa njia ya mawimbi ya Baharini.

MALENGO

Kazi za maendeleo

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imepanga kuendeleza na kutekeleza miradi ya maendeleo ifuatayo:-

i. Mradi wa Ujenzi wa njia ya pili ya umeme - Unguja
ii. Mradi wa Uimarishaji wa Njia za kusambazia Umeme Unguja
iii. Mradi wa usambazaji umeme Vijijini.
iv. Mradi wa ufungaji Mita 10,00 za Tukuza
v. Kuendeleza Mpango wa Upatikanaji wa Nishati mbadala.

Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Pili ya Umeme – Unguja

Mhe. Mwenyekiti, lengo la mradi huu ni kuongeza uwezo wa kiwango cha matumizi kufikia Megawati 100 katika kisiwa hiki cha Unguja.

Wizara itahakikisha kuwa Shirika la Umeme (*ZECO*) na Shirika la Nuguvu za Umeme (*TANESCO*) wanatekeleza wajibu wao hatua kwa hatua na kuhakikisha deni la *TANESCO* lisio la lazima na utata wa deni hilo unaondoka. *(Makofi)*

Mradi wa Uimarishaji Njia za Kusambaza Umeme Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa uimarishaji wa njia za usambazaji umeme na ujenzi wa vituo vya umeme unaofadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la *JICA*, unatarajiwa kuanza katika mwaka ujao wa fedha, yaani mwaka huu.

Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha kwa kuziongezea uwezo njia za usambazaji umeme zinazokwenda kusini, kaskazini na Fumba pamoja na ujenzi wa vituo vipya vya umeme katika maeneo ya Mtoni, Mwanyanya na Welezo. Aidha, mradi huu pia utahusisha na ununuzi wa spea na vifaa mbali mbali vya umeme.

Mradi wa Usambazaji Umeme – Vijijini

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Umeme itahakikisha kuwa inakamilisha kusambaza umeme katika vijiji vilivyosalia, kutokana na kumalizika kwa Awamu ya Nne ya mradi huo uliofadhiliwa na Serikali ya Norway. *(Makofi)*

Mradi wa Ufungaji Mita 10,000 za TUKUZA

Mhe. Mwenyekiti, shirika litaendeleza mradi huu wa ufungaji wa mita za TUKUZA, ambapo katika mwaka ujao wa fedha jumla ya mita 10,000 zinatarajiwa kufungwa katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu. Kazi hii ya ufungaji wa mita za TUKUZA itaenda sambamba na kazi ya kuongeza vituo vya kuuzia umeme, ili kuwasogezea huduma kwa karibu zaidi wananchi.

Kuendeleza Mpango wa Upatikanaji wa Nishati Mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo juu ushiriki wa wizara yangu katika kusimamia miradi ya maendeleo mbali mbali. Lengo hili ni muhimu sana kwa kuendeleza mpango wa upatikanaji wa vyanzo mbadala vya kuzalisha Umeme Unguja na Pemba.

Mapato na Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, shirika linakadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 57.7/=. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 53.2/= zitatokana na mauzo ya umeme na shilingi bilioni 4.5/=, zinatarajiwa kukusanywa kutokana na mapato mengineyo. Aidha matumizi ya shirika yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 56.9/=, kwa kazi za uendeshaji na maendeleo. Shirika linategemea kupata faida ya uendesaji ya shilingi milioni 790/=.

IDARA YA NISHATI NA MADINI

UTEKELEZAJI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Idara ya Nishati na Madini ilisimamia na kutekeleza mambo yafuatayo:-

Kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Zanzibar
Mhe. Mwenyekiti, Sera ya Nishati ya Zanzibar ilikamilika na kupitishwa rasmi na Baraza la Mapinduzi Disemba 2009. Baadaye Sera hiyo ililetwa katika Baraza lako Tukufu Januari 2010 kwa kupata baraka za Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia limepewa kipaumbele. Bado msisitizo umewekwa katika kuihuisha Nishati hii kuwa ni muhimili mkubwa wa Uchumi wetu. Kwa kuwa Uchumi sio suala la Muungano, ushughulikiaji wa Rasilimali ya Nishati hii haupaswi kuwa suala la Muungano. Dhamira ya kulitoa katika Orodha ya Muungano iko pale pale. *(Makofi)*

Aidha, Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Nishati "*Implementation Plan of Energy Policy*" umeshaandaliwa na kupelekwa katika Ubalozi wa Sweden kwa kuomba ufadhili katika kipindi cha awamu ya pili ya mradi wa Sera ya Nishati ambacho kiko katika matayarisho.

Kuendeleza Jitihada zaidi za Kuwafikishia Eimu ya Umeme wa Jua Wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba

Mhe. Mwenyekiti, juhudi za kuwafikishia huduma za nishati mbadala kama vile nishati ya Umeme wa jua kwa visiwa vidogo vidogo vya Unguja na Pemba inaendelea. Mpango wa kutoa elimu juu ya matumizi bora ya umeme wa jua unaendelezwa kwa ushirikiano wa Jumuia inayojishughulisha na Umeme wa jua ya hapa Zanzibar (*ZASEA*) chini ya ufadhili wa Jumuia ya Ushirikiano kati ya Ujerumani na Tanzania (*DTP*).

Hivi sasa wananchi wengi pamoja na Mahoteli tayari wamehamasika na wanaendelea kutumia nishati ya jua. Aidha hivi sasa kwa kushirikiana na *ZASEA* tumeanzisha mpango wa kutoa elimu ya umeme wa jua mashuleni unaojulikana kama (*Solar Programe in School*). Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho "J".

Kushiriki Kikamilifu katika Masuala yote ya Nishati ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, ushiriki wetu katika Kamati za Nishati za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki unaendelea vizuri. Kwa mujibu wa kalenda ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki, Mkutano Mkuu wa Mafuta wa Jumuia hiyo (*East African Petroleum Conference)* hufanyika kila baada ya miaka miwili tangu ulipoanzishwa mwaka 2003. Mkutano wa tano umefanyika Uganda tarehe 2 mpaka 4 Februari 2011 na kuwashirikisha Viongozi wa ngazi ya juu wa wizara yetu na pia kutoka *ZIPA*.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la Mikutano hii ni kuweka juhudi za pamoja miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki katika masuala ya utafutaji wa mafuta kwenye ukanda huu. Pamoja na lengo hilo Zanzibar inafaidika na mikutano hii kwa kuwaongezea maarifa na taaluma za utafutaji na uchimbaji wa mafuta wafanyakazi wa Sekta ya Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta nyengine kama vile za Mazingira, Utalii na Uwekezaji za nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki nazo pia hufaidika na mikutano hii ya mafuta kwani mikutano hii huwajumuisha pamoja wataalamu na viongozi wa Sekta hizo katika eneo la Afrika Mashariki.

Kwa upande wa Nishati ya Umeme, Jumuia ya Afrika ya Mashariki imeandaa kikundi kazi kinachojulikana kwa jina la "*East African Power Master Plan*" ambacho Idara yetu pamoja na Shirika la Umeme (*ZECO*) ni mjumbe wa kikundi kazi hicho. Kwa ujumla Sekta za Nishati ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki zinatoa taarifa zao za utekelezaji kwa Sekta za Nishati za hapa Zanzibar.

Kuendelea Kusimamia Uagizaji wa Mafuta Zanzibar (Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa).

Mhe. Mwenyekiti, uagizaji na uingizaji wa nishati ya mafuta hapa nchini unaendelea vizuri. Changamoto zilizojitokeza katika siku za karibuni ni kwa baadhi ya makampuni kutotowa huduma ipasavyo kwa kisingizio cha kutaka kupandisha bei ya bidhaa hiyo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tumekuwa tukilipatia ufumbuzi suala hili kwa kuzingatia maslahi ya wananchi wa Zanzíbar.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nishati inaendelea kufuatilia takwimu za mafuta ya *petrol* yanayoingia katika "*Depot*" za Mtoni kila wiki, ili kuhakikisha nishati hiyo ipo ya kutosha hapa nchini. Hata hivyo, wizara yangu inaishauri Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuweka chombo cha

kupimia mafuta "*Flow Meter"* kutoka kwenye meli kuja kwenye matangi ili ipatikane takwimu bora na sahihi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu ya bidhaa hiyo ni kama inavyoonekana katika kiambatisho "K"

Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika Kuandaa Programu ya Mafunzo ambayo Itasaidia Idara ya Nishati na Madini pamoja na Wizara kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi Makaazi Maji na Nishati inaendelea kufanya juhudi ya kuwapatia Mafunzo wafanyakazi wa Idara hii na Wizara kwa jumla, ili kuweza kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa fani ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la *PETRAD* imewapatia mafunzo wafanyakazi wawili (2) katika kipindi cha mwaka 2010 /2011 katika nyanja ya "*Petroleum Policy and Management"* na *"Petroleum Development and Operations*" nchini Norway. Hivyo kufanya idadi ya wanafunzi hao kufikia kumi (10) kuanzia mwaka 2002 hadi 2011.

Vile vile semina na warsha kadhaa katika fani ya Mafuta na Gesi Asilia zimefanywa hapa Zanzibar kwa washirika mbali mbali kwa lengo la kutoa ufahamu zaidi katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi wa Idara hii "*Training Needs Assessment*" umeshaanda chini ya ufadhili wa Norway.

Aidha, Kampuni ya *Ras El Khaimah Tanzania Ltd*. ya *UAE* imekubali kugharamia mafunzo kwa Wazanzibari wenye sifa ya kujiunga na Masomo ya juu yanayohusu "*Petroleum Engineering na Petroleum Geo- Science*". *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tayari mfanyakazi mmoja anaendelea na masomo huko Dubai, juhudi za kupeleka wengine 9 zinaonekano kidogo kutofanikiwa kutokana na kukosekana kwa makubaliano rasmi ya mchango wa kila upande katika masomo yao. Kwa hivyo, bado majadiliano yanaendelea sambamba na mazungumzo na taasisi nyengine mbali mbali zenye nia ya kutusaidia katika suala hili.

Utekelezaji wa Sera ya Nishati utatuwezesha kutekeleza ahadi yetu ya kupeleka vijana wa Kizanzibari kusomea masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta. *(Makofi)*

MALENGO

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nishati na Madini katika mwaka wa fedha 2011/2012 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuandaa na Kusimamia mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Zanzibar.

ii. Kuendelea na juhudi za kuwapatia wananchi wa Zanzíbar elimu juu ya matumizi ya umeme wa jua.

iii. Kushiriki kikamilifu katika masuala yote ya nishati ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki.

iv. Kuendelea kusimamia upatikanaji wa mafuta Zanzibar (Dizeli, Petroli na Mafuta ya taa).

v. Kutunga Sheria ya usimamizi wa '*Depot'* za mafuta za Serikali na kuhakikisha kuwa *Depot* hizo zinachangia Idara ya Nishati.

vi. Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuandaa na kutekeleza programu ya mafunzo ambayo itasaidia Idara ya Nishati na Madini pamoja na Wizara kwa ujumla.

vii. Kushirikiana na Serikali ya Norway katika utekelezaji wa kazi ya tathmini ya mazingira ya Zanzibar (*Strategic Environmental Impact Assesment*) ambayo itatoa muelekeo wa nchi kwenye sekta ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

viii. Kusimamia shughuli, mipango na maandalizi ya utafiti na hatimae uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asali.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Nishati na Madini iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi milioni 122,928,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi bilioni 48/= kwa kazi za maendeleo.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuwatumikia wananchi wenzangu kupitia wizara hii, ambayo inawagusa wananchi wenyewe ama mmoja mmoja au kwa ujumla wao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wizara yangu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mashirika ya Kimataifa na Yasiyo ya Kimataifa, Sekta Binafsi, *NGO's*, *CBO's* na wananchi kwa jumla kwa mashirikiano mkubwa waliyoyaonyesha na wizara yangu kwa misaada yao ya hali na mali waliyoitoa na wanayoendelea kutoa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yangu.

Washiriki hao ni pamoja na JAPAN, NORWAY, SWEDEN, MAREKANI, CHINA, EGYPT, FINLAND, *UNICEF, UNESCO, UNDP, DFID, JICA, Sida, DED, UN HABITAT, AfDB, TASAF, ZATI, IFA*, ANGOZA, TUME YA UKIMWI ZANZIBAR, *NORAD, RED CROSS, ACRA*, BENKI YA DUNIA, UBELGIJI, *RAK GAS TANZANIA, EU, PETRAD, MCC* ya Marekani, pamoja na wale wote ambao kwa bahati mbaya hatukuweza kuwataja . Tumepata faraja kubwa sana kwa michango yao kwa maendeleo ya nchi yetu, tunaahidi kuienzi na kuiendeleza na kuithamini michango hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe, Mhe. Mwenyekiti, Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein, kwa imani yake kwangu na kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuitumikia nchi yangu. Aidha namshukuru Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kwa misaada na maelekezo yao kwangu wote ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na maisha marefu pamoja na familia zao. *(Makofi)*

Tunaomba pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilizotembelea na kufanya vikao na wizara yangu. Maoni, ushauri na maelekezo yao kwetu yamesaidia sana sio tu katika utekelezaji wa kazi bali pia katika uandikaji wa hotuba hii. Shukurani maalum kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa msaada wao mkubwa kwetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kumshukuru sana Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali pamoja na wafanyakazi wenzake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuwezesha vitabu vya Bajeti za Wizara zote kupatikana kwa wakati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, shukurani maalum ziwaendee wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara ya Ardhi Makaazi Maji na Nishati, kwa msaada wao mkubwa kwangu Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu bila ya msaada na mashirikiano yao bajeti hii isingeweza kuwasilishwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba pia uniruhusu kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Donge, kwa heshima kubwa waliyonipa kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao. Ninawashukuru sana na *Inshaallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu (S.W) tutafikia malengo tuliyoyakusuidia. Waendelee kunipa mashirikiano na kuniamini nami nitaendelea kuwatumikia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapokee, wayajadili kwa kina, watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Kwa hivyo, tunayo imani kubwa kuwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ili wizara yangu iweze kutekeleza kazi, majukumu na malengo niliyoyaeleza, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 5,026,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi bilioni 4,996,902,000/= kwa kazi za Maendeleo kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naliomba Baraza lako Tukufu likubali matumizi ya Wizara yangu jumla ya shilingi bilioni 10,022,902,000/= na pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya shilingi bilioni 2,198,343,000/= kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Kwa ufafanuzi zaidi ninaomba muangalie kiambatanisho L1 na L2.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Mwenyekiti, Hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii adhimu uliyonipa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia afya njema leo hii na kutuwezesha kukutana kwa ajili ya shughuli muhimu ya kujadili na kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Aidha nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili nianze kuichangia Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa mashirikiano makubwa alioipatia kamati yetu katika kipindi kifupi tu, tulipoanza kushika wadhifa huo. Kamati yetu imefurahishwa sana kutokana na milango ya ofisi yake kuwa wazi pale kamati inapotaka kukutana naye hasa kwa lengo la kuhakikisha kuwa serikali inafanya kazi kwa ukaribu zaidi na Kamati na kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapenda kwa dhati kutambua ushirikiano mkubwa iliopatiwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati chini ya uongozi wa Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na wasaidizi wake wote pamoja na watendaji wote wa wizara hii. Ushirikiano wao umeisaidia sana kamati katika kutekeleza kazi zake kwa ufanisi hasa wakati wa kazi ya kupitia bajeti ya wizara hiyo. Ni matarajio yetu kuwa wizara itaendelea kutupatia ushirkiano, ili kamati iweze kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Kanuni ya 94 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, ilipewa kazi ya kufikiria Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka 2011/2012. Kwa ushirikiano mkubwa wa wajumbe wenzangu wa kamati hii, kazi hiyo ilifanyika vizuri.

Hivyo, nichukue fursa hii tena kuwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kwa ushirikiano huo walionipa wakati wote wa utendaji wa kazi hiyo na kazi nyenginezo za Kamati. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati hiyo kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Shawana Bukheit Hassan - Mjumbe

4. Mhe. Subeti Khamis Faki - Mjumbe
5. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
6. Mhe. Salum Amour Mtondoo - Mjumbe
7. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
8. Ndg. Mussa Kombo Bakari - Katibu
9. Ndg Aziza Wazir Kheir - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya awali, sasa naomba uniruhusu nianze kutoa maoni ya Kamati kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012. Hotuba hii ya maoni ya kamati, itagusa tu baadhi ya maeneo ambayo kamati yetu imehisi kuwa hatuna budi kuyatolea maelezo. Maeneo hayo ni kama yafuatayo:-

UTAFITI KATIKA WIZARA

Mhe. Mwenyekiti, utafiti una nafasi kubwa katika maendeleo ya nchi kwa kufahamu kwa uhakika changamoto kadhaa zilizopo na jinsi ya kuzikabili changamoto hizo. Kwa mantiki hiyo, kamati yetu inaunga mkono uamuzi wa serikali wa kuingiza rasmi suala la utafiti katika Idara ya Mipango na Sera ya kila wizara ikiwemo Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuhakikisha wazo hilo la serikali linakuwa na maana, wizara haina budi kulichukulia suala la utafiti kwa uzito mkubwa kwa kuhakikisha kuwa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaimarishwa kwa kuwa na watendaji wenye uwezo wa kutekeleza jukumu hilo la kufanya utafiti, lakini pia kunakuwa na fedha zitakazowezesha tafiti hizo kufanyika. Ni matarajio ya Kamati hii kuwa baada ya muda mfupi tutashuhudia matunda makubwa ya idara hii katika kuleta maendeleo ya wizara na nchi kwa ujumla.

MIGOGORO YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeridhishwa na jitihada zinazochukuliwa na wizara kupitia idara zake zinazohusiana na ardhi na upimaji katika kuleta mageuzi ya kisera na kiutekelezaji katika sekta ya ardhi hapa Zanzibar. Hata hivyo, Kamati yetu inasikitishwa sana na suala la migogoro ya Ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara hivi sasa na kusababisha chuki na uadui miongoni mwa wananchi. Aidha migogoro hiyo kwa kiasi kikubwa,

imepelekea kuongezeka kwa kesi katika Mahakama ya Ardhi, jambo ambalo linaigharimu serikali fedha nyingi katika kuitatua.

Kamati inaamini kuwa migogoro mingi inaweza kuepukwa ikiwa watendaji wa sekta hii watazingatia sheria na utaalam wao wakati wa kutekeleza shughuli zao. Hivyo, Kamati inashauri uongozi wa wizara kuongeza juhudi za kuleta mageuzi zaidi katika sekta ya ardhi, ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima ambayo imekuwa ikiigharimu serikali na viongozi wake fedha nyingi katika kuitatua, pamoja na muda ambao ungeweza kutumika katika shughuli nyengine za kimaendeleo.

MRUNDIKANO WA KESI KATIKA MAHAKAMA YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa kesi zinazohusiana na ardhi, Mahakama ya Ardhi imekuwa taasisi muhimu sana katika kusimamia haki za wananchi wa Zanzibar. Ili kukabiliana na ongezeko hilo la kesi, Serikali kwa kutumia busara zake, ilifanya marekebisho ya sheria iliyoanzisha Mahakama ya Ardhi ili Mwenyekiti wa Mahakama hiyo apate wataalam wengine watakaoweza kuamua kesi za masuala ya ardhi. Kamati yetu inasikitika kuona hadi sasa ni Naibu Mwenyekiti pekee ndiye aliyeteuliwa lakini Mahakimu wa Mikoa wa Ardhi bado hawajateuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kutoteuliwa kwa wasaidizi hawa katika mikoa, kunapelekea kasi ya uamuzi wa kesi zinazowasilishwa katika mahakama hiyo kuwa ndogo sana na hivyo kuathiri haki za wananchi kwa kuwa upatikanaji huo wa haki huchelewa sana. Uteuzi wa mahakimu hawa ulipaswa kufanywa haraka sana ili kunusuru haki za watu. Ukifanya rejea ya takwimu zilizowasilishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wastani wa kesi zaidi ya kumi hufunguliwa kila mwezi hapa Unguja, lakini inaonyesha wastani wa chini ya kesi mbili hutatuliwa kwa kila mwezi, huku kesi zaidi zikiendelea kufunguliwa. Hiyo ni ishara mbaya ambayo hatuna budi kuifanyia kazi kabla wananchi hawajapoteza imani juu ya upatikanaji wa haki zao zinazohusiana na masuala ya ardhi.

Pamoja na kwamba katika hotuba hii suala la kushirikiana na Idara ya Mahakama katika kuwapata Mahakimu wa Mikoa limetajwa, Kamati yetu inaiomba sana Serikali kuharakisha uteuzi wa mahakimu hao ili kuongeza kasi ya utoaji wa maamuzi katika kesi za ardhi. Aidha, kutokana na uzito wa masuala ya ardhi hapa Zanzibar, Kamati inasisitiza kuteuliwa wanasheria

waadilifu na wenye uwezo mkubwa, watakaoumudu kutatua migogoro hiyo kwa haraka lakini kwa uadilifu mkubwa na kwa haki.

Mhe. Mwenyekiti, Kutokana na migogoro mingi ya Ardhi iliyopo hivi sasa, Kamati inaisisitiza Wizara ifanye juhudi za makusudi kuisaidia Mahakama ya Ardhi katika bajeti hii kuiwekea fungu maalum ambalo litaisaidia Mahakama kutekelza kwa ufanisi majukumu yake ya kila siku.

MAFUNZO KWA WATENDAJI

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo kwa watendaji wa idara mbali mbali wa wizara ni muhimu sana katika kuleta ufanisi katika kazi. Kamati yetu inaipongeza sana wizara kwa kuandaa program ya kusomesha watendaji wake kupitia taasisi mbali mbali za wizara. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kiasi ya watendaji 55 wanachukua kozi za muda mrefu ndani na nje ya nchi na watendaji 35 wamechukua kozi za muda mfupi. Hiyo ni hatua nzuri katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Mbali na jitihada hizo, Kamati imebaini kuwepo kwa wataalam wachache katika baadhi ya idara kulinganisha na ukubwa wa majukumu ya taasisi hizo, hasa katika Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Mipango Miji na Vijiji kwa uchache, kutokana na ugumu wa kupata wataalam wa fani hizo. Kamati inashauri wizara kuwasiliana na wizara ya Elimu kwa lengo la kuhakikisha vijana wanasomeshwa katika fani hizo ili kutatua tatizo la wataalam kwa baadhi ya fani.

MATENGENEZO KATIKA NYUMBA ZA MAENDELEO

Mhe. Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujenga nyumba za maendeleo kwa ajili ya kutatua tatizo la makaazi kwa wananchi hasa wa kipato cha chini, sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba ulikuwa wa busara sana na unafaa kupongezwa na kuenziwa. Nyumba hizo ambazo zimejengwa miaka mingi iliyopita, zimeanza kuchakaa na hivyo kuhitaji matengenezo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, jukumu kubwa la kuzifanyia matengenezo nyumba hizo limewekwa chini ya Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi. Kamati yetu inahisi kuwa Idara hii ambayo katika bajeti ya mwaka 2011/2012 imetengewa

wastani wa kiasi cha shilingi milioni mia moja na hamsini, haitoweza kutekeleza jukumu hili zito ambalo ni muhimu kwa ajili ya usalama wa wakaazi wa nyumba hizo ambao wengi wao hawamudu kuzifanyia matengenezo hasa matengenezo makubwa nyumba hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu baada ya kutembelea baadhi ya nyumba hizi hasa zile ziliopo Kengeja, Pemba na sehemu nyenginezo, ilibaini kuwa nyumba hizo ziko katika hali mbaya sana na hivyo kuhatarisha maisha ya wakaazi wa nyumba hizo. Kamati inatoa wito kwa serikali kuchukua hatua ya kuzifanyia matengenezo haraka nyumba hizo, ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

CHANGAMOTO YA UPATIKANAJI WA MAJI

Mhe. Mwenyekiti, Upatikanaji wa maji safi na salama ni miongoni mwa changamoto kubwa hapa Zanzibar. Kamati yetu inaipongeza Mamlaka ya Maji na wizara kwa ujumla kwa jitihada za kutatua tatizo la maji mjini na vijijini. Halikadhalika, Kamati imefarijika kuona katika makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo kwa mwaka 2011/2012, zaidi ya shilingi milioni mia sita zimetengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pekee kwa ajili ya miradi inayolenga kuwafikishia maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar. Ni matarajio yetu kuwa fedha hizo zitatumiwa vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuona baada ya mfupi matatizo haya ya maji yanapatiwa ufumbuzi.

Mheshmiwa Spika, changamoto kubwa iliyopo sasa ni upatikanaji wa uhakika wa maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi, tatizo linalosababisha wananchi wengi kutoona umuhimu wa kulipia huduma hiyo ya maji kwa Mamlaka ya Maji na hivyo kuikosesha mamlaka mapato. Hata hivyo, wananchi hao wamekuwa wakitumia fedha nyingi kwa ajili ya kununua maji kutoka kwa watu mbali mbali ambapo wakati mwengine maji hayo huwa si safi wala salama.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inatambua juhudi za serikali za kutatua tatizo hilo hasa katika kuweka mfumo mpya wa usambazaji maji baada ya mabomba yaliopo sasa kuchakaa sana. Tunatoa wito kwa wataalam wetu na wizara kwa ujumla kuifanya kazi hiyo kwa uangalifu mkubwa ili kutimiza matarajio ya wananchi wengi, wananchi ambao walikuwa na matarajio makubwa ya

kuondokana na tazizo la maji tangu wakati wa utekelezaji wa mradi wa maji wa mkoa wa Mjini Magharibi kwa awamu ya kwanza na ya pili, chini ya ufadhili wa Japan. Kamati inaamini kuwa wizara ikiweza kutatua tatizo hili la maji, wananchi watahamasika sana kulipia huduma hiyo, hatua ambayo itaifanya Mamlaka ya Maji kuwa na chanzo kikubwa cha kusanya mapato zaidi.

HUDUMA YA KUUNGIWA UMEME KWA MKOPO

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Zanzibar mjini na vijijini wamehamasika sana kutaka kuungiwa na kutumia huduma ya umeme. Hata hivyo, gharama za kuunga umeme kwa wananchi wetu ni kubwa sana kulinganisha na kipato cha wananchi hao. Kamati yetu inatoa wito kwa wizara kupitia kwa Bodi ya Shirika la Umeme kubadili misimamo ya sera zake kuhusiana na ukopeshaji wa huduma ya kuwaungia wananchi umeme kwa njia ya mkopo, ili wananchi hasa wa kipato cha chini wamudu kutumia nishati ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaamini kuwa suala la kuwaungia umeme wananchi kwa njia ya mkopo litasaidia sana kuongeza makusanyo ya Shirika na hivyo kuimarisha uwezo wa kifedha wa shirika. Kwa mfano, umeme unaopatikana huko Pemba kutoka Tanga ni kiasi ya megawati 20 lakini kwa bahati mbaya, ni megawati 6 tu ndio zinazotumika kwa sasa na sababu kubwa ni kuwa wananchi wengi wanashindwa kugharamia uungaji wa huduma hiyo. Kwa msingi huo, Kamati yetu inatoa wito kwa wizara na taasisi zake husika, kutoa huduma hiyo ya kuunganisha umeme kwa wananchi kwa mkopo ili kuwafanya wananchi wafaidike na huduma hiyo lakini pia kuongeza wigo wa mapato ya shirika kwa kuongeza wateja wa shirika.

DENI LA TANESCO KWA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ambayo Kamati ya Baraza lako tukufu ya Mawasiliano na Ujenzi inasikitishwa nalo na imekuwa ikipigia kelele sana ni suala la deni kubwa linalofikia shilingi bilioni arobaini, ambalo Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) limelitoza Shirika la Umeme Zanzibar kufuatia kupandisha bei ya umeme kwa asilimia 168 wakati watumiaji wa Tanzania Bara walipandishiwa bei ya umeme kwa asilimia 21 pekee.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu haikubaliani na deni hilo na tunaomba Serikali itoe tamko madhubuti kuhusiana na suala hili la muda mrefu juu ya namna gani litamalizwa ndani ya muda mfupi.

CHANGAMOTO YA UPATIKANAJI WA UMEME MBADALA

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar na Tanzania kwa ujumla imekumbwa na tatizo kubwa la mgao wa umeme ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Hivi karibuni, Shirikisho la wenyeviwanda Tanzania (CTI) lilitoa taarifa ya athari ya mgao wa umeme katika sekta ya viwanda Tanzania ambapo taarifa hiyo ilieleza kuwa kiasi ya asilimia kumi ya viwanda vilisitisha shughuli zake kutokana na tatizo la umeme nchini.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2011/2012, suala la kuimarisha sekta ya viwanda limeonekana kupewa kipaumbele. Kuna haja kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujizatiti zaidi kuchukua hatua madhubuti na za haraka katika suala la kutafuta vyanzo mbadala vya kuzalisha umeme hapa Zanzibar kama kweli tunahitaji kuiendeleza sekta ya viwanda ambayo ni tegemeo kubwa katika kunyanyua uchumi wa nchi. Ni dhahiri kuwa itakuwa vigumu sana kuwashawishi wawekezaji katika sekta ya viwanda kuwekeza nchini ikiwa tutaendelea kutegemea umeme wa maji kutoka Tanzania Bara, ambao kila siku zinavyokwenda umekuwa hauna uhakika wa kupatikana kwake.

SUALA LA UCHIMBAJI WA MAFUTA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaunga mkono kwa dhati hoja ya kuitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuharakisha hatua za utafutaji na uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar, kwa maslahi ya wazanzibari. Hatua ya wenzetu wa Tanzania Bara kutafuta, kuchimba na kufaidika na gesi ambayo ni jambo la muungano, bila ya kuishirikisha kimaamuzi na kimaslahi, serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kunahalalisha hoja hii ya kuitaka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuanza hatua za utafutaji na uchimbaji huo haraka kwa lengo la kuikwamua Zanzibar kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaamini kuwa mijadala mikali inayojitokeza katika Baraza lako tukufu ambayo msingi wake hasa ni uchache wa rasilimali tulizonazo, inaweza kupungua sana baada ya kuanza uchimbaji wa nishati hiyo

ya mafuta. Tulitarajia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri tungeona mikakati kadhaa ikielezwa kutekelezwa na wizara kama matayarisho ya kuanza kwa kazi ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, hata kama kazi rasmi za utafutaji na uchimbaji hazitoanza haraka kiasi hicho, basi angalau tungeelezwa namna ambavyo vijana wetu wanaandaliwa katika fani zinazohusiana na mafuta kwa kasi zaidi, ili tutakapoanza uchimbaji rasmi, tuwe na rasilimali watu ya kutosha katika sekta hiyo ya mafuta. Katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Kiambatanisho C 2, kinaonyesha ni watu wawili tu ndio wanaopatiwa mafunzo ya muda mfupi katika masuala ya Sera ya Mafuta, ambao Kamati yetu inahisi ni kidogo sana kwa nchi inayotarajia kuingia katika uchimbaji wa mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inashauri suala la kusomesha vijana wetu katika Nyanja mbali mbali za mafuta, lipewe kipaumbele cha aina ya kipekee ili tusije kujuta pale tutakapoona wakati wa uchimbaji wa mafuta utakapoanza ni wageni ndio wanaofaidika na ajira katika sekta hiyo, kama ilivyojitokeza katika sekta ya utalii.

HITIMISHO.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inatarajia kuwa ushauri na mapendekezo iliyoyatoa kwa wizara na serikali kwa ujumla, yatazingatiwa na kufanyiwa kazi kwa kadri itakavyowezekana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012. Turejee kuwaomba wasimamizi na watendaji wote wa wizara hii, kufanyakazi kwa moyo wa kujituma, uadilifu mkubwa na kwa mujibu wa sheria na taaluma zao, kwa lengo la kuiletea maendeleo nchi yetu.

Kamati inaamini kuwa wizara ina uongozi na watendaji wanaoweza kusimamia majukumu yanayopaswa kutekelezwa kupitia bajeti hii. Kinachohitajika ni ushirikiano baina ya uongozi na watendaji wa wizara, ujasiri na kufanya kazi kwa nia njema kwa maslahi ya wazanzibari tunaowawakilisha.

Mhe. Mwenyekiti, Mwisho, kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kitope, naomba kutamka kuwa tunaunga mkono hotuba ya Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na tunawatakia utekelezaji mwema wa bajeti hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kuwasilisha.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwenzo baada ya mwenyekiti wa kamati kuwasilisha hoja yake, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuteuliwa kukamata nafasi hii muhimu naamini kwamba Rais kafanya baada ya kuona uwezo wa Mhe. Ali Juma Shamhuna katika masuala ya uzoefu na mambo yake mengine katika uendeshaji wa Wizara, naamini Mhe. Ali Juma Shamhuna kama waziri hatomuangusha Rais.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye mapitio kidogo ya bajeti ya mwaka jana kwa ufupi, katika bajeti ya maendeleo tuliambiwa kwamba mwaka jana Wizara hii ilitengewa bilioni 69 na mara hii wizara hii imetengewa bilioni 101 hapana shaka kwamba bajeti ya maendeleo kwa mwaka huu kwa wizara hii imeongezeka, lakini ilikuwa Mhe. Waziri atupe ufafanuzi juu ya utekelezaji maana yake kabla hajaomba fedha nyingizaidi ilikuwa ni vyema atueleze utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2010/2011.

Jengine katika bajeti hii ni suala la usambazaji wa umeme vijijini mwaka jana ilitengewa jumla ya bilioni 99 kama sikosei na mara hii imezidi lakini vijiji vya Pemba havikuonyesha hapa imeainishwa tu kwamba vijiji vya Unguja, sasa ni kwa sababu gani ni kwa sababu tayari vijiji vyote vya Pemba sasa hivi vinawaka umeme au ni kwa sababu gani.

Nikitoka hapo kwenye utekelezaji wa bajeti sasa niende kwenye suala la Idara ya Nyumba marehemu baba wa Taifa wa Zanzibar marehemu Shehe Abeid Amani Karume mungu amlaze pahala pema, moja kati ya dhamira kubwa ya mapinduzi ni kwa ajili ya kuwapa wananchi na kuwaweka katika makazi bora, ndio sababu marehemu akatujengea nyumba za maendeleo tunaipongeza juhudi hiyo. Mwenyezi Mungu ishaalla azidi kumuweka pahala pema.

Lakini tatizo lililojitokeza serikali hizi kwa kweli hazikuweza kuzitekeleza na kuendeleza matunda ya mapinduzi, kitu ambacho kimetupa usumbufu mkubwa sana na katika kuzisimamia nyumba zile ndio serikali ikaja na wazo la kuanzisha Idara ya Nyumba, lakini hali iko je hali ya kudhiimarisha na kuziendeleza nyumba zile ni mbaya sana, sasa katika mahitaji tuliyokuwa nayo sasa hivi kwa wananchi wetu wa Zanzibar na katika kuendeleza dhamira ya muasisi wa taifa letu nadhani sasa wakati umefika wa serikali kubadilisha utaratibu wake. Ni vyema tuondokane na kuwa na Idara ya Nyumba sasa hivi lazima tuanzishe shirika, shirika ambalo litakuwa na uwezo wa kukopa na kukopesha na ambalo litakuwa na uwezo wa kuzisimamia nyumba zile na kuziendeleza, sasa hivi wananchi wa Zanzibar wanahitaji nyumba tena ikiwezekana nyumba ambazo wananchi wanaweza kukopeshwa.

Lakini ni bahati mbaya sana zilizopo sasa hivi zinaanguka na hakuna *program* yoyote ile ya kuendeleza suala hili la ujenzi wa nyumba kitu ambacho ni mahitaji makubwa, wafanyakazi wetu hawana majumba, wanafunzi kutoka vyuoni hawana makazi. Sasa ni wakati wa serikali kufikiria namna ya kuanzisha shirika la nyumba ili liweze kutafuta mbinu na mitaji ili tujengewe nyumba zenye gharama nafuu. Idara ya nyumba sasa hivi imeshindwa kukusanya kodi hata hizi nyumba tulizokuwa nazo sasa hivi ukiangalia ripoti ya mdhibiti moja kati ya kwiri kubwa sana na serikali katika eneo hili inapoteza pesa nyingi sana, katika kukusanya kodi katika nyumba alizozianzisha muasisi wa taifa hili.

Kwa hivyo rai yangu naishauri serikali ifikirie namna ya kuanzisha shirika la nyumba ili liweze kutafuta mbinu ya kujenga makaazi bora kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye Shirika la Umeme, shirika la umeme kwa mujibu wa sera yake na taratibu zake ni shirika ambalo linafanya biashara kwa upande mmoja na kutoa huduma, kama hivyo ndivyo na shirika karibuni mwaka jana lilitengewa fedha maalum kwa ajili ya kulifanyia mageuzi ingawa mara hii hatukuiona *program ile financial turner round* ingawa mara hii hatukuiona program ile. Katika hiyo basi naomba nimuulize Mhe. Waziri moja kati ya kitu alichotwambia katika bajeti yake ni mapungufu ya Shirika katika kukusanya mapato, katueleza hapa mwaka jana kwamba Shirika lilipangiwa kukusanya bilioni 47 lakini utekelezaji wake shirika limeweza kutekeleza kwa kukusanya shilingi bilioni 24 sawa na asilimia 51.

Lakini mara hii shirika linakusudia kukusanya bilioni 57 ikiwa shirika mwaka jana lilishindwa kukusanya shs. Bilioni 47 na kukusanya nusu ya fedha hiyo kwa nini Mhe. Waziri usiweke katika kiwango hicho, kwa sababu hiyo ndio inayoonekana ndio uwezo wa Shirika kukusanya au kuna maajabu gani ambayo mwaka huu utatokea ili wafikie katika kiwango hicho. Mimi nadhani ilikuwa iangaliwa hali ya Shirika halafu kima kile kile walichoweza kukusanya ndio kiwe kile kile, labda tuambiwe kuna vitu vyengine ambavyo vinazidi.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na shirika kuwa na sera hiyo ya kutoa huduma. Tuna tatizo kubwa sana kwa vijiji vyetu. Kama nilivyosema mwanzo bado vijiji vya Pemba na Unguja vingi sana bado havijaenea huduma hii ya umeme, wananchi bado hawajafaidika na huduma hiyo ya umeme.
Wananchi wetu pamoja wakishirikiana na viongozi wao Wabunge na Wawakilishi wamekuwa wakifanya juhudi kubwa sana kuendeleza vijiji hivi kwa kuutafuta umeme. Kuna vijiji kadhaa wa kadhaa tumetafuta nguzo, nguzo tumeziweka na bahati mbaya sana nguzo sasa hivi nguzo zimeshazidi zaidi ya miaka miwili zinaendelea kuliwa na wadudu. Nini mchango wa serikali Mhe.

Waziri katika hili. Nini mchango wa Shirika katika hili. Ikiwa wananchi wenyewe tayari wameshafika hatua ya kusimamisha maguzo wakashindwa na kupata waya.

Nataka nikwambie kile kijiji changu cha Gongomawe tayari, uliniahidi utakuja hukuja. Nataka nikupe taarifa kwamba tayari umeme umeshafika Gongomawe. Kuna vijiji kadhaa katika Jimbo la Chakechake wananchi wameshapigana wameshapata nguzo lakini tatizo lao ni waya. Nilizungumza na Meneja wa Shirika nashukuru alinambia numuandikie barua, niliandika barua lakini hadi sasa kwa kweli sijapata jawabu lolote. Sikusudii kwamba alikusudia kunidanganya au kunisumbua Mwakilishi mzima, sikusudii hivyo.

Mhe. Waziri utakapokuja naiomba wizara inieleze nini mchango wao katika vile vijiji ambavyo tayari wananchi wameshapigana na wameshapata nguzo, tatizo lao ni waya. Nini mchango wa shirika na serikali katika hili.

Mhe. Naibu Spika, katika hoja hiyo kama ni Wawakilishi kwa kweli haturidhiki na juhudi za serikali katika suala zima la kuleta umeme mbadala. Umeme ndio maisha, umeme ndio uchumi, umeme ndio maendeleo. Hadi leo kama walivyosema wenzangu tunategemea umeme kutoka Bara wao wenyewe wana *crisis* kubwa sana ya umeme, kila siku mgao, ni tatizo kuweza kutegemea umeme kutoka Bara.

Hili tuliloambiwa kwamba serikali au wizara itajaribu kuwatafuta tena. Picha inayoonekana hapa kwamba kulikuwa na *initiatives* za kuweza kutafuta wawekezaji lakini baadaye zikakatika. Ndio maana Waziri ulipokuja ukasema mtawatafuta tena Waizrail, hawakuja kuwekeza.

Serikali kwa kweli haijaonesha umakini katika suala hili. Kama ni Wawakilisi sasa ni lazima tuweze kuisimamia serikali kwa sababu nchi kukosa umeme wa uhakika ni tatizo kubwa sana. Tuona mfano hapa wakati nchi ilipokuja kuingia katika matatizo miezi mitatu hali yetu tulikuwa hatuifahamu.

Sasa tunaiagiza serikali kwamba tumechoka na mtindo wa hadithi katika vitabu. Sasa tunataka kuona hatua za dhati, hatua za makusudi zikichukuliwa kuhakikisha kwamba sasa tunakuwa na umeme wa uhakika katika visiwa vyetu. Nategemea tukijaaliwa katika bajeti ya mwakani hadithi hizi zisije tena hizi. Kwa sababu Mheshimiwa ni mpya katika wizara hii kwa bajeti hii kwa kweli tutakuangalia. Tunachotaka tunasema kwamba tumechoshwa na hadithi hizi za kila siku kwamba tutafanya hivi. Mategemeo yetu kuwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja serikali itakuja na majibu juu ya suala zima la kuwa na umeme wa uhakika, umeme mbadala katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa wenzetu wa Bara wako mbali katika hili. Sasa hivi katika maeneo ya Iringa, maeneo ya Makambako tayari kuna mradi wa upepo umeshafanyiwa utafiti na sasa hivi wapo katika kazi. Tafiti zinatwambia katika maeno ya Makunduchi, Kizimkazi na sehemu nyengine na Mtambwe maeneo ya Gando ni maeneo mazuri sana ya upepo. Kwa hivyo tunahitaji tupate jawabu kamili katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho ni suala la mafuta. Serikali inajaribu kulichezea Baraza la Wawakilishi. Suala la mafuta Zanzibar utafiti wake ulifanyika mwanzo kuliko hata Tanzania Bara. Taarifa zinatwambia kwamba tafiti zilifanyika tangu kipindi cha enzi za ukoloni. Wenzetu katika masuala ya utafiti wa mafuta walianza katika miaka ya karibuni. Wameanza na sasa hivi tunashuhudia hatua, wameanza kupata gesi. Tangu mwaka 2004 watu Bara wanaendelea kufaidi tunda hili la Muungano, gesi.

Naishukuru Serikali ya Mapinduzi, Baraza la Mapinduzi limekaa likaamua na Baraza la Wawakilishi hili lilikaa, likaamua kwamba suala la mafuta halina mjadala wala suala la mafuta halina mbadala katika kuifanya serikali isiweze kutekeleza kwa ajili ya kuwatafutia Wazanzibari. Tatizo letu ni uchumi na rasilimali tayari ipo. Matatizo yetu yote ya uchumi jawabu lake lipo. Wenzetu Bara tayari wameshaanza kufaidika na mabilioni ya shilingi yanayotokana na gesi. Rasilimali ya Muungano, fedha hizo ambazo ilikuwa na sisi ni haki yetu tuzipate. Ni kiasi gani tumepata katika hizo.

Mhe. Waziri leo karudia suala hili kwamba suala hili ni la Mungano, ni kweli kuwa ni la Muungano. Jawabu lake ni kulitoa katika kero. Sisi hatukatai na hilo, hilo wacha tulitoe na limeshatoka. Maana yake mtu akisema hataki ndio hataki. Mtu ikiwa kitu ni chenu shirika akisema hataki basi maana yake hataki na akisema hataki maanaye tayari hilo lishatoka. Hakuna hata mmoja aliyetiwa pingu katika kuungana hapa, tuliungana kwa hiyari zetu. Na ikiwa ni jambo la hiyari maana yake nini? Maana yake ni kwamba chochote ambacho hatutaki kiwe cha muungano kwa sababu ni chetu kitaendela kuwa ni chetu.

Sasa katika hili inaonekana katika viongozi wetu wa SMZ hawajawa tayari na hili. Tusizunguke wala tusibabaishane hawajawa tayari na hili kuna mambo ambayo ni ya muungano lakini sisi tulipotaka kuyatoa katika muungano au tulipotaka kuyachukua sisi katika mamlaka yetu tumeyatoa. Suala la Elimu ya Juu ni suala la Muungano, lini tuliruhusiwa na Bunge sisi tutoe. Mbona sasa hivi tuna Vyuo vyetu Vikuu hapa. Suala la Bandari ni suala la Muungano lakini kwa nini tuna Bandari zetu hapa ni lini tulikwenda tukaomba ruhusa. Mimi naamini tusiwasingizie Watanganyika, tusiwasingizie watu wa Bara. Watu wa Bara hili hatujawasikia kwa sababu yote tunayoyazungumza ni masuala ya Muungano. Lini waliotwambia kwamba sisi tusiendelee na shughuli zetu

mpaka leo tukasema kuwa ndio sababu kuu inayotufanya kwamba tushindwe kulitekeleza hili.

Mwaka jana katika kikao tulipewa taarifa kwamba kuna wanafunzi kumi na tukaambiwa Wawakilishi tuwahamasishe watu wetu majimboni waombe nafasi hizi. Taarifa tunazo mpaka leo kwamba kuna wanafunzi 10 katika hizo hatua za kuona kwamba suala hili lipo katika mchakato wa utekelezaji. Niimani yetu kwamba sasa hivi kuna Wazanzibari 10 wanasomea masuala haya. Jibu lililokuja leo sijui kuna Mzanzibari mmoja sijui wawili wapo Norway sijui wapi. Kwa kweli mnatudanganya, serikali mnatudanganya.

Namuomba katika hili Mhe. Waziri atakapokuja atwambie agizo lililotolewa katika Baraza la Wawakilishi kwamba kuna Wazanzibari 10, hebu atwambie lilitekelezwa. Na kama halikutekelezwa atwambie ni kwa nini halikutekelezwa. Na ni kwa nini serikali haikurudi tena kwetu ikatwambia kwamba lile suala halikutekelezwa. Mtuachie tu tuendelee kuwa na imani kwamba kuna wenzetu. Kweli majimboni kwetu tunasema hilo, kwamba jamani kati suala la utekelezaji juu ya hili kuna wenzetu sasa hivi ingawa hatumjui nani na nani, lakini kwa mujibu wa taarifa za Baraza tunawenzetu sasa hivi wanasomea mafuta ku 10. Kumbe vile si kweli, kumbe kuna mmoja na huyo mmoja sijui mambo ya utafiti.

Huu ni ushahidi tosha kwamba serikali bado haijawa tayari na suala hili. Mheshimiwa kwa niaba ya watu wa Chakechake kwa sababu sasa tunataka kufanya kazi na kwa kuwa sasa tunataka tuione serikali kwa sababu hizi hatuko tayari kwamba tutasubiri Bunge litupe idhini sisi hatupo tayari kwa hilo. Baraza la Wawakilishi kama chombo cha wananchi kimeamua, Baraza la Mapinduzi kama ndio Serikali ya Zanzibar imeamua. Kwa maana hiyo huku taratibu zikiendelea hatujafungika sie na kuchukua hatua.

Nakusudia kuondosha shilingi mia kwa kutumia ibara ya 96(6) cha Kanuni kifungu (b) katika Idara ya Nishati, mpaka pale hitakapopewa maelezo juu ya utekelezaji wa sera hii. Kama si hivyo Mheshimiwa kwa kweli hapa leo jamaa zangu wa Kojani wanasema **"Haudundwi wala mpira hautiwi kwapani"** Mheshimiwa siungi mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikachangia hotuba hii ya Mhe. Waziri Ali Juma Shamuhuna (Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati).

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi kubwa na ngumu ambayo aliyopewa kwa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Wizara yake ni uhai wetu. Kwanza nataka nianze na jimboni kwangu. Jimbo

langu la Kwamtipura bado lina matatizo makubwa sana ya maji. Nimejaribu kuzungumza katika hotuba ya serikali, hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais na leo Mwenyewe kwa kuwa yupo nitaomba vile vile nilizungumze suala hili.

Mheshimiwa jimbo langu lina shehia tatu, Kwamtipura, Shaurimoyo na Mkele. Shihia zangu zote hazipati maji kama inavyostahili, naomba sana Mheshimiwa. Tumeona mipango ya serikali, jitihada zipo, uchimbaji wa visima 52, kuongeza nguvu ukarabati. Tunakumbea Mwenyezi Mungu akusaidie akupe wasaa ili kuweza kukamilisha haya. Mwaka huu sisemi sana. Nilisema wizara nitaipa mwaka mmoja vyenginevyo tutaomba JWTZ wafanye hii kazi. Lakini naamini Mhe. Waziri kwa ulivyojipanga safari hii tunategemea maji yataweza kupatikana.

Mimi nilikuwa na ushauri, katika mfuko wa jimbo. Wenzetu wa Bunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kule huwa wanapewa pesa kwa ajili ya maendeleo ya majimbo. Tunaishukuru Serikali ya Zanzibar tunategemea pengine ndani ya mwaka huu na sisi huenda tukapata fungu hilo. Katika fedha tulizozipata milioni 25 mwaka uliopita, milioni 13 tulitumia kwa ajili ya masuala ya maji jimboni. Baada ya kuondoa umasikini tunazidi umasikini. Kama maji yangelikuwa yanapatikana fedha zile tungezielekeza katika maeneo mengine. Ndio maana nikakuombea Mwenyezi Mungu akusaidie Mhe. Waziri ili haya tunayoyasema muyakubali ili muweze kupata fedha kwa ajili ya maji katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi.

Pili la jimboni kwangu nataka nizungumzie suala la hati miliki. Katika kutekeleza majukumu yetu kuisaidia serikali kupunguza umasikini, katika jimbo letu la Kwamtipura tumejitahidi tuna miradi mikubwa mitatu kwa mine. Tumejenga hospitali ya jimbo la Kwamtipura. Nashukuru Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, nilikuona ulikuja pale kupata huduma. Hospitali ile tumeshapimiwa lakini mpaka leo hatuna hati miliki. Niliandika barua kumuomba Katibu Mkuu lakini inaonesha pengine majukumu yamemzidi hapa nilikuwa nakumbushia.

Vile vile tuna skuli za chekechea mbili tuna Skuli ya Kwamtipura Chekechea na nyengine ipo Shehia ya Mkele pale *Government Press*. Mheshimiwa tunaomba tupatiwe Hatimiliki kwa sababu tumeshapoteza nguvu sana za wananchi ili wasijewakatokezea wajanja wakaja akawema hospitali yao na zile Chekechea ni zao. Pia jimbo langu la Kwamtipura sasa hivi tunakusudia kujenga Skuli ya Sekondari ya Ungundi ndani ya jimbo letu ni ya wananchi wenyewe. Ndio hiyo hiyo katika uisaidia serikali kupunguza umasikini. Eneo hilo Mheshimiwa lipo pale pale *Government Press* baina ya hiyo skuli ya Chekechea ninayoizungumza na *Government Press* pana uwanja pale umeshapimwa lakini bado hatimiliki hatujapewa. Ujenzi huu tunataka *once*

tukipata tu huu mfuko wa maendeleo wa Zanzibar basi mradi wa mwanzo ambao tunataka kuutekeleza ni mradi huu wa Skuli ya Sekondari ya Ufundi katika jimbo la Kwamtipura.

Nashukuru sana serikali ina miradi mengine mikubwa, serikali tayari imenisaidia mradi wa mtaro kutoka Darajabovu kupitia Mboriborini, serikali imeshaahidi kwamba itautekeleza. Lakini kwa kuwa tuna ahadi ya Mhe. Rais katika ujenzi wa barabara inayotokea kwa Abasihuseni kupitia Mboriborini mpaka Darajabovu maarufu Tawi la CUF au Makao Makuu ya Wilaya ya CUF, tunategemea kwa kuwa kuna ahadi ya Rais mradi huu utafanyika ndani ya kipindi hichi. Aidha Bajeti ya mwaka huu au mwaka ujao kwa mujibu wa hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa sasa nizungumzie suala la Kitaifa. Sisi Baraza la Wawakilishi Baraza lilopita Serikali ya Awamu ya Sita kwa kweli ilifanya kazi kubwa sana. Nakushukuru sana Mhe. Waziri katika mtu ambaye ulikuwa mahiri sana katika kutetea maslahi ya Zanzibar hasa katika suala la mafuta Mhe. Waziri ulikuwa ni wewe. Nilitegemea katika hotuba yako ungetueleza kwamba ikifika katika kikao cha Oktoba utaleta sheria ambayo itaipa mamlaka ya kuanzisha uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar. Nilijitahidi sana kukusikiliza lakini eneo hilo sikuliona. Kitu nilichoridhika ni kimoja kwa kuwema kwamba masuala ya kiuchumi si masuala ya Muungano. Serikali bado ina nia ya kuhakikisha kwamba Zanzibar tunachima mafuta.

Mheshimiwa mimi nilikuwa naomba sana mwenzangu kasema atatoa shilingi mia, mimi huenda nikaja nikazuia lile fungu la kawaida la mipango. Mheshimiwa kifungu 04 Mipango na Uendeshaji, nitakizuia. Sitaki ije iwe kama ya rafiki yangu, Sahibu wangu Mhe. Juma Duni. Mimi kauli yako Mheshimiwa itaniridhisha, kama haikuniridhisha naweza nikaja nikataka kauli kubwa zaidi.

Mheshimiwa bado tunapiga danadana suala la mafuta. Kitu tunachokiomba kwa kuwa mamlaka ya Baraza la Wawakilishi ndio mamlaka ya wananchi kwa mujibu wa Katiba yetu na Baraza la Mapinduzi limekwisha kuamua suala la mafuta liondolewe katika mambo ya muungano. *Process* iliyobakia ni kuleta sheria kuanzisha mamlaka ya mafuta Zanzibar, bila ya hivyo tutakuwa tunapiga danadana. Katika kitabu chako umeeleza mambo mengi humu lakini haya hote Mheshimiwa kama hatujakuwa na sheria hakuna kitakachoendelea. Bado wapo watu wa kutusaidia katika masuala haya ya uchimbaji wa mafuta na gesi kwa hapa Zanzibar. Sitaki niseme sana katika suala hili kwa sababu nimeshaeleza nia yangu.

Mheshimiwa faida ya mafuta ni nyingi, sisi sote viongozi wetu kila siku tunasikia wanapokwenda Falme za Kiarabu wanakwenda kuomba misaada. Waarabu hawana migomba, hawana mipapai, hawana mpunga, wanayo mafuta. Wazanzibari sisi tupo milioni moja na laki tatu pamoja na kuzaa sana tumeshaongezeka tunaweza tukafika milioni moja na laki nne. Mafuta tuliyokuwa nayo Zanzibar yanatutosha. Yakichimbwa mafuta hapa mapipa laki moja kwa siku, kwa muda wa siku 10 mapipa milioni moja. Siku kumi na tatu kila mtu anapipa lake Zanzibar la Mafuta. Tunaogopa kitu gani? Kwa hesabu za haraka hara hii miradi yote itakuwa upuuzi. Tunataka na sisi Zanzibar tuwe tunasaidia wenzetu.

Juzi Waheshimiwa Mawaziri walikuwa wemeshatumwa waende Libya wakaombe msaada. Libya sasa hivi *sakaratul mauti*, tutaomba misaada mpaka lini. Tuchimbe rasilimali tuliyokuwa nayo. Tunataka Zanzibar na sisi ndani wa Wakati wetu huu sisi kama Wajumbe wa Baraza kuna kampuni iko tayari kufanya utafiti na kuchimba mafuta ndani ya miaka mitatu. Ndani ya miaka mitatu sisi tumo Barazani bado. Tunataka tutajike na sisi Zanzibar inaisaidia Comoro, Tanzania Bara na sehemu nyengine yoyote, mafuta tunayo. Uchumi wetu tunao lakini waswahili wanasema tunaukalia.

Mheshimiwa kwa kuwa umenambia dakika zangu nitakuja kumalizia siku ya Jumatatu leo nitaomba niishie hapo kwa heshima yako na maneno yangu mengine nitakuja kumalizia Jumatatu.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla ya kuakhirisha kikao naomba kusoma tangazo lifuatalo. Tunaomba uwatangazie Waheshimiwa wanawake wote kuhudhuria katika mkutano wa kujadili maendeleo ya bajeti ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, itakayofanyika siku ya tarehe 9/7/2011 saa tatu ya asubuhi hapo katika Ukumbi wa Wizara Shangani. Baada ya maelekezo hayo kwa heshima na taadhima nachukua fursa hii kuliakhirisha Baraza hadi Jumatatu asubuhi saa 3:00.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 11/07/2011 saa 3:00 za asubuhi)